Kikao cha Saba – Tarehe 05 Oktoba, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe katika Kikao cha Baraza la Wawakilishi cha tarehe 2 Oktoba, 2017, Mhe. Hidaya Ali Makame wa Nafasi za Wanawake aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Mhe. Naibu Waziri Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi aliahidi kujibu kwa maandishi. Kwa Mujibu wa Kanuni ya 40(4) ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la 2016 sasa namuomba Mhe. Waziri Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi asome jibu la nyongeza lililoulizwa na Mjumbe huyo:

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa adhini yako naomba kusoma majibu kama nilivyotowa taarifa, wakati nikijibu swali 50 ililoulizwa na swali na nyongeza na Mhe. Hidaya Ali Makame alietaka kujua ni kiasi gani cha fedha ambazo zitatumika kuwalipa watu wanaolipia mashamba jibu la swali hilo kama ifuatavyo:-

Idadi ya wafanyakazi watakaohitajika katika kazi hiyo ni ishirini na tano (25) ni kiasi cha fedha kitakachotumika katika kazi hiyo, ni Tanzania Shilingi milioni 15, kwa mchanganua ufuatao:-

Idadi ya watu ni 15, siku sitini (60) kiasi elfu kumi (10) jumla kumi na tano elfu (15,000) Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili , Mifugo na Uvuvi , katibu kwa shughuli inayofuata.

HATI YA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuweka Mezani Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Maliasili , Mifugo na Uvuvi ya Utekelezaji ya Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa Mwaka 2016/2017. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ili naye awasilishe Hati Mezani. Kwa niaba yake namuona Mhe. Hamad Abdalla Rashid.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti naomba kuweka Hati Mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya Utekelezaji ya Maagizo ya Kamati ya Mwaka 2016/2017 Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 3

Ucheleweshwaji wa Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDF)

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: (Kny. Mhe. Abdalla Maulid Diwani): – Aliuliza:

Pamoja na Serikali kupitia mfuko wake wa CDF wa kutoa pesa za mfuko wa jimbo ili kwenda sambamba na ahadi pamoja na ilani ya Chama, kwa bahati mbaya pesa hizi zinachelewa kupatikana kwa wakati muafaka.

Ni lini Ofisi yako itaamua kubadilisha taratibu za utoaji wa pesa za mfuko wa Jimbo mara tu baada ya kumaliza uchaguzi ili Wawakilishi waendelee kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulidi Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe swali lake Nam. 3 lakini kabla naomba kutanguliza maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ni mpango maalum ulioanzishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Kupitia Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Namba 4 ya mwaka 2012 na Sheria ya Marekebisho ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo Namba 5 ya mwaka 2016 ambazo zinaelezea uanzishaji na utaratibu wote wa uendeshaji na usimamizi wa Mfuko huo kwa lengo la kusaidia wananchi katika Majimbo yao kupitia utekelezaji wa Miradi midogo midogo waliyoibua wao wenyewe.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulidi Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe swali lake Nam. 3 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza, nakubali kwamba fedha hizo ni kweli mara nyingi huwa zinachelewa kupatikana kwa wakati muafaka. Sababu kuu ya kuchelewa kutolewa kwa fedha hizo katika mkupuo wa awamu inayofuata ni ucheleweshaji wa marejesho kutoka majimboni pamoja na kuchelewa kwa uwasilishaji wa majina na nambari za Akaunti yaani Benki ya Kamati ya Maendeleo ya Jimbo.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa uzoefu unaonesha kwamba mara zote baada ya uchaguzi majimbo yetu huwa yanachelewa kuunda Kamati zao na pia Kamati zilizomaliza muda wake huwa haziwasilishi marejesho ya matumizi ya fedha zilizotolewa awamu ya mwisho kama ilivyoelekeza Sheria. Kutokana na sababu hizo Serikali imekuwa ikichukua hatua ya kuzuia utoaji wa fedha za awamu nyengine baada ya uchaguzi kwa majimbo yote ambayo yanashindwa kufanya marejesho ya matumizi ya awamu iliyopita na kuwasilisha taarifa za majina ya Kamati za Jimbo na Nambari za Akaunti ya Benki iliyopangwa kama ambavyo Sheria inavyoelekeza. Serikali itaendelea kutekeleza utaratibu wa uendeshaji wa Mfuko huo kwa mujibu wa Sheria hizo ambazo zimetungwa na Baraza hili Tukufu. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. naibu Waziri namuomba kumuuliza swali kama hivi ifutavyo:

Je Mhe. Naibu Waziri, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliwahi kupata elimu katika suala zima la urejeshaji wa fedha za Mfuko wa Majimbo kwa wakati.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, Mwakilishi wa Viti Maalum kutoka katika Mkoa wa Magharibi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kupitishwa kwa Sheria hii ndani ya Baraza hili Tukufu Wawakilishi wote Baraza la Wawakilishi waliweza kupata Semina elekezi kuhusiana na Sheria hii ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo wakati huo ilipopitishwa, hapa naizungumzia ile Sheria Nam. 4 ya mwaka 2012, kupita Sheria hii ilifika katika Baraza hili Tukufu Waheshimiwa Wawakilishi walipata fursa ya kujadili, wakapata semina elekezi mpaka wakaridhia wakaweza kuipitia. Kwa hivyo tunaamini fika Mhe. Spika, katika Baraza hili wakati Sheria hii inatungwa kulikuwa kuna semina iliyotolewa kwa Waheshimiwa Wajumbe, lakini pia hata ukitizama marekebisho wa ile Sheria Nam. 5 ya 2016, nayo pia ilitoa fursa kwa wajumbe kuendelea kujenga uwelewa wakati wanapitia marekebisho ya sheria hiyo.

Kwa hivyo Mhe. Spika, sisi tunaendelea kuamini kwamba semina ya awali ya kisheria imetolewa lakini hata hivyo ofisi yangu imekuwa ikiwasisitiza Waheshimiwa Wawakilishi wenye majimbo na kamati zao kufanya hivyo na kufika ofisini pale ambapo wamekuwa wakihitaji maelekezo mengine na tumekuwa tukifanya hivyo kwa yale majimbo ambayo yamekuwa yamefika. Lakini pia Mhe. Spika, ofisi yangu imeweza pia kufanya semina maalum kwa wajumbe wa kamati hizi za maendeleo wa majimbo husika katika majimbo yote ya Unguja na Pemba. Kamati zote hizi wajumbe wake wameweza kupatiwa semina hii nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika kwa kunipa nafasi ya kuuliza suali dogo la nyongeza lakini nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini katika majibu yake Mhe. Waziri alisema tatizo kubwa ambalo linawakabili Serikali kutupa fedha Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo hizi za CDF ni kutorejesha kwa wakati. Lakini yako majimbo yanarejesha kwa wakati sasa kutegeneza hukumu kwa wote wakati si sahihi lakini naomba nimuulize yeye anijibu ni kwa nini serikali au wizara yake isiweke utaratibu kwa wale ambao wamerejesha kwa wakati, wakapewa fedha hizi ili waweze kuendelea na shughuli zao.

Lakini la pili Serikali kuendelea kufanya hivyo kwa kuwahukumu wote hawaoni kuwa kuna majimbo ambayo yamerejeshwa kwa wakati, watakuwa hawajawatendea haki inayostahiki kisheria.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni swali lake (a) (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kwanza nieleze furaha yangu kwa swali hili kuulizwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa kwa sababu Mhe. Miraji ni Mwenyekiti wa PAC yeye alikuwa anayaona matatizo aliona wakati wa Kamati, lakini utaratibu wa kutoa pesa hizi kwa serikali ni mfumo tunapoweza ku-*release* pesa hizi tunatoa katika majimbo yote. Tabu inapotukuta pale ambapo tunapoweza kutoa kwa awamu na changamoto inayotukuta inaikuta sisi tunaotoa pesa hii. Kwa mfano, wakati tunatoa pesa kuanzia mwezi wa tatu 2017 tumejikuta mpaka jimbo la mwisho tunatoa pesa Mhe. Spika, kunako mwezi wa saba.

Kwa nini tumefikia mwezi wa saba, tumefikia mwezi wa saba kwa sababu kuna baadhi ya majimbo kuna matatizo ambayo nimeweza kuyaainisha katika jibu langu la msingi, sasa matatizo yale yanapelekea wakati mwengine usumbufu kwa wananchi husika ambao wanahitaji maendeleo kupitia pesa za mfuko wa jimbo.

(b) Lakini pili tumepokea wazo lake tutatizama utaratibu mzuri itakapobidi watu hawa kwa kuweza kuwa-*categorize* wale ambao watawahi kule kurudisha mrejesho tutatizama, tunaweza tukatoa kipaumbele kwa ambao wamewahi na wale ambao wamechelewa tutaendelea kuwastahamilia kwa mujibu wa sheria, hasa ukisoma sheria ya *section* 25 ndani ya sheria yetu ya Mfuko wa Jimbo nakushukuru Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Spika, nakushukuru sana mimi nitaomba niulize maswali (a) na (b) kwa Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

(a) Kwanza masuala yangu mimi mepesi sana, hizo fedha wanazoziongea za mfuko wa jimbo wanazo au hawana tungependa kujua.

(b) Kwa kuwa Mhe. Miraji Khamis Mussa kauliza swali zuri sana kwa wale ambao waliorejesha marejesho vizuri kabisa kwa wakati bado swali Mhe. Naibu Waziri hajalijibu vizuri, sisi tunataka tujue tuliorejesha mapema kwa vielelezo kamili fedha watatupa mapema au watasubiri mpaka wamalize wote watupe mwisho.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy, Mwakilishi wa Jimbo la Chaani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Serikali pesa zakuzitoa katika majimbo haya inayo na mpaka sasa Serikali kupitia Wizara ya Fedha, pesa kwa mwaka 2017/2018 katika bajeti hii tayari zimeshatengwa. Tutaanza kulifanya hilo mara tu baada ya kupata lakini Mhe. Spika, tunakichosema hili mpaka sasa katika zile pesa ambazo tumetowa katika mwaka 2016/2017 kuna majimbo manne tu ambayo yameleta mrejesho. Kwa tukianza kutoa kidogo kidogo hivi Mhe. Spika, wakati mwengine inatupa wakati mgumu tunaendelea kuwasisitiza Waheshimiwa Wajumbe tunaomba sana Waheshimiwa wajumbe tumepewa pesa za maendeleo tumezitumia tulete *return* kwa mujibu wa sheria yetu sisi tunachokifanya ni utekelezaji wa sheria iliyopitishwa na Baraza hili tukufu hatuwezi kutumia njia nyengine. Kwa hiyo tunawaomba Waheshimiwa wa majimbo husika watuletee mrejesho watakapoleta mrejesho sisi tutatizama katika majimbo yetu 54 tuliyokuwa nayo mpaka sasa Mhe. Spika, ni majimbo manne tu, sitaki kusema kwamba la Chaani limo au halimo lakini Mhe. Spika, ni majimbo manne kwa hivyo tunawasisitiza wenzetu watuletee hii pesa wafanye mrejesho tunawaingizia pesa katika mwaka wa fedha 2017/2018 nakushukuru Mhe. Spika.

Nam. 116

Nafasi za Ajira kwa Vijana Wanaomaliza Mafunzo ya JKU

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma - Aliuliza:

Serikali ya Jamhuri ya Muungano imekuwa na utaratibu wa kuwachukua vijana wake na kuwaweka (JKT) na wakimaliza mafunzo yao huwaweka malezi na zinapotokea nafasi za ajira Serikalini wao hupewa kipaumbele kwa mujibu wa sifa zao tofauti na Serikali yetu kwa vijana wanaopitia JKU ambao huachiwa kurudi mitaani na kuchukuliwa wengine wasiopita huko.

Je, Serikali ina mpango gani wa ziada kwa vijana wale tunaowaweka jeshini kwa miaka miwili au zaidi na baadae kuwaruhusu mitaani bila ya kuwapa mtaji.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma Mwakilishi wa Viti Maalum kupitia Vijana swali lake Nam. 116 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, malengo makuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuweka vijana wa kizanzibari katika Makambi ya JKU ni kuwafunza maadili mema pamoja na kuwa wazalendo kwa nchi yao.

Mhe. Spika, hivyo vijana wanaomaliza elimu ya Sekondari na vyuo ni vyema wakajiunga na JKU kwa kipindi cha miaka miwili, kwani vijana wanapokuwa makambini wanapata fursa ya kuelimishwa mambo mbali mbali ya kizalendo ikiwemo somo la uraia na mapenzi kwa kuipenda nchi yao. Aidha, vijana hufundishwa kazi za mikono kwa mfano kilimo, useremala, ufundi na ushoni ili wapate kujiajiri mara wanapomaliza mafunzo yao.

Mhe. Spika, kwa hivi sasa JKU haijaanza kutoa mitaji kwa vijana hao, isipokuwa huwafundisha ujasiriamali na namna ya kujikusanya na kutafuta mitaji kutoka vyanzo vyengine nje ya JKU.

Mhe. Spika, suala la ajira halina uhusiano wa moja kwa moja kwa vijana kujiunga na JKU, isipokuwa ni miongoni mwa vipaumbele katika kuajiriwa. Kwa mujibu wa sheria Nam. 2/2011 ya Utumishi wa Umma kifungu cha 57(3) (a) (b) na (c) kumewekwa utaratibu wa ajira kuwa ajira zote lazima zitangazwe na kila mwenye sifa anastahiki kuomba na kwa aliyekamilisha vigezo anastahiki kuajiriwa pasi na kuzingatia kama amepita JKU au la kutokana na uwezo huo wa kisheria imepelekea kuwa JKU kukosa nguvu ya kulisimamia suala hili.

Mhe. Spika, kwa msingi huo lengo la Serikali ni kuelimisha vijana na baadae vijana hao waweze kujiajiri. Hata hivyo, ikitokea fursa ya kuajiri basi vijana hao huajiriwa, kwa mfano mwaka 2015/2016 kati ya vijana 1200 waliomaliza mafunzo ya JKU ni vijana 162 waliopatiwa ajira katika Taasisi mbali mbali za ulinzi na usalama za SMZ na SMT. Aidha, kuanzishwa kwa Shirika la Uwakala la Ulinzi la JKU, litawezesha kuajiriwa vijana wengi wanaomaliza JKU. Pamoja na hayo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ inawasiliana na Wizara inayohusiana na maendeleo ya vijana kutafuta uwezekano wa kuwasaidia vijana hao mara tu wanapomaliza JKU ili waweze kujiajiri wenyewe. Ahsante.

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Spika, kutokana na majibu ya Mhe. Waziri majibu mazuri ya kututia moyo na kutujenga imani vijana nilikuwa nataka kumuliza swali dogo tu la nyongeza. Je Mhe. Waziri, wizara haioni kama sasa hivi ipo haja ya kuweza kuwapatia mitaji vijana wale ili wakitoka waweze kujiajiri wenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ inaona haja na umuhimu wa kutafuta namna ya kuwapatia vijana mitaji na nilipokuwa nikijibu suala langu mama nilisema hivi sasa tunawasiliana na Wizara ya uwezeshaji ili kuona jinsi gani atunaweza kuwapatia mitaji vijana hawa.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mhe. Waziri, lakini awali nimpongeze sana kwa majibu yake mazuri juu ya suala mama ambalo ameuliza Mhe. Salha.

Mhe. Spika, swali langu lina sehemu (a) na (b) pamoja na majibu mazuri Mheshimiwa ameeleza kwamba vijana wanaokwenda JKT miongoni mwa mafunzo ambayo wanayapata ni yale ya kuwajenga kiuzalendo, lakini sio vijana wote wanajengeka kiuzalendo wengine wanamaliza miaka yao miwili lakini ule uzalendo haujajengeka.

a) Je, hatuoni vijana hawa kubaki mitaani kwa miaka mingi inaweza wakashawishiwa na wakaweza kujiingiza katika vikundi vya ugaidi ambavyo hivi sasa vimetanda katika nchi za ukanda wa Afrika ya Mashariki.

b) Amezungumzia juu ya suala la wakala wa ulinzi ambao zaidi amelenga wale JKU, Je, kwa vijana hawa ambao wamemaliza JKT hatuoni nao waingie katika suala hili la kupata ajira itakapoanza hii wakala wa ulinzi.

Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ :

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuaavyo:

a) Kwanza msingi mkubwa kama nilivyosema vijana ni kuwafundisha uzalendo na kazi nyengine za amali, sasa vijana kuwepo mitaani na kuanza kujihusisha na shughuli nyengine zisizotarajiwa kama zile alizozitaja za ugaidi, hiyo ni akili ya mtu mwenyewe, fikra na mawazo aliyonayo lakini lengo la kuwafundisha uzalendo maana yake ni kujiepusha na mambo maovu kwa nchi na suala la ugaidi ni suala ovu kabisa na nchi yao.

Kama nilivyosema Serikali ina lengo zuri la kuweza kuwafunza vijana hawa sasa kama wapo ambao wanaingia katika mikondo hiyo basi si lengo la Serikali kuwafundisha uzalendo na ukakamavu halafu mafunzo hayo wakenda wakayatumia kinyume na sheria na taratibu za nchi. Wale ambao pengine watabainika kujihusisha navitendo hivyo basi Serikali haitasita kuweza kuwachukulia hatua.

b) Tumeanzisha uwakala wa ulinzi na tunatarajia vijana waliopo JKU kuwachukua katika kikosi hichi cha uwakala wa ulinzi, hatuoni kwamba na vijana Walioko JKT nao

wakapata fursa hii. Kwa kweli vijana wanaokwenda JKT na wanaokwenda JKU wote wanakwenda kwa lengo moja na kusudio moja la Serikali zetu zote mbili, kwa hivyo kama kuna kijana ambae amekwenda JKT au amekwenda JKU hawa wote wanayo haki ya kuweza kupata fursa katika fursa ya ajira kwenye vikosi vya ulinzi na usalama.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mimi kwanza niipongeze Serikali kwa azma nzima ya kuwaweka vijana katika makambi na kujua wajibu wao kwa hatima ya nchi yetu na kuwa watarajiwa wema katika kulinda nchi yetu na kujua ubaya wa uhalifu usitokee katika maeneo yetu. Lakini kwa kuwa nia ya JKU ni kuwakusanya vijana kuwaweka pamoja kwa ajili ya kupata kazi mbali mbali katika sehemu mbali mbali.

Je, kwa kuwa kuna huu uwakala wa ulinzi kupitia JKU nafikiri hii itakuwa ni changamoto kubwa ya kuondoa matatizo ya ukosefu wa ajira katika sehemu za mahoteli au ulinzi sehemu mbali mbali, Mhe. Waziri kwa kuliangalia hili kama kuna sera imetungwa au inataka kutungwa sera hiyo imefikia wapi mpaka sasa hivi, ili vijana hawa wawekwe pamoja na kuweza kupatikana pindi inapotokea sehemu ya ulinzi wawe rahisi kuwapata.

Mhe. Waziri Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza napenda nimfahamishe Mhe. Mwakilishi na Wajumbe wa Baraza hili katika Baraza lililopita Serikali ilileta Mswada wa Sheria na tukatunga Sheria ya Uwakala wa Ulinzi wa Uwekezaji na Utalii, Sheria ile inawataka waekezaji wote wa aina zote kufika katika uwakala wa ulinzi na kupata walinzi wa uhakika kwa ajili ya kulinda ule uwekezaji uliopo ndani ya nchi yetu, hivi karibuni tu Mhe. Rais amemteua Mkurugenzi Mtendaji na tayari amemteua Mwenyekiti wa Bodi wa Uwakala wa Ulinzi na tayari wapo wanafanyakazi si muda mrefu na mimi nitapata nafasi ya kuwateua Wajumbe wa bodi ili zile *process* za Uwakala wa Ulinzi ziweza kufanya kazi ahsante sana.

Nam. 32

Umuhimu wa Sheria ya Ndoa

Mhe. Suleiman Sarhan Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajitahidi katika kuleta usawa, haki na kuondoa uonevu wa kijinsia. Lakini katika jamii kumekuwa na uonevu kwa mke na watoto pindi inapotokea kutokuelewana kwa wana ndoa na mwisho kuachana au talaka.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka sheria ya kugawana mali baada ya kuachana (talaka).

(b) Serikali ina mpango gani wa kuwapatia haki zao mke na watoto baada ya mume au baba watoto kuwatelekeza kimaisha.

(c) Je, Serikali haioni chanzo cha watoto wa mitaani ni baba kutekeleza familia yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kama inavyoeleweka kwamba, Ndoa zote za Kiislamu, zinaongozwa na sheria ya Dini ya Kiislamu (Qur-an na Sunnah). Aya ya 241 ya Suratul Albakra inasema kwamba:-

"Wanawake waliopewa Talaka baada ya kuingia harusi wana haki ya kupewa mali ya kuwaliwaza wapewe kwa kadri ya uwezo na umasikini wa mume huyo''

Aidha, Mswada wa Sheria Mpya ya Mahkama ya Kadhi ya 2017, Mswada ambao tumeujadili na kupitisha siku ya Jumatano tarehe 27/9/2017 imeipa uwezo Mahkama ya Kadhi kushughulikia masuala yote ya kimadai na kesi zote ambazo wadawa ni waislamu. Hivyo, Sheria zote hizo zinaruhusu mgawanyo wa mali baada ya kuachana ilimradi tu utaratibu wa kisheria ufuatwe.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika jawabu (a) kwamba masuala ya ndoa za Kiislam yanaongozwa na Sheria za Dini ya Kiislamu, na iwapo Baba/Mume ametelekeza familia yake, mlalamikaji anatakiwa aende katika Mahakama ya Kadhi ili malalamiko yao yapatiwe ufumbuzi wa Kisheria. Sambamba na hilo sheria ya kuwalinda wajane na watoto ya 2005 imeeleza wazi wajibu wa baba kutoa matunzo kwa mjane na watoto.

(c) Mhe.Spika, kuna sababu nyingi zinazopelekea kuongezeka kwa watoto wa mitaani ikiwemo hiyo aliyoisema Mheshimiwa Suleiman ya kwamba kutelekeza familia yake. Mbali ya sababu hiyo zipo sababu nyengine ikiwemo, mmong'onyoko wa maadili, kuwachana kwa wanandoa na kupelekea kusambaratika kwa watoto, ugumu wa maisha na sababu nyingi nyenginezo. Katika kulitafutia ufumbuzi suala hilo, wizara yangu kupitia Afisi ya Mufti inaendelea kuelimisha jamii juu ya athari za Talaka na kuepuka ongezeko la watoto wa Mitaani.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa aya za Qur-ani alizothibitishia lakini pamoja na hayo hili tatizo limekuwa kubwa sana la watoto wa mitaani na talaka ambazo hazishi sababu.

Sasa mimi namuuliza Mhe. Waziri kwamba kuna sheria za dini na kuna sheria za Serikali katika nchi zetu, Je, kwani dini inakataa kutunga sheria ndogo ndogo au kanuni za kukazia haki au kuweza kumpatia haki wale ambao wamefanyiwa dhulma.

Lakini (b) kuna watoto wanazaliwa nje ya ndoa wengine wanasema watoto wa haramu wengine wanasema ni watoto wa nje ya ndoa, Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapatia haki zao watoto wale kwa kupitia DNA.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c).

a) Mhe. Spika, kama nilivyotoa maelezo yangu katika swali mama ni kwamba kawaida dini ya kiislam huwa inatoa muangaza katika kutoa haki za watu zikiwemo haki za watoto, tunapoisoma Qur-ani kuna aya mbali mbali ambazo inasisitiza kwamba watoto wapewe haki zao. Kwa minajili hiyo niseme kwamba Qur-ani yenyewe haijakataza kwamba zisiwepo haki za watoto kwa maana ya sheria ndogo ndogo zisiwepo, lakini inasisitiza zaidi kwamba watoto walindwe kwa hivyo kulindwa kwa watoto kuna taratibu zetu sisi wenyewe binaadam kutunga sheria mbali mbali. Kwa hivyo Sheria ya Kiislam inasisitiza zaidi kwamba watoto walindwe kwa hivyo hakuna ubaya kwa maana hizi sheria zetu kuwalinda hawa watoto na ndio maana tuna sheria mbali mbali ambazo zinalinda watu mbali mbali, wakiwemo hao watoto.

b) Mhe. Spika, kidini au Dini ya Kiislam nadhani iko wazi imetoa maelezo mazuri tu namna ya hawa watoto ambao wanazaliwa nje ya ndoa, kidini ya kiislam lakini sambamba na hilo hakuna ubaya wewe baba ambae utakuwa umechangia suala lile kutokezea kumsaidia kama binaadamu wa kawaida, hiyo iko wazi kama binaadamu wa kawaida anatakiwa kumsaidia hilo. Lakini tukienda Kidini kuna utaratibu wake maalum ambao naamini nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi mnauelewa vizuri zaidi.

Nam. 82

Changamoto Wanazopata Waekezaji Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Pamoja na kazi nzuri wanayofanya Mamlaka ya Ukuzaji na Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar *(ZIPA)* za kuharakisha maendeleo ya uwekezaji Zanzibar, bado kuna changamoto kadhaa waekezaji wanakumbana nazo kupitia Taasisi nyengine za Serikali kama vile Ardhi na Mazingira n.k ambazo huwasumbua waekezaji na kurudisha nyuma juhudi za Serikali kuu katika Sekta ya Uwekezaji.

(a) Je, kwanini Waekezaji wanasumbuliwa na baadhi ya Taasisi za Serikali kama zilizotajwa hapo juu wakati suala la uwekezaji ni muhimu kwa nchi yetu.

(b) Je, Serikali inasaidia vipi Waekezaji wanaosumbuliwa na Taasisi hizo ili miradi wanayotaka kuanzisha isikwame.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82 lenye vipengele (a) na (b) kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza, ni muhimu kuelewa kuwa ukiacha Sheria ya Uwekezaji, masuala ya uwekezaji yanaongozwa pia na Sheria nyengine kadhaa ikiwemo zinazosimamia masuala ya Ardhi, Mazingira, na mara kadhaa Sheria inayohusu Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe. Taasisi zinazosimamia Sheria hizo nazo zinapaswa kusimamia vyema Sheria hata pale inapohusu uwekezaji. Hata hivyo, kasoro zozote zinapojitokeza ni vyema zikaratibiwa pamoja ili kufanikisha azma njema ya Serikali ya kuvutia uwekezaji nchini.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Waekezaji hawasumbuliwi na Taasisi za Serikali. Kilichopo ni namna tu Sheria zinazoongoza masuala mbalimbali zinavosimamiwa utekelezaji wake ambao mara nyengine hauendani na matakwa ya Waekezaji na hivyo kuleta dhana ya usumbufu.

(b) Mhe. Spika**,** Serikali imekuwa ikiwasaidia waekezaji kupitia uratibu wa *ZIPA.* Aidha, inapobidi Serikali huunda Kamati au Timu za watendaji au hata Mawaziri kushughulikia masuala tofauti yanapojitokeza kutegemea uzito wa jambo lenyewe na utatuzi unaohitajika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya kusikitisha kwa mara ya kwanza kwa Mhe. Waziri leo ambaye sina mashaka na utendaji wake nisikitike sana na ninaposema masuala yafanyieni kazi, ilikuwa nisi-*declay interest* lakini kuna msemo shika shika na mwenyewe uko nyuma itabidi ni-*declay interest* niseme maana yake nido yamenikuta mimi hata nilikuwa sitaki kutumia chombo hichi kwa ku-*declay interest.*

Mhe. Waziri kama kuna mtu aliyeathirika katika Serikali mmoja ni mimi kuna waekezaji ZIPA kibali dola 1000, hakuna kibali cha ujenzi kuliko ZIPA dola 1000 moja, ku-*register* kampuni karibu 2000 na *registation* imefanyika na taasisi zote za Serikali ziliitwa pale na Mkurugenzi Mkuu Salum, kama kuna mtu anastahiki kupata pongezi katika nchi hii katika waekezaji Salum na nipelekee salam, kazi kwa Salum hailali ikafika siku ya pili unapata jawabu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa majibu haya hayakuridhisha mimi mwenyewe nimeathirika nimechukuliwa pesa zangu hakuna kinachoendelea ….

Mhe. Spika: Mhe. Jaku swali lako ni nini?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Swali langu lini Serikali itajipanga kuwa makini kwa waekezaji kama nchi nyengine zilivyo, tukatumia mkono mrefu baada ya mkono mfupi hilo la kwanza.

Lakini la pili. Mhe. Waziri kuna waekezaji watano wanatafuta vibali sasa hivi vilipokuwa vinatoka ZIPA hakuna usumbufu sasa kufika huko Ardhi wanafanya mazoezi bila ya kutaka ya kupanda ngazi na kushuka, Je, lini mtawapumzisha waekezaji hao baada ya kulazimishwa kufanya mazoezi kwa nguvu bila ya hiyari yao.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kama nilivyosema mwanzo uwekezaji nchini unasimamiwa na Sheria, Sheria ambazo zimetungwa na kupitishwa na Baraza hili ni vyema sana Mhe. Spika, waekezaji wote wa ndani na nje wakafuata sheria zilizopo, nasema kwamba pale yanapotokea matatizo Serikali mara nyingi sana inafanya utaratibu wa kutatua matatizo hayo, ama huundwa kamati kwa ajili ya kushughulikia lile tatizo linalohusika. Lakini la msingi la mwanzo ambalo linahitajika ni kwa waekezaji kufuata sheria zilizopo ama ziwe za ardhi kuomba vibali vya uhamiaji na kazi, masuala ya ulipaji wa kodi haya ni mambo ya msingi kwa muwekezaji kuyafuata, sasa pale ambapo hayafuatwi ndio mara nyingi huwa yanatokea matatizo yanayohitaji sasa Serikali kuyaingilia na kuyatafutia ufumbuzi.

Kwa hivyo mimi ningewashauri waekezaji wote wakasoma taratibu zetu, wakasoma muongozo wa uwekezaji uliopo na hivi karibuni umepitishwa muongozo mpya ili kuondokana na usumbufu huo. Lakini hili suala la kutoa huduma na kuwaepushia waekezaji kwenda katika eneo moja na jengine kufuata huduma hizo, hivi sasa serikali inaandaa utaratibu wa kuwa na kituo kimoja cha kutoa huduma kwa waekezaji, *One Stop Centre.*

Hivi karibuni kama Mhe. Mjumbe alifuatilia tulikuwa na semina kubwa ya watendaji wote wanaohusika wa taasisi zote, kulizungumza suala hili. Wizara tayari imeunda timu ya kuweka vizuri ndani ya wiki mbili tunatarajia *concept* ya *One Stop Centre* itawasilishwa serikalini kwa ajili ya kujadiliwa na kupata muongozo. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Spika: Hapana Mhe. Jaku. Mhe. Hamza Hassan Juma, swali la nyongeza.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii ili kumuuliza swali moja la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Spika, mimi nampongeza sana Mhe. Jaku Hashim kwa kuona hii kadhia iliyokuwepo katika suala la usumbufu kwa wekezaji wetu wa ndani pamoja na wa nje. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa kijibu swali alisema, waekezaji wanapaswa kufuata sheria za nchi, sheria za mazingira, sheria za ardhi pamoja na sheria za *ZIPA* ili kuwekeza uwekezaji wao. Mhe. Spika, nina ushahidi kuna waekezaji ambao wameshapata vibali vya mazingira, lakini mpaka leo *ZIPA* wanashindwa kutoa *certificate* ili kuweza kupata hati ya ardhi. *(Makofi)*

Lakini vile vile nina ushahidi kuna waekezaji hawana vibali vya mazingira, hawana *lease* lakini wameruhusiwa kuwekeza miradi yao. Sasa huu ni ukiukwaji wa sheria, lakini vile vile ni ubinafsi katika utendaji wa kazi. Mhe. Waziri nataka atuthibitishie je, tukimpa ushahidi huo ataweza kuusimamia ili hao waekezaji waweze kupata haki yao ya uwekezaji, ili kuondoa urasimu na usumbufu katika nchi yetu kwenye uekezaji?

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, narudia kusema kwamba upo muongozo na muongozo huo unahitaji kufuatwa na waekezaji wote.

Mhe. Spika, lakini mazungumzo au suala la Mhe, Hamza Hassan kidogo linapingana na la Mhe. Jaku Hashim. Mmoja anasema *ZIPA* inafanyakazi vizuri, mwengine anasema *ZIPA* hiyo hiyo ina kasoro. Kwa hivyo, ningeomba Waheshimiwa Wajumbe mkatupa hasa, nini *assessment* yenu katika chombo hiki. Kwa sababu mawili yanapingana. Nilitaka hilo niliweke wazi kwa sababu yamepingana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ninachoamini mimi ambaye ndiye msimamizi wa chombo hiki kwamba *ZIPA* inafanya kazi zake vizuri na kwa mujibu wa sheria iliyowekwa. Pale inapotokea tatizo, basi ni vyema Waheshimiwa Wawakilishi mkatuarifu kwa mapema kwamba hili tatizo lipo, na nimesema kwamba serikali linapotokea tatizo basi haiachi kuchukua hatua. Tutalichukulia hatua sasa, kama lipo tatizo ambalo mmeligundua, kuna watu wamepewa vibali vya mazingira lakini *ZIPA* hawajatoa *Certificate of Investment* basi tuambieni, lakini ndani ya utaratibu kwamba *ZIPA* inatoa *Certificate of Investment* tuambieni. Lakini ndani ya utaratibu kwamba *ZIPA* inatoa *Certificate of Investment* ndani ya kipindi cha wiki tatu, hiyo iko kwa mujibu wa muongozo ambao tumeuweka, sasa kama liko tatizo tuarifuni tutalifanyia kazi hilo tatizo lilokuwepo. *(Makofi)*

Nam. 58

Maslahi Madogo ya Walimu Waliomaliza Diploma ya Elimu Mjumuisho

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Aliuliza:-

Mhe. Spika, baada ya Serikali kuanzisha elimu mjumuisho kwa lengo la kuwajumuisha wanafunzi wote wale wenye mahitaji maalum na wale wasio na mahitaji maalum, walimu wengi walikuwa na hamasa ya kujiunga na Chuo cha Kiislam ili kujiunga na cheti cha "*Inclusive*" au Diploma. Hata hivyo, hivi sasa walimu wengi wamerudi nyuma kujiunga na Diploma hiyo kutokana na Wizara kutokuzingatia maslahi ya walimu waliomaliza Diploma Chuoni hapo.

Je, ni sababu gani zinazopelekea walimu waliomaliza Diploma ya "*Inclusive*" kutokuongezewa posho kulingana na elimu yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa ufafanuzi kuwa, Chuo cha Kiislamu cha Mazizini, kinatoa mafunzo ya elimu mjumuisho kwa ngazi ya Cheti tu, na Diploma ya Elimu Mjumuisho inatolewa katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Katika taratibu za Utumishi wa Umma hakuna taratibu za mtumishi kusoma cheti kwa mara ya kwanza na baadae kujiunga na masomo ya cheti chengine na akarekebishiwa mshahara wake kwa kupewa mshahara wa ngazi ya juu.

Hata hivyo, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, inalifanyia kazi suala hili kwa kuwasiliana na Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, juu ya namna ya kuwapatia haki zao. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, ningependa kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Je, ni lini mawasiliano hayo baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora yamefanyika, na ni hatua gani za mawasiliano hayo yalivyofikiwa hadi sasa?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, mawasiliano hayo yamefanyika kitambo na kwa sasa hatua iliyofikia na kuweza kuzungumza zaidi na Mamlaka nyengine, kwa mfano Wizara ya Fedha na Mipango ili kuona haki zao zinapatikana.

Mhe. Spika, niseme kwamba kwa mujibu wa taratibu za utumishi ziliopo, walimu hawa wanastahiki kupewa haki yao, hasa katika kifungu cha 82(i)(ii) inaeleza wazi wazi, kwamba mfanyakazi ambaye anakwenda masomoni na atakaporudi masomoni, kwa mfano cheti, akirudi na cheti basi anapandishwa ngazi kwa mfano alikuwa hana. Mfanyakazi wa digirii akienda kusomea *Master* halikadhalika. Sasa hawa walikwenda katika masomo ya cheti na tayari wana cheti. Kwa hivyo, ina maana kanuni niliyoitaja nukta mbili, inasema watu hawa hupewa, wanaita *increment* moja na nusu kila mwaka wanasoma na hili linafanyiwa kazi hasa.

Nam. 60

Kutafuta Ajira za Ughaibuni Kwa Vijana

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Aliuliza:-

Kutokana na tatizo la ajira ambalo linaikabili Zanzibar kama zilivyo nchi zinazoendelea, vijana wengi wamekuwa na utaratibu wa kuondoka nchini kwenda kutafuta ajira hasa katika nchi za Arabuni. Hata hivyo, vijana hao wamekuwa wakipata matatizo makubwa wanapokuwa katika nchi hizo za kigeni na katika siku za hivi karibuni raia kutoka Tanzania, Kenya na Burundi wameripotiwa kufanyiwa vitendo vya kikatili na baadhi yao kuteswa hadi kufa.

(a) Je, Serikali inazo habari za vitendo hivyo vya ukatili wanavyofanyiwa vijana hao.

(b) Serikali imechukua hatua gani katika kuwalinda na kuwasaidia vijana wetu.

(c) Kwa kuwa safari za vijana hao kwenda nchi za nje huratibiwa na mawakala, je Serikali ina makubaliano yoyote na Mawakala hao.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa heshima na tadhima naomba nichukuwe nafasi hii sana kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi ya kuweza kukutana tena leo. Lakini pia nichukuwe nafasi ya kuweza kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 60 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, imekua ikipokea habari kupitia vianzio mbali mbali zinazothibitika na zisizothibitika, kuhusiana na vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa baadhi ya vijana hao. Kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 ni kesi moja tu tuliyoipokea na kuthibitika ambayo ni mfanyakazi wa kike nchini Dubai kwa tukio linalosemekana amegongwa na geti, tukio ambalo linaendelea kufanyiwa uchunguzi. Matukio mengine yanayosambazwa na vyombo vya habari hatuna uthibitisho rasmi.

(b) Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, inachukua hatua zifuatazo katika kuwalinda na kuwasaidia vijana wetu.

i. Kuanzisha mtandao wa Mawakala wa Ajira waliosajiliwa na serikali baina ya Tanzania na Oman, ambapo Mawakala hawa ndio wanakuwa dhamana kwa vijana waliopata ajira.

ii. Kuweka kumbukumbu za kila muajiri na mfanyakazi wake, ili ikitokea tatizo taratibu za kisheria ziweze kuchukuliwa.

iii. Ofisi za Kibalozi za Tanzania hutuma kwetu taarifa zinazohusu muajiri, muajiriwa, wakala waliopitia, namba ya simu ya muajiri, nambari ya mkataba, pasipoti namba ya muajiriwa na nambari ya risiti iliyolipiwa ubalozini ili tuweze kuhakiki na utambuzi na kuwaruhusu kwenda kufanyakazi nje ya nchi.

iv. Maofisa wa wizara kupitia Idara ya Ajira walishafanya safari kikazi, kwa baadhi ya nchi za kiarabu kufuatilia wafanyakazi wetu na kujenga mahusiano mema na nchi husika.

(c) Mhe. Spika, ndio maana serikali kupitia wizara ina mashirikiano na Taasisi za Wakala binafsi wa ajira, ambazo zinafanya kazi hiyo kwa kuwapeleka vijana nje ya nchi kufanya kazi.

Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa: Ahsante Mhe. Spika, kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri tegemeo la wanawake. Nilitaka kujua tu ni vikundi vingapi vya hao mawakala ambao mmevisajili kwa hapa Zanzibar vinavyowapeleka vijana wetu nje.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba nilichukuwe swali hili, kwa sababu hivi karibuni kutokana na matukio mbali mbali ambayo yamekuwa yakitokea, kuna baadhi tumeanza kuwafuta. Kwa hivyo, naomba nilichukuwe hili ili niweze kuthibitisha ni wangapi sasa hivi ambao wamekuwa *register* tena kwa mara nyengine, ili niweze kumjibu kwa uhakika zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe, Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu ambayo hayaridhishi sana ya Mhe. Waziri. Kwa kuwa katika jibu lake mama alisema kwamba kuna baadhi ya maofisa wamefanya ziara katika baadhi ya nchi za Kiarabu.

Je, ni nchi ngapi ambazo wamefanya mpaka sasa. Pia ni nchi ipi na ipo wamefanya ziara hizo?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, naomba arejee kipengele cha mwisho Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Kauliza kwamba ni nchi ngapi wamefanya ziara na ni nchi zipi, yaani uzitaje hizo nchi. Hebu Mhe. Mjumbe naomba ulirudie hilo swali lako.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe, Spika. Nilimuuliza swali kwamba kwa kuwa katika jibu lake mama alisema kwamba kuna baadhi ya maofisa ambao wamefanya ziara katika baadhi ya nchi za Kiarabu.

Je, ni nchi ngapi ambazo wamefanya hizo ziara. Lakini pia atuambie ni nchi ipi na ipi ambazo wamefanya hizo ziara. Kwa sababu hili tatizo limekuwa kubwa sana.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante Mhe. Spika, kwa heshima nipende kusema tu kwamba katika kufuatilia hizi shughuli, maofisa pamoja na wizara wameweza kufuatilia katika nchi moja ya Qatar, ambayo kwa makusudi kabisa tulikwenda kuangalia hali halisi za wafanyakazi waliokuwepo kule na wanavyofanya.

Pia kwa sababu nchi nyengine zilikuwa hazina Mabalozi, hivi sasa Mhe. Rais wetu ameteuwa mabalozi katika nchi ambazo zilikuwa hazina mabalozi, utaratibu wa mawasiliano ya karibu unaendelea. Tunashukuru sasa hivi ndio maana kumekuwa hata hili wimbi tulokuwa tunalisikia kila baada ya muda mfupi halisikiki tena.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Spika, kutokana na majibu ya Mhe. Waziri, ametuambia kuna taarifa mbali mbali zinazotolewa kutokupitia Ubalozini, na taarifa nyengine zinatoka kwa waajiri wao, nilikuwa nataka kujua.

Je, wizara ina taarifa gani na ina taarifa ya vijana wangapi waliofuata utaratibu huo katika nchi hizo. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nasikitika kwamba hapa kuna Echo kidogo haisikiki. Hilo swali la mwisho ulilotaka kuuliza swali la mwisho, ulitaka kujua nini, hilo la mwisho.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba kurejea. Kutokana na taarifa ya Mhe. Waziri. Je, wizara ina taarifa ya vijana wangapi waliofuata utaratibu kama alioueleza yeye katika jawabu lake mama. Ahsante?

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, mpaka sasa hivi kuna vijana zaidi ya 1,500 ambao wamesajiliwa na wamekwenda na wanafanyakazi huko.

Nam. 57

Utafiti na Uzalishaji wa Zao la Minazi

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:-

Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Lakini kabla ya kuuliza swali, naomba nifanye marekebisho kidogo yaliyojitokeza katika hilo swali langu katika kipengele cha (b) ambapo mwandishi aliandika "dawa yoyote ambayo inazaa".

Mhe. Spika, sikukusudia hivyo, kwa sababu najua dawa haizai. Lakini isomeke, je kuna dawa yoyote ambayo inaweza kutumika. Ahsante sana, baada ya marekebisho hayo naomba swali langu nambari 57 lijibiwe, ahsante sana Mhe. Spika.

Kwa kuwa Wizara ya Kilimo ina wataalamu na wafanyakazi ambao kwa kutumia taaluma yao wanaweza kuongeza uzalishaji mkubwa wa nazi ambazo kutokana na ongezeko la watu, na kwa sababu ya upungufu mkubwa wa zao hilo uliopo na bei ya nazi imepanda hadi kufikia zaidi ya shilingi 1000 kwa nazi moja.

(a) Je, Wizara kwa kutumia wataalamu wake ina mpango gani wa kutafuta au kufanya utafiti wa kupata mbegu za minazi ambazo inaweza kuzaa kwa muda

mfupi na kuwashajihisha wakulima kuipanda kwa wingi ili kupunguza upungufu wa nazi uliopo hivi sasa.

(b) Je, kuna mbolea au dawa yoyote ambayo inaweza kutumika na kuifanya minazi ambayo imeacha kuzaa kwa muda ikarejesha uzazi wake kama mwanzo.

(c) Je, ni aina gani ya miche ya minazi ambayo inaanza kwa muda wa miaka 3 na kama ipo inapatikana wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Ahsate sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe napenda kutoa maelezo mafupi kuhusiana na swali hili.

Mhe. Spika, katika vipindi vya miaka 35 iliyopita utafiti wa minazi ulifanyika kwa kiwango kikubwa kwa kujumuisha zaidi ya aina tano (5) za mbegu za kigeni pamoja na mbili (2) za asili (*East African Tall* na Kitamli). Utafiti huu ulibainisha wazi kuwa mbegu za asili ndizo zenye kustahamili mazingira ya Zanzibar, ambayo pindipo ikishughulikiwa vizuri, yaani (kupaliliwa, kuwekewa mbolea na kukingwa na wadudu waharibifu hasa mdudu bungu wa minazi), zinao uwezo wa kuzalisha nazi zisizipungua 50 kwa mnazi mmoja kwa mwaka na kuishi miaka zaidi ya 75 ikiwa inazalisha. Minazi mifupi ilionekana kuzalisha nazi nyingi (wastani wa zaidi ya nazi 100 kwa mnazi kwa mwaka) lakini baada ya miaka michache (wastani wa miaka 15) huduma hushuka kwa kiwango kikubwa cha uzalishaji wake.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara inaotesha wastani wa miche 20,000 kwa mwaka. Lengo ni kuisambaza kwa wakulima, kwa vile minazi yetu ya asili inao uwezo mkubwa wa kuzalisha nazi kwa muda mrefu na zenye ubora, kwa kulinganisha na minazi mifupi ambayo huzalisha kwa muda mfupi na nazi zisizo na ubora unaofanana na mbegu ya asili.

(b) Mhe. Spika, minazi mingi ambayo inaonekana kuacha kuzaa kwa muda, kutokana na mashambulizi ya wadudu ambao husababisha kudondoka au kukauka kwa vidaka zaidi ya asilimia 50. Minazi inao uwezo wa kurejesha uzalishaji wake pindipo wadudu hawa watadhibitiwa kwa mbinu za asili, ikiwemo kuchanganya miti ya matunda kwenye shamba la minazi.

(c) Mhe. Spika, aina za mbegu fupi za minazi zinao uwezo wa kuanza kuzaa kuanzia miaka mitatu tokea kupandwa, lakini kama nilivyoeleza katika maelezo ya utangulizi, nazi zitokanazo na mbegu hizi hazina ubora kulinganisha na minazi yetu ya asili, hususan katika kiwango cha mafuta. Mbegu fupi ambazo hivi sasa

zinapatikana hapa Zanzibar ni Kitamli, *Malayan Yellow Dwarf (MYD), Malayan Green Dwarf (MGD)* na *Cameroon Red Dwarf (CRD),* na zinapatikana katika mashamba ya wakulima na mbegu ya *MGD* inapatikana katika shamba la Utafiti wa Minazi Kijichi.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya kitaalamu ya Mhe. Naibu Waziri, nafurahi. Lakini naomba niulize tu swali moja dogo, kwa sababu ilionekana kwamba hii ni vipindi vya miaka 35.

(a) Mhe. Spika, kwanza ningetaka nijuwe je, kipindi cha mwisho ambacho mmefanya utafiti na kubaini haya mliyoyaeleza ilikuwa ni mwaka gani.
(b) Kwa kuwa umekiri kwamba miongoni mwa matatizo, kuna matatizo ya wadudu

wanaoababisha kukatika kwa vidaka na kupukutika na mambo mengine na mkatoa maelezo kwamba kutumia kilimo mchanganyiko. Lakini ukiachia hicho kilimo mchanganyiko ambacho wakulima wetu wanakilima kwenye nayo mashamba ya minazi.

(b) Je, dawa gani inayotumika kwa kuwauwa wadudu hawa wanaoshambulia hivyo vidaka ambayo na taaluma yake mmeipeleka kwa wakulima ili wakulima wakaitumia wakapata mazao zaidi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, ulipomalizika utafiti huu ya minazi kama nilivyosema miaka 35 iliyopita mradi huu ulimalizika mwaka 2005.

b) Mhe. Spika, dawa ambayo inatumika kumuuwa mdudu huyu bungu inaitwa andro lakini haishauriwi kutumia kwa sababu hii dawa inapigwa juu kwenye yale matawi na unapopiga inaathiri pamoja na wale viumbe ambao wanaruka. Inashauri zaidi kutumia hii dawa ya asili kuotesha miche ya matunda ndani ya shamba la minazi ili kuweza kuwakimbiza wale sisimizi wanaoharibu, kwani sisimizi na bungu ndio marafiki wanaokaa katika minazi hiyo. Nashukuru.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini ningependa nimuulize suali dogo la nyongeza lenye kitoto (a) na (b).

a) Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametwambia kwamba kuna miche 20,000 ambayo tayari imeshatayarishwa ni wakulima wangapi ambao wamepatiwa miche hiyo ili waweze kuendeleza kilimo hicho cha Minazi.

b) Je, ikiwa kama yale mashamba ya Serikali yana minazi peke yake na wakati hapa umetwambia kwamba yachanganywe pamoja na miche ya matunda ili iweze kusaidia wale wadudu ambao wanaharibu mbigu hizi za minazi. Je, ni utaratibu gani mnaochukua nyinyi kama Wizara kwa haya mashamba yenu ya Wizara ili kuweza kuhifadhi hizi mbegu za minazi yaweze kuzaa na dawa gani mnazotumia kwa minazi ile ambayo imo ndani ya mashamba yale ambayo hamna miche ya matunda. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Wakulima waliofaidika na miche hii zi zaidi ya 500 Unguja na Pemba.
b) Minazi ipo haizai sasa hivi tunaichukua kupandishia ile minazi ili kuweka mengine na ile mikongwe kuifanyia utaratibu mwengine.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipatia fursa hii kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napenda na mimi nimuulize nimuulize suali moja lenye (a) na (b).

Kwa kuwa mnazi ni zao tunalolitegemea sana katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba kwa kupikia vyakula mbali mbali na pia tunapata mafuta yaliyobora katika mnazi.

a) Je, serikali inapotoa hii miche ya minazi kuwapatia wananchi kuna na wataalamu ambao mnawafuatanisha nao ili waweze kupanda minazi hiyo kitaalamu ili yaweze kupatikana mazao yaliyo bora.

b) Ni lini serikali itawafuatilia wakulima pale inapowapa miche wakapande ili kuona ufanisi unapatikana na utunzaji bora wa miche hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Wataalamu tunao wengi na tunapowapa miche hii tunajaribu kuwapa yale maneno ya kitaalamu na ikiwa zaidi basi wanaambatanishwa na wahusika.

b) Serikali ipo tayari muda wowote kuwasaidia wakulima wetu hawa wa minazi ili kuweza kulikuza zao hili tuweze kufaidika zaidi.

Nam. 45

Takwimu za Uzalishaji Mchele Zanzibar

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Takwimu zinaonesha kwamba jumla ya tani 88,903.60 za mchele ziliagizwa na wafanyabiashara wetu kutoka nje kwa kipindi cha mwaka 2016 na kwa sababu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inacho kitengo cha uhakika wa chakula na wataalamu wengi wa kilimo ambao wanaweza kufahamu ni kiasi gani cha mchele unaohitajika kwa mwaka.

(a) Je, ni tani ngapi za mchele zinatosheleza kwa chakula bila ya kuwa na upungufu hapa Zanzibar.

(b) Je, ni tani ngapi za mchele ambazo tunaweza kuzalisha hapa zanzibar na mahitaji yalibaki ndio tukaagiza kutoka Nje.

(c) Je, ni kiasi gani cha Mchele kutoka Tanzania Bara unaoingizwa Zanzibar kwa mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 45 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, tani za mchele zinazotosheleza kwa chakula bila ya kuwa na upungufu hapa Zanzibar ni thamanini na tisa elfu na mia mbili (89,200) ambazo zinatosheleza mahitaji ya nchi kwa mwaka mzima.

(b) Mhe. Spika, hizi sasa Zanzibar inazalisha wastani wa tani ishirini elfu mia tisa na thamanini na tano (20,985) za mchele kwa mwaka. Hata hivyo Zanzibar inaweza kuongeza uzalishaji wa mchele na kufikia tani sitini elfu (60,000) kwa mwaka iwapo tutaendeleza kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji. Serikali kupitia Wizara Kilimo bado inaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji na matarajio yetu kwamba pindipo ujenzi ukikapokamilika, tutaongeza uzalishaji wa mpunga. Hivi sasa kwa sehemu kubwa kinategemea mvua na asilimia 98 ya eneo linalolimwa mpunga linategemea mvua.

(c) Mhe. Spika, kwa wastani Zanzibar inaingiza tani elfu tano mia tano na tisini na sita (5,596) za mchele kwa mwaka kutoka Tanzania Bara na inaingiza tani tisini na saba elfu mia sita kutoka Thailand na Vietnam.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahan kidogo utaniwia radhi samahani. Mhe. Spika, nampongeza sana Waziri wka majibu yake mazuri, sasa anaonekana kidogo mambo yake yameanza kuonyoka yapo vizuri, ahsante.

Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo Waziri umenipatia kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar na Wafanyabiashara kutaka kujua muelekeo wa biashara kwa sababu chakula hichi cha mchele ndiyo chakula chetu kikubwa. Kwa kuwa Waziri umejibu kwamba Zanzibar tunatoa hizo tani ishirini elfu na mia tisa na thamanini na tano na tano elfu tano mia tano na tisini na sita zilizobaki ndizo huingizwa kutoka Tanzania Bara.

a) Mhe. Spika, sisi Zanzibar ni kisiwa na tuna milango mingi ya kuingilia hapa kutoka Bara. Mimi nilitaka kujua je, Wizara imepataje kujua kwa uhalisia kwamba hizi tani elfu tano mia tano na tisini na tisa tu ndizo zinazoingizwa kutoka Tanzania Bara. Kwa sababu ukiachilia mbali muda wa mavuno ukimaliza wananchi wetu ndani ya kipindi cha miezi mitatu wamemaliza chakula chao.

b) Je, nijitihada gani za uhakika kwa Wizara itakazozichukua ili kuhakikisha hizi tani elfu tano, mia tano tisini na sita zilizobakia kama zinazalishwa hapa hapa na tunaachana na kuingiza mchele kutoka Tanzania Bara. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Mhe. Spika, Wizara ina wataalamu wake ambao inatumia kuchukua takwimu hizi, kwa hivyo sisi tunatumia wataalamu hao kupata takwimu mchele unaingizwa tani ngapi ndani ya Zanzibar.

b) Katika swali hili kuna mradi ambao wa ERPP mradi huu unaongeza tani zaidi kwa ajili ya kupata mavuno zaidi, unatumia maji kidogo, mbolea kidogo, eneo dogo lakini mazao yanakuwa ni mengi. Kutokana na mradi huu na miradi mengine na mradi mwengine wa EXIM ambao tukikamilisha basi tunahakikisha kwamba tani hizi zitazidi zaidi ya hizo efu ishirini.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mimi nilikuwa namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba tuna mabonde ya mpunga pale Kibirinzi yaliyofikwa na maji ya bahari na wananchi wale mpaka leo hawapati tena kile kilimo, lakini serikali iliahidi kuwapatia maeneo mengine au kuwafanyia utaratibu mwengine lakini mpaka leo hawajafanyiwa chochote nilikuwa nauliza serikali.

a) Je, ni kauli gani au hatua gani zimeshukuliwa kuhusu wananchi wale.

b) Kwa kuwa wananchi wale hawapati sehemu ya kulima kupatia yale mazao yao. Serikali imewatizamaje katika suala la kuwakimu kichakula katika muda huu ambao hawajapatiwa eneo au ndiyo hawana mpangilio wowote.

Mhe. Spika: Mheshimiwa hilo ni suali jipya naomba ulilete kwa maandishi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipoingia Barazani hapa mwanzo mwanzo alituahidi kipindi cha bajeti akasema hatutomaliza muda hapa mchele hatutoagiza nje. Je, kauli ile anayo mpaka leo au akishindwa atajiuzulu kwa kulidanganya Baraza.

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali hilo nalifuta naliacha, tunaendelea Wizara inayofuata.

Nampongeza Waziri wa Kilimo leo majibu yalikuwa mazuri sana, mafupi yamekaa vizuri sana. Ahsante sana hongera sana.

Nam. 77

Uingizwaji wa Dawa za Kupuliza Mbu Ambazo Hazina Kiwango

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Kumekuwa na kasi ya uingizwaji wa dawa za mbu za kupuliza ambazo zinaonekana zipo chini ya kiwango ambapo dawa hizo zinapopulizwa zinaingia mikononi mwa mpulizaji badala ya kusambaa kwa njia ya hewa.

(a) Je, Wizara imegundua tatizo la dawa hizo.

(b) Je, ukaguzi unafanywa kwa namna gani mpaka dawa hizo zinaingizwa katika matumizi ya watu nchini kwetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 77 kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kawaida kupitia Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi, ukaguzi huwa unafanywa kwa njia ya kuangalia dawa hizo pale zinapoingia nchini (Bandarini). Vipimo mbali mbali huangaliwa ikiwemo tarehe ya kutengenezwa na kumaliza muda wa matumizi ili kuhakikisha dawa hizo ni salama na zina viwango vinavyohitajika.

Mhe. Spika, kazi hii hufanywa kwa mashirikiano makubwa baina ya Wizara ya Afya na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kupitia taasisi husika ambazo zinahusika na kulinda viwango na usalama wa dawa kwa matumizi nchini.

Mhe. Spika, inatokezea kidogo, wakati wakala inapofanya ukaguzi kwa kubaini bidhaa zilizopitwa na wakati *(Expired)* katika maghala, kwa baadhi ya wakati hukuta pia bidhaa ambazo ni nzima lakini hazikuhifadhiwa ipasavyo na kiuhalisia kutohifadhiwa ipasavyo, hupelekea bidhaa hiyo kupotea ubora wake. Wakala anapokutana na hali hiyo hutoa maelekezo kwa wahusika ili kunusuru ubora wa bidhaa hiyo kwa manufaa ya watumiaji.

Mhe. Spika, Wizara yangu inafatilia kwa kina taarifa juu ya kuwepo kwa dawa hizi, pindi zikibainika na uwezekano wa kuleta madhara kwa binadamu, hatua za kudhibiti zitachukuliwa mara moja. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, nilitegemea suala hili hasa litajibiwa na Wizara ya Biashara. Sasa Mhe. Naibu Waziri utaangalia au kama Waziri yeyote atasaidia si vibaya kwa mujibu wa Kanuni zetu za Baraza.

Mhe. Naibu Waziri mmepitisha Sheria ndani ya Baraza hili kuna Kampuni inaitwa Kilimanjaro Dubai na Kampuni nyengine kukagua zile dawa, vyakula kutokana na kiwango cha chake, lakini inatokana hizo Kampuni zilizokuwepo ni mzigo zinashindwa kusimamia majukumu yake na wafanyabiashara kule hutozwa ada.

a) Je, serikali ina kauli gani kuhusu tukio hilo, tunaletewa dawa na nyengine zinabadilishwa baada ya *heat* inaitwa *hot* baada ya *hot* inaitwa *heat* zinabadilishwa majina tu, lakini kile kile chakula chenyewe ni mchele unabadilishwa mapishi tu, unaweza kupika biriani, pilau, mseto.

b) Je, serikali haioni haja sasa baada ya kuumiza wafanyabiashara kutozwa ada vitu hivyo huko nje ya kampuni ya viwango ambapo imeshindwa majukumu yake. Lini serikali itatoa kauli kutafuta wakala wengine waweze kushindwa majukumu haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli kwamba serikali inayo wakala nje ya nchi ambayo ni *ZBF, Zanzibar Bureau Standard* Wakala hii inafanya kazi katika nchi tofauti ikiwemo Dubai, China na kadhalika. Wakala huyo wa viwango ana kazi ya ukaguzi wa bidhaa mbali mbali za vyakula na vyombo vya moto na kadhalika. Lakini bado naomba nirudi kwenye jibu langu la msingi kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Spika, inawezekana kwamba dawa hizi kule zilikaguliwa na ziliingia katika nchi zikakaguliwa na zikawa zipo salama lakini zikaharibika au zikapoteza ubora kidogo katika mazingira ya kuzihifadhi. Nilikuwa namuomba atupe muda ili wakala wa bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi hapa Zanzibar ifanye utafiti wake baadae itatoa taarifa kuhusu dawa hizo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, ahsante kwa kuniona pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri ningeomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa muuliza swali ameongeza juu ya kiwango cha dawa tofauti na alivyojibu Mhe. Waziri cha ku-*expire* au laa, nataka kujua tu serikali ina mkakati gani wa kuunda maabara ya kuona sasa tunapima vitu hivi hapa nchini vya viwango.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mheshimiwa suala hilo tunalichukua kama ni ushauri uliotupa Wizara tutalifanyia kazi na naamini kwamba tutapata jawabu zuri la utekelezaji katika suala hilo.

Nam. 20

Kuondolewa Gari za Abiria Zenye Tairi Moja

Mhe. Suleiman Sarahan Said – Aliuliza:

Katika kulinda maisha ya wananchi wake, Serikali ilitoa agizo la gari za abiria zenye tairi moja moja nyuma kama gari za HIACE kuondoka katika soko la usafirishaji abiria. Lakini gari hizo bado zinashamiri kuletwa na kuendelea na biashara hiyo.

(a) Je, daladala za tairi moja moja nyuma hazina umuhimu tena wa kuziondoa katika sekta ya usafirishaji abiria.

(b) Nini lengo la serikali kuhusu kuziondoa daladala hizo kwenye biashara hiyo. Na kama bado lengo hilo lipo ni lini Serikali imeweka mwisho wa matumizi ya gari hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Umuhimu wa kuziondoa daladala zote zenye tairi mbili katika biashara ya daladala upo palepale kama inavyoeleza kanuni ya 52 ya gari za biashara.

(b) Lengo kuu la serikali kuziondoa gari hizo ni kulinda maisha ya raia wake na kuweka usalama wa abiria na mali zao na serikali tayari imesimamisha usajili wa gari mpya za aina hii ila zile zilizokuwepo zimalizike wenyewe lakini kutokana na ujanja unaotumiwa na wenye magari wa kubadilisha kila kitu katika "*chasis*" za gari zilizokuwepo serikali inaandaa utaratibu mpya na utakapokamilika itatangazwa rasmi siku ya mwisho ya matumizi ya gari za aina hiyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Spika, na mimi nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina swali la (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwa kuwa serikali inajua kuwa kuna udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wamiliki wa gari hizo. Je, serikali imetoa elimu gani kwa wamiliki hao na itawasaidiaje katika kuwasaidia kibiashara na kutokupata hasara.

b) Kwa kuwa serikali imeona gari za aina hiyo hazifai au pengine zina kasoro katika suala la biashara hiyo. Je, serikali kwa gari hizo zitawabadilishia njia kuwatoa mjini kuwapeleka mashamba au zitafuta leseni kabisa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

a) Kwanza napenda kumuarifu kuwa kwa mujibu wa sheria yetu ya Nam. 7 ya 2003 ya usafiri barabarani kifungu Nam. 14(2) (c) kinaelezea Wajumbe wa Bodi, katika wajumbe wale wamo wajumbe kutoka watu wanaohusika na mambo ya usafiri

yaani daladala. Kupitia wale tunakuwa tunaelewesha namna gani ambapo utaratibu watumie katika kuwaelimisha watu.

Kwanza si cheat, pili kwamba hizi gari tumeziondosha kwa sababu ya usalama wao na abiria wetu, kwa sababu zile gari zinakuwa haziwezi kuhimili katika mwendo mkubwa. Kama nilivyosema gari hizi nyingi asilimia zaidi ya 50 zipo mjini zaidi. Sisi tunahakika kwamba hizi gari tutakapoziondoa moja kwa moja na ndio lengo letu kuziondoa moja kwa moja basi wanaweza kuzitumia kwa matumizi mengine, lakini kwa vile ajali ni nyingi tunaomba sana tuendelee kukubali kwamba zile gari zisiendelee kufanya kazi tena. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Spika, mimi naipongeza serikali kwa kuwaza wazo hilo muhimu, juu ya kusema kwamba gari zenye tairi moja ziondoke lakini swali langu liko hapa tunapotembea pengine na Mhe. Waziri kapata nafasi hizo tumetembea katika sehemu mbali mbali mfano Ethiopia, Zambia, Rwanda, Tanzania Bara pia ndani ndani zipo gari hizi bado zinatumika na kwa hapa Zanzibar tunamini usalama wa maeneo yetu yapo karibu na hali hiyo Mwenyezi Mungu anatuondoshea ajali hazitokei.

Je, hivyo Mhe. Waziri kwa kuzingatia ajira za watu wetu na huduma mbali mbali kwa wanyonge gari hizi ziondoshwe wataofaidika si matajiri wenye uwezo wa kununua magari makubwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kujuchukua nafasi hii Mhe. Ali Suleiman Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Kijito Upele swali lake kama ifutavyo:

Tunajua ni kweli lakini hata hivyo maisha ya binadamu nayo ni muhimu katika kipindi cha Januari mpaka Agosti zimetokea zaidi ya ajali 387 za gari pamoja na pikipiki na vifo zaidi ya 110. Kwa hivyo tunajua daladala hizi namna gani zinavyohatarisha usalama wa watu wetu na vile vile mimi nina imani kubwa sana hawa watu ambao nitawaondoa kwa utaratibu maalum wanalielewa hilo kwa sababu tayari tushatoa elimu kwa hivyo watustahamilie lakini usalama wa watu wetu ni muhimu zaidi kuliko mali zetu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante swali la mwisho linaulizwa na Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Konde.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nijibiwe swali langu nambari 46 lakini kabla ya kunijibu niliomba Mhe. Waziri afanye marekebisho kwa sababu swali langu mimi lilikuwa linahusiana na barabara ya Mtambwe sio Mtambile ilikuwa ni Mtambwe Daya sio Mtambili Daya kwa hivyo baada ya hapo naomba swali hili lijibiwe ahsante.

Nam. 46

Kumong'onyoka kwa Barabara ya Mtambwe – Daya, Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa Barabara ya Mtambwe-Daya katika eneo la Kinyasini kwa Yakob eneo hilo lilimong'onyoka na kuanza kuonesha athari kubwa jambo ambalo lilipelekea kurejewa matengenezo ya ujenzi kwa eneo hilo lakini hata hivyo muda mfupi tu baadae kutokana na mvua kubwa zilionyesha za masika, eneo hilo limeshaanza kukatika tena licha ya kujengwa kwa mawe na kutumia waya Maalum.

(a) Je, Wizara inafahamu kwamba eneo la barabara limeshaanza kukatika tena.

(b) Je, wataalamu watachukuwa hatua gani za dharura kulihami kabla athari kubwa zaidi haijatokea.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:

Ahsante sana Mhe Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji napenda kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid suala lake Nam. 46 lenye vipengele (a) na (b) baada ya kufanya marekebishi ni kweli aliyosasema ni kwamba.

Barabara ya Mtambwe-Daya ni miongoni wa barabara zenye jumla ya urefu wa kilomita 32 zilizojengwa kupitia ufadhili wa MCC na kukamilika miaka minne iliyopita. Kutokana na maumbile ya ardhi ya barabara ya Mtambwe-Daya, maeneo mengi yalijazwa udongo na kifusi kwa kiwango kikubwa na baada ya mvua kunyesha baadhi ya maeneo hayo likiwemo la Kinyasini kwa Yakob yaliaanza kukatika na hivyo kulazimika kumtafuta Mkandarasi mwingine wa kuzifanyia matengenezo maalumu sehemu hizo kwa kujengwa mawe yaliyopangwa kwenye nyavu maalum wenyewe wanaita *(gabion)* ili kuzuia kukatika kwa barabara hiyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu kama ifuatavyo;-

a) Ndio Wizara yangu inafahamu kuwa eneo hilo limeanza tena kukatika baada ya mvua kubwa za masika zilizonyesha mfululizo mwezi April na Mei 2017, na juzi tarehe 22 mimi nilikwenda kuangalia athari hiyo.

b) Watalaam wa Wizara wanalifanyia kazi eneo hilo na mengineyo yaliyoathirika kutokana na mvua zilizonyesha mfululizo mwezi Aprili na Mei 2017 ili kubaini chanzo cha kukatika kwa maeneo hayo na kuyafanyia tathimini ambapo baadhi ya maeneo ya barabara za Pemba yaliyoathirika tayari yameshafanyiwa tathmini ya gharama kwa ajili ya matengenezo ambayo yatafanywa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza swali dogo la nyongeza Mhe. Waziri pamoja na majibu mazuri sana yenye kutia moyo kwa ajili ya watumiaji wa barabara hiyo Watu wa Mtambwe na Wazanzibari wote kwa jumla ambao wanatusikiliza.

a) Kwa kuwa wataalamu wameshakwenda na kuona hiyo athari iliyojitokeza na kwamba hatua za dharura sasa zinahitajika kutokana na eneo lile kwamba tutakapoliwachia linaweza likaendelea na kuingiza hasara zaidi mimi ningependa kujua ni kipindi gani kinatarajiwa kulifanyia marekebisho ya kudumu tukapata ufumbuzi wa kudumu wa eneo lile ambapo mara ya kwanza lishafanyiwa na mara ya pili lishafanyiwa na mara ya pili lishajitokeza tena.

b) Ni kiasi gani cha fedha ambacho baada ya wataalamu kukagua kitahitajika kwa kufanya haya marekebisho ambayo yatakuwa ya muda mefu ili kuhakikisha halitaendelea tena kukatika eneo lile lilokuwa linakatika mara kwa mara. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a), (b) kama ifuatavyo.

Kama ulivyosema yako maeneo mengi ambayo baada ya mvua kubwa hivi yameathirika watalamu wetu wameenda kuchukuwa udongo ili kuchukuwa ufanywe *test* baada ya kufanya udongo ule *test* basi tutajua ni kiasi gani tutataka kutumia katika kufanyia marekebisho sehemu zile.

Kama ulivyosema kwamba kiasi cha fedha kitajulikana baada ya kufanya tathmini na pale ambapo tutapata fedha basi haraka tutandelea kufanya marekebisho sehemu zile, kwani kuna sehemu zilitokea athari hizo wakati wa mvua na takribani anazijua zikiwemo Chamangwana na sehemu nyengine tofauti na kishatumia takribani milion 200,000,000. kwa hili namuhakikishia kwamba baada ya kufanya tathmini tunaendelea kuhakikisha kwamba tunazirekebisha zile sehemu ili barabara zile ziendelee kutumika kwa muda mrefu zaidi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye kitoto (a) na (b) kama ifuatavyo:

Pamoja na majibu mazuri Mhe. Waziri uliyotupa lakini nataka kuuliza swali hilo kuhusiana na barabara ya Wete - Gando ambayo nayo imekatika. Jee Mhe. Waziri nataka nijue kwamba Mhusika wa kuitengeneza barabara ile au eneo lile lilokatika ni Wizara ama ni nani na kama ni Wizara ni sababu iliyofanya hadi leo eneo lile halijetengenezwa hadi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Spika kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Maryam Thani Juma

Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Gando swali lake lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Ile barabara baada ya kujengwa na Mkandarasi wa MECO muda wake ambao unakuwa mwaka mmoja ulipita hivi sasa dhamana wa kutengeneza barabara ile ni chini ya Wizara yetu kupitia Idara ya UUB.

Kama nilivyosema kwamba tayari tumeshaanza kufanya marekebisho lakini tunataka baadaye tuweke na lami kabisa, lakini kama nilivyosema mwanzo barabara ile kama ilivyokuwa barabara ya Mtambwe Daya tunachukuwa udongo wake wa kufanyia *test* kwa sababu kama ulivyosema baada ya kuathirika na mvua imeonekana kwamba ule udongo unajivuta kwa hiyo kuifanya ile barabara isidumu. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe Spika: Ahsante wakati wa maswali umekwisha Waheshimiwa Wajumbe kama mtakumbuka kwamba inabidi sasa hivi tuahirishe shughuli zetu mpaka saa 11:00 kwa hiyo hoja inayofuata itakuja kuingia kuanza kujadiliwa kuanzia saa 11:00 kwa maana hiyo nachukua nafasi hii sasa kusitisha shughuli za Baraza mpaka saa 11:00 kamili jioni ya leo.

(Saa 4:15 asubuhi Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti, (Mwanaasha Khamis Juma) alikalia kiti

HOJA ZA SERIKALI

Ripoti ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na utukufu kwa kutukutanisha hapa tukiwa wazima na afya njema na zaidi tukiendelea kuongozwa na Mhe. Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohammed Shein pamoja na wasaidizi wake wote. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azidi kutupa amani na utulivu, ili hatimaye atukabidhi kijiti 2020 Mwenyezi Mungu akitujaalia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuwasilisha Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza lako tukufu, kama ambavyo walitupatia wakati walipokuwa wakifanya kazi za kamati katika wizara yangu kwa lengo la kuimarisha utendaji na kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya wizara.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni, Yussuf Hassan Idd, Makamo

Mwenyekiti ambaye ni wewe mwenywe Mhe. Mwenyekiti, nafasi ya wanawake Mhe. Hamida Abdalla Issa pamoja na wajumbe wote wa kamati hiyo kwa ushauri, maelekezo na mashirikiano waliyotupatia muda wote wakati wakitekeleza majukumu yao kwa lengo la kuimarisha kazi zetu za kila siku. Ni imani yangu kuwa ushauri na maelekezo waliyotupatia yamesaidia sana katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya wizara yangu kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inaendela kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira 2020 ya Zanzibar, Ilani ya Uchaguzi wa CCM 2015 - 2020, Mkakati wa Kukusa Uchumi na Kupunguza Umasikini (MKUZA), Malengo ya Maendeleo Endelevu (*SDGs* 2015 - 2025), Mpango wa Mageuzi ya Kilimo (*ATI*), Mpango wa Muda Mrefu wa Usimamizi wa Rasilimali za Misitu, Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji na Mpango Mkakati wa Kuimarisha Usimamizi wa Uvuvi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Yussuf Hassan Iddi ilipata fursa ya kupitia sekra zote za wilaya za wizara hii Unguja na Pemba kwa lengo la kukagua na kupokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti kutoka taasisi na idara tofauti za wizara, pamoja na kupokea taarifa za utekelezaji wa bajeti na majukumu ya wizara.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba niende moja kwa moja kwenye maagizo ya kamati na utekelezaji wake uliofanyika.

Kwanza ni Idara ya Kilimo ambayo ilikuwa na mambo saba.
Agizo nam. 1. Kamati ilisema wizara iwasiliane na wazabuni wanaoleta pembejeo za kilimo ili pembejeo hizo ziwafikie wakulima kwa wakati.

Utekelezaji. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango tayari imepata mzabuni *Bajuta International (T) Ltd* ya Arusha kwa ajili ya kuleta tani 700 za mbolea (*TSP*). Tani 900 za *Urea*, mbegu tani 350, pamoja na dawa za kuulia magugu lita 15,000. Serikali tayari imelipa mzabuni deni la nyuma la pembejeo la shilingi 600/= milioni. Kupitia programu ya *ERPP* tani 306 za *Urea* na tani 152 za *DAP* mbolea zimenunuliwa kwa ajili ya kuendeleza wakulima wa mpunga wa umwagiliaji maji.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya ziada Kampuni ya Bajuta tayari imewasilisha tani 100 za mbolea (Tani 65 Urea na tani 35 *DAP*), kwa ajili ya kilimo cha mpunga wa umwagiliaji maji. Hivyo, wakulima kuanzia sasa wanapata mbolea bila ya matatizo yoyote. *(Makofi)*

Agizo nam. 2. Wizara kwa kushirikiana na Masheha na Serikali za Wilaya ihakikishe mabonde yanayotumika kwa shughuli za kilimo na maeneo ya vianzio vya maji hayavamiwi.

Utekelezaji. Wizara inashirikiana na masheha, Kamati za Kilimo za maeneo ya Serikali za Wilaya katika kuhamasisha wananchi juu ya matumizi bora ya maeneo ya kilimo, kutunza vyanzo vya maji na utunzaji wa mazingira, ili kuhakikisha mabonde yaliyo chini

ya usimamizi wa wizara yanatumika kwa kazi za kilimo. Aidha, wizara kwa kushirikiana na *FAO* inatekeleza mradi wa kuhifadhi mito kama vile Mwanakombo, Chaani na Kianga. Mpango huu pia unawafundisha wakulima na wana jamii juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya ziada serikali imetuagiza tuanze kazi ya kuyapima maeneo yote ya kilimo, ambapo kazi hii inatarajiwa kuanza robo ya pili ya mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, jumla ya shilingi 12, 377,200 zimetengwa kwa ajili ya upimaji wa maeneo ya kilimo.

Agizo nam. 3. Wizara itoe elimu kwa wakulima juu ya mpango wa wizara kwa kununua pembejeo za kilimo kutoka kwa wakulima, ili kuondoa malalamiko yasio ya lazima.

Utekelezaji. Wizara kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wakulima imeshatoa elimu katika mabonde ya Tibirinzi, Weni, Mangwena na Dobi kwa mabonde ya umwagiliaji maji na Kohowe, Msaani, Chanjaani kwa mpunga wa kutegemea mvua juu ya mpango wa kununua mbegu kutoka kwa wakulima kwa ajili ya msimu wa mwaka 2017/2018. Aidha, jumla ya tani 15.5 za mbegu ya mpunga tayari zimenunuliwa. Kazi hii imeanza vizuri na wakulima wamelipwa kwa mujibu wa taratibu na hakuna mkulima yeyote aliyekopwa mwaka huu.

Agizo nam. 4. Wizara itoe ushirikiano wa dhati kwa wawekezaji wote wanaowekeza au wanaokusudia kuwekeza kwenye sekta zinazosimamiwa na Wizara ya Kilimo.

Utekelezaji. Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Mpango na Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar, inaendelea kutoa ushirikiano wa dhati kwa wawekezaji. Aidha, wizara kwa kushirikiana na *ZIPA* imesajili miradi ya umwagiliaji maji kwa kampuni ya *NETAFIM* ya India na Kampuni ya *ENCHELON* kwa ajili ya uzalishaji wa sukari ya Stevia huko Bambi.

Agizo Nam. 5. Wizara ishajihishe wananchi kulima kilimo cha *spices*, kwani kilimo hiki kimekuwa na soko kubwa ulimwenguni.

Utekelezaji. Wizara kwa kushirikiana na Asasi Zisizo za Serikali, ikiwemo *Zenj Spices* ya Zanzibar (*Zanzibar Organic Spices Growers)* na Kamapuni ya Lecon ya Ujerumani, imewashijihisha vikundi vya wakulima, uzalishaji wa mazao ya viungo na kuwaunganisha na masoko ya bidhaa huko Ujerumani. Aidha, wizara inaendelea kutoa elimu pamoja na upatikanaji wa miche bora, wiara pia imekamilisha ujenzi wa jengo la usarifu la Kizimbani na inaendelea kukamilisha ujenzi wa kituo cha usarifu wa mazao Pujini, Pemba. Mpango wa Mkakati wa Mazao ya Viungo na Minazi umetayarishwa kupitia Idara ya Misitu na Kilimo.

Agizo nam. 6. Wizara indelee na jitihada zake kwa kutumia fedha za *OC* kwa kufanya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji maji pale hali inaporuhusu, ili huduma hii iwafikie wakulima wote kwa maeneo yao.

Utekelezaji. Kwa kutumia fedha za *OC* wizara imekarabati misingi ya umwagiliaji maji katika mabonde ya Cheju mita 200, Kibokwa mita 300, Mwera 50, Bumbwi Sudi 180 na Uzini mita 100 kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba wamekarabati umefanyika katika bonde la Mangwena mita 100 pamoja na bwawa la Kangagani kwa kushirikiana na *Costech*. Kazi hii Mheshimiwa inaendelea. *(Makofi)*

Agizo nam. 7. Wizara indelee kufuatilia ili kuhakikisha Shirika la Umeme (*ZECO*) linafanya matengenezo ya nguzo zilizoinama katika bonde la Cheju.

Utekelezaji. Wizara imewasiliana na Shirika la Umeme na tayari shirika limeshabadilisha nguzo sita za umeme zilizokuwa zinahofiwa kuleta madhara. Aidha, wizara inaendela kushirikiana na Shirika la la *ZECO* kwa kubadilisha nguzo nyengie saba zilizoanguka hivi karibuni kufuatia mvua kubwa za masika.

Idara ya Maendele ya Mifugo ina hoja 12.

Agizo nam. 1. Serikali kupitia wizara iandae utaratibu maalum wa kudhibiti uingizaji wa bidhaa za mifugo kutoka nje ya nchi hasa zile ambazo zinazalishwa kwa wingi hapa ndani.

Utekelezaji. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi itashirikiana na Bodi ya Chakula na Vipodozi, Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha kuandaa kanuni ya udhibiti wa uingiaji *(Export/Import Regulation)* za bidhaa za mifugo.

Agizo nam. 2. Kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa wafugaji.

Utekelezaji. Wizara imetoa elimu ya ufugaji bora wafugaji kuku, mbuzi, ng'ombe wa maziwa kwa vikundi 131, Unguja 351 na Pmba 80. Vile vile kupitia Madaraka Mikoani ugatuzi baadhi ya maofisa wa mifugo wa uzalishaji wamehamishiwa katika Halmashauri za Wilaya ili kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa wafugaji. *(Makofi)*

Agizo nam. 3. Wizara iongeze ajira kwa wataalamu wa mifugo ili tuwe na wataalamu wa kutosha.

Utekelezaji. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kupitia Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeomba nafasi za ajira 68 kwa maafisa wa mifugo. Vile vile kupitia programu ya *ASSP/ASPD-L*, wizara imeteuwa na kuwajengea uwezo wa kitaaluma na kuwapatia vifaa vya huduma binafsi na tiba kwa jamii 204, Unguja 108 na Pemba 96 kwa ajili ya kutoa huduma za matibabu ya mifugo katika ngazi ya shehia. Wizara katika kipindi cha miaka mitatu imepeleka nchini China jumla ya vijana 15 kwa ajili ya mafunzo ya udaktari wa mifugo. Vile vile kwa mwaka fedha 2017/2018 wizara imesajili vijana 16 ambao watakwenda China kwa ajili ya mafunzo ya udaktari wa mifugo.

Agizo nam. 4. Wizara iendelee kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kuzalisha pembejeo za mifugo na kilimo.

Utekelezaji. Wizara kwa kushirikiana na *ZIPA* inaendelea na jitihada za kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya kuzalisha pembejeo za mifugo na kilimo.

Agizo nam. 5. Serikali ianzishe mpango maalum wa kuhamasisha wananchi kula bidhaa za mifugo kama vile mayai na maziwa ikiwemo na siku maalum ya kunywa maziwa.

Utekelezaji. Wizara itarejesha tena Siku Maalum ya Kunywa Maziwa Zanzibar kila mwezi wa Juni. Vile vile kupitia Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe programu maalum ya lishe maskulini inaendelea kutoa taaluma na uhamasishaji wa utumiaji wa maziwa skuli.

Agizo nam 6. Wizara iandae mpango wa kuanzisha kituo cha utafiti wa mifugo ili kufanya tafiti za aina mbali mbali.

Utekelezaji. Serikali tayari imeshaanzisha taasisi ya utafiti wa mifugo kwa lengo la kuendeleza utafiti wa mifugo hapa nchini. Katika mpango kazi wa taasisi hiyo, mpango wa utekelezaji wa utafiti unaandaliwa katika robo ya pili ya mwaka huu.

Agizo nam. 7. Kutokana na ongezeko kubwa la ukuaji wa Sekta ya Kilimo, sambamba na ukuaji wa Sekta ya Mifugo, tayari yameanza malalamiko ya maeneo ya wazi kwa wakulima na wafugaji, ili kunusuru migogoro ambayo inaweza kujitokeza hapo baadae. Serikali ianzishe mpango maalum kwa kutengeneza maeneo ya mifugo.

Utekelezaji. Wizara inaendelea kuwashajihisha wafugaji kufuga ufugaji wa kisasa *zero grazing*, ili waweze kutumia eneo dogo la ardhi kwa kufuga ng'ombe wachache wa kisasa na wenye tija na kuacha kufuga ufugaji wa kizamani wa kutumia kamba. Jitihada zaidi zinafanyika kwa wafugaji kupanda majani na kulisha masalia ya mazao.

Agizo nam. 8. Wizara itafute namna bora zaidi ya kuliimarisha na kuliendeleza Shamba la Mifugo Pangeni kwa lengo la kuimarisha Sekta ya Mifugo.

Utekelezaji. Wizara inaendelea na jitihada ya kuliimarisha na kuliendeleza Shamba la Mifugo Pangeni kwa kutumia kwa kazi za mifugo na kualisha mitamba ya ng'ombe wa kisasa wa maziwa kwa ajili ya kuuziwa mifugo wafugaji wadogo wadogo. Kwa mwaka 2017/2018, wizara imejiandaa kuweka mbinu ya maji na kutekeleza njia ya kuelekea Shamba la Mifugo Pangeni.

Agizo nam. 9. Wizara iandae mpango maalum kwa kuongeza idadi ya mifugo katika shamba la mifugo Pangeni pamoja na kuzuwia kuuza mifugo inayozaliwa katika shamba hilo kwa muda.

Utekelezaji. Wizara imechukua ushauri na mapendekezo yaliyotolewa kwa muda huu ng'ombe 32 waliobaki wataendelezwa na kuimarishwa hapo shambani.

Agizo nam. 10. Wiara itafute suluhisho la maji katika Shamba la Mifugo Pangeni. Kupitia Mradi wa Miundombinu na Kuendeleza Wafugaji Wadogo Wadogo.

Utekelezaji. Wizara imetenga fedha kutoka serikali, ambapo pamoja na kazi nyengne pia kazi ya kuchimba kisima itafanyika ili kumaliza tatizo la upatikanaji wa maji katika Shamba hilo la Mifugo Pangeni.

Agizo nam. 11. Wizara ihakikishe upatikanaji hatimiliki wa shamba hilo.

Utekelezaji. Tangu miaka 60 eneo la Shamba la Pangeni limepimwa, limechorwa ramani na limetengwa maalum kwa kazi ya mifugo. Aidha, suala la upatikanaji wa hatimiliki linaendelea.

Agizo nam. 12. Wizara ianzishe mpango maalum wa kuifanyia matengenezo njia ya kuelekea Shamba la Pangeni.

Utekelezaji. Wizara inaendelea na jitihada ya kuifanyia matengenezo njia ya kuelekea Shamba la Mifugo Pangeni kupitia mradi wa miundombinu ya mifugo.

Idara ya Misitu na Mali Zisizorejesheka ina hoja 16

Agizo nam. 1. Wizara kwa kushirikiana na taasisi husika iendelee kukomesha matumizi ya msumeno wa moto.

Utekelezaji. Wizara kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama inaendelea na kampeni ya kuzuwia matumizi ya msumeno wa moto hapa nchini. Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na kufanya doria ya kuikamata na kuichoma moto misumeno hiyo. Jumla ya misumeno 55 Unguja 31 na Pemba 24 imekamatwa na kuhifadhiwa na Idara ya Misitu, kazi ya msako inaendelea kupitia masheha na vyombo vya ulinzi.

Mhe. Mwenyekiti, juhudi za kuelimisha wananchi juu ya umarufuku wa matumizi ya msumeno ya moto zinaendelea, lakini bado hatujapata mashirikiano ya kutosha na masheha ambao ndio walio karibu sana na wananchi.

Agizo nam. 2. Kuwe na usimamizi na utaratibu wa uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka.

Utekelezaji. Wizara inaendelea kukusanya taarifa kuhusu mahitaji na matumizi ya maliasili zisizorejesheka (*resource survey and/or assessment*) kwa ajili ya kutayarisha mpango mkakati wa matumizi endelevu ya maliasili hizo hapa nchini. Aidha, wizara imetayarisha mpango kazi wa mwaka 2017/2018 kwa usimamizi wa matumizi ya mali zisizorejesheka.

Agizo nam. 3. Serikali ianzishe sera maalum ya '*Green Policy'* ili tuweze kupanda miti kwa wingi katika nchi yetu.

Utekelezaji. Wizara tayari imeandaa mpango mkakati kwa ajili ya kutekeleza upandaji miti mijini na vijijini kama ilivyoelekezwa katika sera na sheria za misitu Zanzibar. Aidha, mpango huo unatekelezwa katika siku maalum ya upandaji miti kitaifa unaofanyika katika mwezi wa Machi kila mwaka. Mkakati huu unahusu upandaji wa miti ya minazi, mikarafuu, miti ya matunda na kivuli katika maeneo ya barabara na maeneo yaliyopo matupu. Pia wananchi hupatiwa miti hiyo bure kupitia masheha.

Agizo nam. 4. Wizara itoe taarifa maalum mbele ya Baraza hili tukufu hali halisi ya uchimbaji mchanga ili Wajumbe wa Baraza hili pamoja na wananchi waelewe dhamira ya serikali juu ya matumizi ya rasilimali ya mchanga.

Utekelezaji. Wizara tayari imeshatoa taarifa serikalini na kwa wananchi kuhusu hali ya upatikanaji wa mchanga hapa nchini. Wizara iko tayari kuwasilisha taarifa maalum kuhusu hali halisi ya uchimbaji mchanga hapa Zanzibar mara baada ya kupata ridhaa ya Baraza la Mapinduzi na hatimaye kuwasilisha hapa Baraza la Wawakilishi.

Agizo nam. 5. Wizara iangalie upya mgao wa mapato unaoingia katika Idara ya Misitu kwa kupitia misitu ya Jozani. Je, idara inastahiki kupata mgao huo?

Utekelezaji. Wizara itafanya mapitio kuhusu mgao wa mapato yanayotokana na makusanyo ya Jozani. Idara inastahiki kupata mgao huo kwa mujibu wa kanuni iliyopo. Hata hivyo, mgao wa mapato ya Jozani upo kwa mujibu wa sheria Nam. 10 ya Usimamizi wa Misitu ya mwaka 1996 kupitia Kanuni Nam. LN 26 ya mwaka 2009, ambayo imeweka utaratibu wa mgawanyo wa mapato yanayopatikana katika hifadhi hiyo. Utaratibu huo ni kama ifuatavyo:

- Asilimia 40 ya mapato yote yanatumika kwa uendelezaji wa hifadhi yenyewe,
- Asilimia 30 ni kwa ajili ya kulipa fidia kwa wenye mashamba eneo la Jozani, ambao mazao yao yanaharibiwa na kimapunju.
- Asilimia 20 ni kwa ajili ya Idara ya Misitu na
- Asilimia 10 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya jamii katika vijiji tisa vinavyozunguka hifadhi ya Jozani.

Agizo nam. 6. Msitu wa Jozani unao mgao wake kwa ajili ya kuendesha shughuli za misitu. Hivyo itumie fedha hizo kutatua changamoto zake zikiwemo kuunganisha *internet* katika eneo hilo.

Utekelezaji. Fedha zinazopatikana katika mgao wa Jozani zimetumika kwa ajili ya usimamizi wa maendeleo ya hifadhi ya Jozani. Wastani wa shilingi 15 milioni zimetengwa kwa kazi ya ufungaji wa *internet* kupitia Kampuni ya Simu ya *Halotel*. Jamii zinazozunguka hifadhi ya Jozani zinanufaika na mapato ya msitu huo, jumla ya shilingi 155 milioni zimegawiwa kwa wanajamii kwa kipindi cha miezi sita tu, Januari mpaka Juni 2017.

Agizo nam. 7. Wizara iandae mpango wa kuongeza nafasi za ajira za misitu.

Utekelezaji. Wizara imetayarisha mpango wa rasilimali watu na kuwasilisha serikalini ambapo unaonesha mahitaji ya wafanyakazi kwa kila sekta. Aidha, vijana watano, wanne wa misitu na mmoja wa nyuki ambao wamesomesha na Mradi wa Hima waliomaliza masomo ya *Diploma* wameajiriwa mwezi wa Septemba, 2017 na vijana saba waliomaliza masomo ya *Diploma* mwezi waa Juni, 2017 kati ya fani ya misitu wanatarajiwa kuombewa ajira hivi karibuni.

Agizo nam. 8. Wizara iendelee kutoa elimu ya kutosha katika maeneo mbali mbali, ili kuhamasisha wananchi kutembelea katika misitu sambamba na kutangaza misitu hiyo ndani na nje ya nchi. Hili agizoa la 8 na 9 yanakwenda pamoja Mhe. Mwenyekiti, yaani wizara iongeze jitihada za kutangaza misitu ndani na nje ya nchi.

Utekelezaji. Wizara imeandaa mpango mkakati kwa Kitengo cha Uhamasishaji wa Misitu ya Jamii na pia kupitia katika tovuti ya wizara. Idara inaendelea kutangaza misitu ya Zanzibar ndani na nje ya nchi. Aidha, kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii na Kampuni ya watembezaji watalii katika kuitangaza misitu hiyo ndani na nje inaendelea.

Agizo nam. 10. Wizara iandae mpango wa kupatikana usafiri wa uhakika kwa ajili ya usimamizi wa misitu.

Utekelezaji. Wizara imeaanda mpango wa upatikanaji wa usafiri kwa ajili ya maendeleo ya msitu. Jumla ya gari tatu zenye thamani ya shilingi milioni 180 zitanunuliwa katika robo ya pili ya mwaka wa fedha 2017/2018. Gari hizo zitanunuliwa kupitia mfuko wa Jozani, gari moja kwa mapato yanayotokana na makusanyo ya mchanga gari mbili milioni 120.

Agizo nam. 11. Uongozi wa misitu uendelee kutoa mashirikiano ya karibu na wanavijiji wanaozunguka msitu, ili wawe walinzi wazuri wa misitu. Wizara imewawezesha uundwaji wa kamati 57 za uhifadhi wa msitu wa jamii kwa Unguja na Pemba.

Agizo nam. 12. Wizara iendelee kutumia wataalamu watu ili kubuni vivutio vingine vya watalii na wananchi wanaokwenda kutembelea kwenye misitu.

Utekelezaji. Wizara inaendelea kutumia wataalamu katika kubuni na kuwasajihisha wanachi kutumia vituo vya utalii vilivyomo kwenye misitu ya Zanzibar, ikiwemo Misitu ya Masingini, Jozani, Kiwengwa na Ngezi.

Katika msitu wa Masingini ujenzi wa mnara umekamilika na ujenzi wa miundombinu mingine ya kuendeleza kituo hicho inaendelea kujengwa. Aidha, serikali imetoa shilingi 50 milioni kuendeleza hifadhi hiyo.

Agizo nam. 13. Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, iangalie uwezekano wa kujenga njia ya kuelekea msitu wa Ngezi. Wizara inaahidi kwamba itashirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, ili kutafuta mbinu za kujenga barabara hiyo pale ambapo uwezo wa kifedha utaruhusu.

Agizo nam. 14. Wizara kwa kupitia mapato yanayotokana na msitu wa Ngezi ijenge majengo kwa ajili ya wafanyakazi. Wizara inakusanya wastani wa shilingi milioni 6 kwa mwaka kutokana na mapato ya watalii katika msitu wa Ngezi, mapato hayo hayakidhi ujenzi wa nyumba kwa ajili ya wafanyakazi. Aidha, wizara inatayarisha mpango kazi ambao utasaidia kuinua mapato katika hifadhi hiyo na kufanya mapitio ya bei ya kuingilia kwa watalii. Jitihada zinafanyika za kuwasiliana na wafadhili ambao watasaidia kuendeleza hifadhi hiyo ya Ngezi. Kwanza tunashukuru Shirika la Norway kwa kuendeleza msitu huu wa Ngezi kwa nguvu zao zote. *(Makofi)*

Agizo la 15. Wizara iongeze juhudi ya kupanda miti ya asili katika eneo la msitu wa Masingini. Wizara inaendelea na utaratibu wa kuongeza upandaji wa miti ya asili ili kuongeza uhifadhi wa asilia katika hifadhi ya Masingini, ambapo msimu wa mwaka 2016 miti 30,100 ya asali na matunda hekta 26 ikiwemo mikungu, mikangazi, mifenesi, pilipili doria, mifuu, mitufaa, mizambarau, miharita, mitondoo, mibirimbi, mishokishoki, midoriani, miembe na miti ya ulaya imepandwa. *(Makofi)*

Agizo nam. 16. Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha mkahawa yaani *Restaurant* katika msitu wa Masingini ambao utakuwa na vyakula vya asili, vikiwemo mihogo, viazi na mashelisheli, ili uweze kujitangaza zaidi. Wizara imetayarisha mpango kazi wa uendelezaji wa hifadhi ya msitu wa Masingini. Ujenzi wa mkahawa unatarajiwa kuanza katika robo tatu ya mwaka 2017/2018. Jumla ya shilingi milioni 60 zimeombwa serikalini kwa ajili ya ujenzi wa mkahawa huo.

Idara ya Utumishi Uendeshaji ina hoja 6

Hoja ya 1. Serikali itamke rasmi kwa yeyote anayemiliki shamba la serikali kinyume na utaratibu, alirudishe na itowe tamko kali kwa atakayekataa kulirudisha.

Utekelezaji. Wizara kwa hatua ya kwanza imetoa tamko rasmi. Aidha, wizara kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama vitamchukulia hatua za kisheria mtu yeyote atakayekiuka tamko hili. Mhe. Mwenyekiti, pia wizara inaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya pamoja na Masheha na wananchi wote watoe ushirikiano wa dhati kwa wizara, ili kuyatambua mashamba yaliyobaki na yaweze kutumika kwa maslahi ya wananchi. Wizara itatoa tamko rasmi kwa kupitia vyombo vya habari kwa kushirikiana na wizara zenye dhamana ya biashara na tawala za mkoa.

Hoja ya 2. Utaratibu wa ukodishaji wa mashamba ya serikali, tuwe wazi ili kuepuka malalamiko yaliopo. Ukodishwaji wa mashamba ya serikali yamefanyika kwa uwazi, ambao zabuni zilitangazwa kwa kupitia vyombo vya habari vya ndani, ikiwemo redio Zanzibar na gazeti la Zanzibar Leo.

Aidha, jumla ya mashamba 4 yamekodishwa kwa zabuni na mashamba 1460 yamekodishwa kwa mnada. Wastani wa shilingi bilioni 2.1 zilikusanywa kwa

ukodishwaji wa mashamba ya serikali ya mikarafuu, kinyume na hapo nyuma ambapo hatuzidi kupata milioni 200 au milioni 300.

Hoja ya 3. Wizara kwa kushirikiana na wizara ya utumishi wa umma itowe vipaumbele vya ajira kwa wataalamu wa kilimo, mifugo na uvuvi ili kuimarisha sekta hizo nchini.

Utekelezaji. Wizara kwa hatua ya kwanza imeajiri wafanyakazi 37 kwa Unguja na Pemba. Hatua ya pili, wizara imewasilisha maombi 72 ya kujaza nafasi tupu. Wizara pia imeorodhesha wahitimu wa Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa mazingatio ya ajira ya mabibi shamba na mabwana shamba. Taarifa hizo zimewasilishwa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mazingatio.

Hoja ya 4. Wizara ihakikishe watumishi wote walioondoka na vyombo vya moto vya wizara vinarudishwa wizarani. Wizara imetekeleza agizo hilo ambapo hadi sasa imekusanya jumla ya magari 13 na pikipiki 15 na kuweka katika utaratibu wa sheria.

Hoja ya 5. Wizara iandae mkakati na utaratibu maalum ili kuhakikisha kuwa wataalamu wanaosomeshwa na wizara hawaondoki na wanazitumia taaluma zao kwa ajili ya kuimarisha shughuli za wizara.

Utekelezaji. Wizara imeandaa mkakati wa mafunzo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kuwataka watumishi wote kujaza mkataba huu kabla ya kuanza masomo ili kuwadhibiti wanapomaliza masomo yao kuendelea na kazi katika ofisi walizotoka. Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kifungu cha 76(1) kinafafanua.

Hoja ya 6. Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, pamoja na Masheha na wananchi wote watowe ushirikiano wa dhati kwa wizara, ili kuyatambua mashamba yaliyobaki na yaweze kutumika kwa maslahi ya wananchi. Kazi hii imeanza kwa kazi kwa upande wa Masheha na Wakuu wa Wilaya, na jumla ya Mashamba 174 yametambuliwa kwa kupitia kwa Masheha wa Pemba.

Chuo cha Kilimo Kizimbani kina maagizo 3.

Agizo la 1. Mara baada ya Mshauri Mwelekezi kuwasilisha maoni yake na kuangaliwa kwa kina, wizara iandae mipango haraka kwa matumizi ya shamba hilo. Mshauri Mwelekezi kwa kupitia mfumo wa zabuni hakupatikana kutokana na kukosa sifa za kufanyakazi hiyo. Kwa hivyo, SMZ ilishauriana na SMT kuhusu namna bora zaidi ya upatikanaji wa eneo la Makurunge. Baada ya mashauriano hayo SMZ imetoa muongozo kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi ya Tanzania Bara, ili Shirika la Nyumba la Taifa litekeleze kazi ya upimaji wa Shamba la Makurunge Bagamoyo.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilitekeleza agizo hilo na kwa kushirikiana na *NHC*, tayari imeandaa makubaliano yenye kuonesha majukumu ya wizara, na

majukumu ya *NHC* katika utekelezaji wa kazi hiyo. Hatua inayofuata ni kukutana na wataalamu wa pande zote mbili, ili kujadiliana njia bora ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Kuhusu upatikanaji wa hati miliki, wizara imearifiwa na Halmashauri kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji ya Tanzania Bara ya mwaka 2007, endapo SMZ itasisitiza kuendelea kupatiwa hati miliki ya shamba kwa matumizi asili. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kimsingi haina pingamizi na utoaji wa hati miliki kwa shughuli za kilimo na mifugo kwa masharti yafuatayo.

1. Kwanza SMZ ilipie gharama za utengenezaji wa hati hiyo ambazo ni shilingi za Kitanzania bilioni 1,255,399,115/=.
2. Kurejesha na kusarenda hati hiyo baada ya mpango wa mji mdogo wa Bagamoyo kupitishwa rasmi. Kutokana na masharti hayo na kuepuka kwa gharama kubwa isiyokuwa na lazima. Wizara imeona ni busara kuendelea kuandaa mpango mpya wa matumizi ya Shamba la RAZABA kama ilivyoelekezwa na SMZ

Idara ya Mpango wa Sera ya Utafiti ina hoja 18

Hoja ya 1. Wizara itafute njia bora ya kuhakikisha kuwa takwimu zinazotolewa na wizara zinakuwa sahihi na tuondokane na utaratibu wa kimazoea wa kukusanya takwimu.

Wizara imetayarisha njia zifuatazo za ukusanyaji wa takwimu sahihi.

1. Wizara, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu imetoa mfunzo kwa wafanyakazi 30 juu ya ukusanyaji wa takwimu. Wizara imetayarisha muongozo wa ukusanyaji, uchambuzi na uandishi wa ripoti ya taarifa za takwimu kuanzia ngazi ya shehia hadi taifa.
2. Wizara, imetayarisha kalenda maalum ya ukusanyaji wa takwimu na aina ya takwimu zinazopaswa kukusanywa.
3. Wizara, imefanya utafiti wa mazao ambayo yalikuwa hayarikodiwi ipasavyo, zikiwemo embe, nazi na machungwa ambayo yatasaidia kujua hali halisi ya uzalishaji wake.

Idara ya Maendeleo na Uvuvi

Agizo. Serikali ihakikishe kusimamia kuzuwia uvuvi haramu, unaofanywa na baadhi ya wavuvi pamoja na kutafuta vyombo vya kutosha, kwa ajili ya kufanya doria za baharini na kuwachukulia hatua za kisheria pale wanapobainika.

Utekelezaji. Wizara inashirikiana na vyombo vya dola KMKM na Polisi na jamii kufanya doria za baharini. Watendaji wa wizara kwa kupitia vyombo vya habari wanatoa elimu ili kudhibiti uvuvi haramu.

Wizara inazifanyia matengenezo boti zake za doria na ina mpango wa kuziongeza ili ziweze kukidhi haja.

Vile vile wizara iendelee na utaratibu maalum wa usimamizi wa madiko, kwani baadhi ya madiko yanaonekana hayatunzwi vizuri na yanatumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa.

Utekekezaji. Wizara imeyatathmini madiko na kugundua yafuatayo.

Jumla ya madiko 80 yametathminiwa kati ya madiko 8 yamepatiwa hati miliki ambayo ni Fumba, Kendwa, Tazari, Nungwi, Matemwe, Pwani Mchangano, Uroa na Kikungwi. Wizara imeshaomba nafasi za ajira 65 katika wizara husika kwa kufuatilia ufumbuzi tatizo la wafanyakazi.

Wizara iunge mkono Wenyeviti wa Kamati za Wavuvi ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo pasi na kuingiliwa na watu wengine. Wizara imeunda Kamati ya Wavuvi na kuendeleza kutoa taaluma za usimamizi endelevu katika kazi ya uvuvi, kwa kupitia kamati husika.

Aidha, wizara ipo karibu na Wenyeviti wa Kamati za Uvuvi, kwani wao ndio wasimamizi wakuu katika Sheria husika. Wizara imewaelimisha Wenyeviti wa Kamati za Wavuvi, ni kuwaelekeza kazi zao ipasavyo kwa kuzingatia sheria na kanuni za uvuvi.

Pia kwa kupitia Mradi wa *SWIOFish,* wenyeviti pamoja na wajumbe wengine wa kamati walipatiwa mafunzo maalum, kuhusu utawala bora katika usimamizi wa uvuvi ambayo yalikuwa na madhumuni ya kuwawezesha kutekeleza usimamizi mzuri wa kazi za uvuvi.

Vile vile, kwa kupitia vikao vya Kamati Tendaji za Wavuvi, wenyeviti hupata nafasi ya kuelimishwa wajibu wao wa utekelezaji wa majukumu yao, zikiwemo sheria na kanuni za uvuvi.

Wizara, imeanza mchakato wa kutayarisha muongozo wa utaratibu wa uendeshaji wa Kamati za Uvuvi. Kwa kupitia muongozo huo wenyeviti watapatiwa mafunzo ya aina mbali mbali ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Wizara, iendelee kutoa elimu kwa wavuvi ili wafahamu umuhimu wa kuwepo kwa maeneo ya uhifadhi baharini. Wizara inaendelea kutoa elimu kwa wavuvi juu ya umuhimu wa uhifadhi wa rasilimali za baharini katika maeneo yote ya bahari, kwa lengo la kutunza rasilimali hizo na mazingira yake.

Wizara, ihakikishe kuwapatia vitambulisho wajumbe wa kamati za uvuvi ili waweze kufanyakazi zao kwa kujiamini. Wizara imechapisha vitambulisho na imewachapia wajumbe wote wa Kamati za Uvuvi. Hata hivyo, baadhi ya kamati zimefanya uchaguzi hivi karibuni na kupata wajumbe wapya. Wizara pia inakusudia kutoa vitambulisho kwa wajumbe wapya pamoja na wale ambao hawakupata hapo awali.

Mhe. Mwenyekiti, Kabla ya kuanza ujenzi wizara ijiridhishe kuwa eneo la ujenzi halitakuwa na athari yoyote ya bahari kwa baadae katika eneo la ujenzi.

Utekelezaji. Utafiti wa hali ya bahari pamoja na thamani ya kimazingira zimefanyika, ili kuhakikisha hakuna athari zozote zinazojitokeza baada ya ujenzi. Aidha, ujenzi wa vituo vya utafiti na mabwawa utazingatia pia Sheria Nam. 3 ya Mazingira ya Zanzibar, inayosisitiza kufanyika kwa tathmini ya mazingira.

Tukizingatia kuwa Zanzibar inaelekea katika uchumi wa bahari kuu, soko pia liendane na ujenzi wa kisasa, ili kuimarisha uvuvi nchini na kuwavutia wawekezaji.

Soko la Samaki litakalojengwa Malindi kwa uhifadhi wa *JICA* na SMZ, litakuwa na miundombinu na huduma zote muhimu ambazo zitasaidia kuimarisha sekta ya uvuvi hapa nchini. Kuendeleza uchumi kwa kupitia rasilimali za bahari na kuongeza uhakika wa salama wa chakula kwa wananchi.

Wizara ihakikishe kuwa mradi unasimamiwa vizuri ili kuhakikisha kuwa unamalizika kwa wakati kama ulivyokubalika katika mkataba.

Utekelezaji. Wizara itahakikisha usimamizi mzuri wa mradi wa soko la kisasa la samaki la Malindi, kwa kuunda timu maalum ya usimamizi wa mradi, ili kuhakikisha unatekelezwa vizuri na unamalizika kwa wakati.

Aidha, kwa mujibu wa makubaliano na Shirika la *JICA* mkandarasi wa ujenzi atatoka Japan na kusimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na *JICA* yenyewe.

Wizara itoe mashirikiano mazuri kwa wavuvi wanaotumia eneo hilo, wakati utakapoanza ujenzi huo wa kuwatafutia eneo jengine kwa kipindi chote cha ujenzi wa soko.

Serikali imeliangalia kwa kina suala hilo na tayari imeshawapangia wavuvi na watumiaji wengine utaratibu mzuri utakaopunguza usumbufu wakati wa ujenzi.

Busara itumike ili kuhakikisha wananchi wanalitumia soko la Tumbe. Mazungumzo yanaendelea na wanakijiji wa Tumbe tayari wameshawasilisha wizarani kamati yao ya soko, na tunategemea baada ya muda mfupi wataanza kulitumia soko hilo bila ya matatizo. *(Makofi)*

Serikali iangalie uwezekano wa kufanya matengenezo ya kasoro zilizopo, ili soko la Tumbe liwe na mazingira mazuri kwa watumiaji wake.

Utekelezaji. Baadhi ya miundo ya maji tayari imetengenezwa na mingine inaendelea baada ya makubaliano ya kamati ambayo tayari imeshaundwa.

Wizara ihakikishe inatafuta njia ya kuingiza mashine ya barafu katika chumba kilichojengwa katika soko la Tumbe.

Utekelezaji. Wizara tayari imeshatafuta mtaalamu wa kuangalia mtambo wa barafu ambao kwa kipindi kirefu umekaa bila ya kufanya kazi, endapo mtambo huo utakuwa

mzima utaingizwa sokoni kwa makubaliano na kamati ambayo tayari imeshaundwa. Mtambo huo ulinunuliwa mwaka 2010, lakini haukuweza kufanyakazi hata siku moja.

Serikali imepanga kujenga Bwawa la Samaki katika eneo la Maruhubi kwa ajili ya uanzishaji wa vifaranga vya samaki, ili wafugaji waondokane na changamoto ya ukosefu wa vifaranga.
Utekelezaji. Ujenzi wa kituo cha kuzalisha vifaranga, yaani *hatchery* ya samaki, umeanza rasmi mwezi Julai 2017, huko *Beit-el-Ras* na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba 2017. Mradi huo unaendelea kwa mujibu wa ratiba na utaratibu uliokubalika hapo awali.

Wizara iendelee kutoa elimu kwa wafugaji wa samaki ili watumie njia za kisasa za kitaalamu katika kufanya shughuli zao kwa lengo la kuwa na uzalishaji mkubwa wa samaki. Wizara inawawezesha wafugaji wa samaki kwa kuwapatia mafunzo ya ufugaji bora wa samaki.

Aidha, kwa kipindi cha miaka miwili 2016/2017 wafugaji 60 wamepatiwa mafunzo ya ufugaji bora wa samaki kutoka kwa wataalamu wa Kichina. Hadi hivi sasa Zanzibar ina vikundi 144 vya ufugaji wa samaki.

Kutokana na kuimarika kwa shughuli za uvuvi na kuhamasika kwa ufugaji wa mazao ya baharini, serikali iandae mpango wa kuanzisha kituo cha utafiti wa mazao baharini ili kiweze kuwasaidia wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini.

Utekelezaji. Wizara kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Vietnam imeandaa andiko la mradi wa kuanzisha kituo cha utafiti wa mazao ya baharini. Wizara kupitia mradi wa *SWIOFish*. unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, imetenga wastani wa dola laki tatu za Kimarekani kwa ajili ya kujenga kituo cha utafiti cha uvuvi katika eneo la Maruhubi.

Aidha, mshauri mwelekezi kwa ajili ya kuandaa michoro ya kituo hicho tayari ameshapatikana.

Wizara kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika iangalie namna gani itaweza kuwasaidia wafugaji wa mazao ya baharini kupata mikopo. Wizara imeanza mazungumzo na taasisi za kifedha, Benki ya Maendeleo ya Kilimo, *CRDB* na *NMB* ili kupata mikopo ya kuwapatia mitaji wafugaji wa samaki.

Aidha, jumla ya vikundi 119 vya wazalishaji wa sekta za kilimo, wamefanyiwa tathmini kwa ajili ya kupatiwa huduma za fedha kwa kupitia benki hizo, hatua hiyo inasubiriwa ni kuja kwa bei ya benki hizo kwa kuangalia tathmini ya mwisho iliyofanywa.

Kamati imeitaka serikali kuleta mbele ya Baraza la Wawakilishi Sheria ya Kuanzishwa Mamlaka Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania, ambayo ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kukidhi masharti ya kifungu cha 132 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Wizara kupitia Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania imekamilisha utaratibu unaohitajika na ipo tayari kuwasilisha sheria hiyo wakati wowote baada ya kupita kwenye Baraza la Mapinduzi.

Afisi Kuu Pemba Afisi kuu Pemba ina mambo tisa (9)

Wizara itakapotoa nafasi ya ajira iangalie upungufu uliopo kwa upande wa Pemba. Kwa mwaka 2016/2017 jumla ya wafanyakazi 49 wameajiriwa kwa kada tofauti wakiwemo Mbwanashamba na Mabibishamba, wahudumu mashambani, madereva, walinzi, mafundi wa matrekta na mafisa wasaidizi uvuvi, mifugo na misitu.
Wizara ihakikishe inatoa ushirikiano katika kipindi chote cha uundaji wa bajeti kwa mwaka huu kwa Afisi kuu Pemba. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wakuu wa Idara zote kutoka Afisi Kuu Pemba wameshirikiana na wenzao waliopo Unguja kwa lengo la matayarisho ya bajeti.

Afisi iendelee kutumia OC zake kwa ajili ya kupunguza madeni ya wafanyakazi, jumla ya wafanyakazi 202 wanawake 107 na wanaume 95 wamelipwa fedha zao za likizo shilingi 20, 200,000/= kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Wizara ihakikishe anapatikana mwanasheria katika Afisi Kuu Pemba kabla ya mwezi wa Septemba, kwani zipo changamoto nyingi za kisheria ambazo zinahitaji uwepo wa mwanasheria, wizara inatarajia wanasheria wawili Pemba katika nafasi mpya za mwaka 2017/2018.

Wizara iendelee kusomesha wataalam wake kwa kuwajengea uwezo wa kufanya tafiti zinazokwenda na wakati kwa upande wa Pemba. Mtaalam mmoja wa utafiti yuko masomoni kwa ngazi ya *PhD*, wizara inaendelea kuwafundisha wataalam wake walioko Pemba hatua kwa hatua kwa kuendana na uwezekano wa kibajeti na rasilimali watu.

Serikali iongeze bajeti ya taasisi ya utafiti Pemba ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi. Wizara imeanza kuchukua hatua kwa kulitafutia tatizo la bajeti kwa kuzingatia mgao wa bajeti. Mwaka uliopita taasisi za utafiti zilikuwa shilingi milioni 25 mwaka huu zimepewa milioni 63 sawa na ongezeko la asilimia 252 la ongezeko ya bajeti ya mwaka uliopita.

Wizara iangalie uwezekano wa kujenga ukuta katika eneo la Kituo cha Utafiti ili kuliekea eneo hilo uzio katika hali ya usalama, kazi ya ujenzi wa ukuta wa kuzunguka eneo la kituo tayari imeshaanza kwa kujenga mita 50 kati ya 1600 za uzio wake. Matarajio ni kuendeleza ujenzi huo hadi kukamilika mzunguko wote.

Serikali itafute vifaa vya maabara kwa ajili ya kuendeshaji wa shughuli za kituo hicho. Wizara imekamilisha upatikanaji wa vifaa vya Maabara Kuu ya Utafiti iliyopo Kizimbani Unguja kwa mwaka huu wa fedha, hii ni kutokana na ukomo wa bajeti kwa mwaka huu, ambapo haiwezeshi wizara kupata vifaa kwa maabara zote mbili.

Wizara itenge fedha kwa ajili ya kuunganisha huduma za mtandao katika eneo hilo. Juhudi za kupatikana huduma za mtandao zinaendelea kuchukuliwa tayari yamefikiwa makubaliano baina ya Shirika la Simu Tanzania *TTCL* kufunga mitandao ya huduma za

internet kituoni hapo ufungaji wa mitandao hiyo inafanyika na fedha tayari zimeshapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusoma yote hayo naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Mweneykiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa ripoti yako. Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimwite Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Awali ya yote, napenda kuelekeza shukurani zangu kwa Mtukufu wa Ulimwengu na muumbaji wa viumbe vyote mbinguni na ardhini kwa kutujaalia uhai na afya njema tukaweza kukutana katika Baraza hili Tukufu, kwa lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar, kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao, ambapo leo tupo hapa kupitia na kujadili Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyowasilishwa katika Baraza hili tukufu katika kikao cha mwezi wa Febuari, mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa hii ni mara yetu ya kwanza kutumia utaratibu huu wa kuwasilisha utekelezaji wa maagizo ya Kamati mbele ya Baraza lako hili tangu kufanyiwa marekebisho kwa Kanuni ya Baraza letu, Toleo la 2016. Sina budi kuipongeza Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuona umuhimu wa kulifanya hili kwani hapo, kuwepo utaratibu huu, mafanikio zaidi yatapatikana kwani baada ya uwasilishaji wa utekelezaji wa maagizo ya Wizara, Baraza litakuwa na fursa nyengine ya kuweza kuthibitisha yale yaliyoelezwa kupitia ziara zake mbali mbali za Kamati za Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, Nachukua fursa hii kuthamini juhudi anazochukua Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi za kutekeleza ipasavyo Ilani ya CCM kwa kutimiza ahadi zake ambazo aliwaahidi wananchi wa Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Kupitia juhudi zake, wananchi wa Zanzibar sasa wanafaidi matunda mazuri kupitia yale aliyoyatekeleza na anayoendelea kuyafanya hususan katika masuala mazima ya kikiimarisha Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie uwezo huo na amjaalie maisha marefu yenye kheri na yeye. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki, ikiwa nitaacha kumshukuru Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa umahiri wake mkubwa wa kuyasimamia vyema majukumu ya wizara zote za serikali, ambapo Zanzibar na wananchi wetu wananeemeka na mafanikio yanayopatikana kutokana na utekelezaji wa wizara hizo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuelekeza salamu zangu za shukurani kwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi; Mhe. Hamad Rashid Mohammed, Naibu Waziri; Mhe. Lulu Msham Abdalla kwa ushirikiano wao mkubwa wanaoutoa kwa kamati ambao unapelekea kupatikana ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yetu, Lakini pia, shukrani za dhati

zimuendee, Katibu Mkuu mpya wa Wizara hiyo ndugu Joseph Abdalla Meza, Manaibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Ofisi yake kwa kushirikiana nasi katika kazi zote za kamati yetu. Kamati inamueleza Katibu Mkuu Meza kwamba Kamati ipo tayari kufanya kazi nae na inamkaribisha sana katika harakati zote za kuwatumikia wananchi wetu kwa kuhakikisha masuala yote ya kilimo, maliasili, mifugo na uvuvi yanaimarika ipasavyo Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kupoteza muda, sasa naomba niwatambue kwa kuwataja majina yao Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambao walitoa mchango na ushauri mkubwa katika utekelezaji wa kazi za Kamati hii, Wajumbe wenyewe ni:-

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Mwenyekiti;
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Makamo Mwenyekiti;
3. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Mjumbe;
4. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Mjumbe;
5. Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe;
6. Mhe. Ussi Yahya Haji - Mjumbe; na
7. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Mjumbe.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu pia inashirikiana ipasavyo na makatibu wawili (2) kutoka Ofisi ya Bazara ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia kutekeleza majukumu yetu, kwa heshima naomba niwatambue makatibu hao ni:

1. Ndugu Asma Ali Kassim - Katibu
2. Ndugu Said Khamis Ramadhan - Katibu

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine, kamati yetu inalo jukumu la kupitia, kuchambua na kujiridhisha na majibu yaliyowasilishwa na wizara hii kuhusu utekelezaji walioufanya wa maagizo yaliyotokana na ziara zilizofanywa na kamati yetu katika kipindi kilichopita na kuwasilisha ripoti yetu hapa Barazani katika mwezi wa Februari, 2017. Leo hii, Kamati yetu inawasilisha hotuba hii ikiwa ni utekelezaji wa Kanuni ya 108 fasili ya (15) ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hiyo, kamati yetu iliwasilisha Maagizo 72 ambayo Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ilitakiwa kutoa majibu majibu katika kikao hichi cha mwezi wa Septemba au Oktoba. Napenda kulieleza Baraza kwamba kamati yetu ilipokea, ilipitia na kujadili ipasavyo utekelezaji wa maagizo hayo. Kiujumla,

kamati yetu ilikubaliana na majibu yaliyotolewa na watendaji wa wizara na kuyaunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe Mwenyekiti. kamati inaipongeza sana wizara kwa kukamilisha ipasavyo utekelezaji wa maagizo ya kamati kwa kuanzisha Taasisi Maalum ya Utafiti wa Mifugo, ambayo itatumika kufanya tafiti za mifugo hapa nchini. Kamati inaimani kwamba kuwepo kwa taasisi hiyo kutaiwezesha wizara na wananchi wetu kutambua matatizo yanayowakabili wafugaji na kuyatafutia ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imeridhishwa sana na hatua iliyochukuliwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa juhudi zake za kuanza utekelezaji wa agizo la kamati kuhusu uanzishwaji wa Bwawa la Kufugia Samaki *(hatchery)* kwa ajili ya uzalishaji wa vifaranga vya samaki ili wafugaji waondokane na changamoto ya ukosefu wa vifaranga.

Kamati ilipata fursa ya kutembelea katika eneo la *Beit-el-Ras* ambapo mradi unafanyika na kujiridhisha hatua iliyofikia ujenzi huo unaoendelea huko na kutarajiwa kumalizika mwezi wa Novemba mwaka huu. Hivyo, kamati inasisitiza kwamba Wizara iongeze bidii katika kusimamia vizuri wajenzi pamoja na kuhakikisha maendeleo endelevu ya kuuimarisha mradi huo, ili uweze kudumu kwa muda mrefu na kuiletea tija Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu hainabudi kuipongeza Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa utekelezaji wa agizo la kukamilisha upatikanaji wa vifaa vya Maabara Kuu ya Utafiti iliopo Kizimbani Unguja. Maabara hizi zitatusaidia kufanya utafiti mbali mbali na kupata ufumbuzi wa changamoto zinazoikabili sekta yetu ya kilimo Zanzibar. Pamoja na mafanikio hayo, jitihada za makusudi zinahitajika kwa ununuzi wa vifaa hivyo kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu kwa kiasi kikubwa ilikubaliana na utekelezaji wa agizo la uimarishaji wa Msitu wa Hifadhi wa Masingini kwa kuendelea kupanda miti mbali mbali ikiwemo mikungu, mifenesi na miharita. Hivyo, kamati inaipongeza sana wizara kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka kwa kuwa na azma nzuri ya kuuendeleza Msitu wetu wa Masingini. Lakini kamati yetu imeishauri wizara kuongeza katika orodha ya miti ambayo imekusudia kuiimarisha katika msitu huo ikiwemo miti ya asili ya Mivule na Misaji. Hili linatokana na uasili wake wa kuwepo na kuoteshwa hapa Zanzibar pamoja na umuhimu wake kiuchumi, kimatibabu na kiutalii.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu agizo la kuliimarisha Shamba la Mifugo Pangeni. Kamati iliarifiwa kuwa kupitia mradi wa miundombinu ya mifugo wizara itachimba kisima ili kuondoa tatizo la maji sambamba na kuifanyia matengenezo njia ya kuelekea shamba hilo. Kwa kuwa agizo hili halijatekelezwa, kamati yetu itaendelea kulifuatilia agizo hili kwa karibu zaidi ili kuongeza kasi ya utekelezaji na yale malengo yaliyowekwa na serikali kwa Shamba la Pangeni yaweze kutimia kwa asilimia kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu ilipokea utekelezaji wa agizo la kuusimamia ipasavyo Mradi wa Soko la Kisasa la Samaki la Malindi, ili kuhakikisha mradi unatekelezwa vizuri na unamalizika kwa wakati. Kamati iliarifiwa kuwa wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi wataunda timu maalum ya kusimamia utekelezaji wa mradi huo ambao utaanza mwaka huu. Kamati yetu itazidi kuufuatilia mradi huu kwa karibu, ili soko hili la Malindi liweze kutoa huduma kama ilivyokusudiwa na serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kutaka kujua kwa kiasi gani wizara inaimarishaje Mpango wa Rasilimali watu katika idara zake hususan kwa upande wa Pemba, ili kutatua changamoto ya ukosefu wa wafanyakazi. Kupitia utekelezaji uliowasilishwa, wizara ilieleza kwamba wafanyakazi walioajiriwa kuwa ni 49 kwa kada tofauti kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kamati inapongeza juhudi hizo ila inasisitiza apatikane mwanasheria, ili awe mwarubaini wa changamoto zinazojitokeza kwa upande wa Pemba.

USHAURI WA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti, mbali na maelekezo ambayo kamati yetu ilitoa ushauri kwa Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa nia njema waliyonayo ya kuhimiza na kusisitiza utekelezaji wake. Miongoni mwa mambo hayo ni:

1) Pamoja na kwamba Zanzibar haiwezi kujitosheleza katika uzalishaji wa mifugo ya kutosha kwa ajili ya nyama na maziwa. Hivyo ni vyema wizara ikawa na mpango mkakati maalum wa kuwasaidia mitaji wafugaji wetu wa ndani ili waweze kuzalisha zaidi na kutatua changamoto hiyo.

2) Pamoja na kutatuliwa kwa Chinjio la Kisakasaka, kuna haja ya chinjo hilo kuimarishwa na kupatiwa miundombinu imara, ikiwemo kuiwekea lami barabara iliyoelekea eneo la chinjio, kwa vile chinjio hilo ni rasilimali kubwa katika upatikanaji wa mapato ya serikali na mahitaji ya nyama kwa matumizi ya kila siku kwa wananchi wetu.

3) Pamoja na kuwa na Sera ya Kijani *(GreenPolicy).* Wizara inatakiwa kuhimiza upandaji wa miti kwa kuwatumia watumiaji na wakaazi katika maeneo husika. Kwa mfano, Idara Maalum zote na Serikali na Skuli za Zanzibar zipande na kuiimarisha miti katika maeneo yanayowazunguka.

4) Pamoja na serikali kumiliki Shamba liliopo Makurunge. Juhudi za makusudi zinahitajika kuchukuliwa, ili kuliimarisha shamba hilo lipate kuwa na tija na serikali. Kamati inaipongeza wizara kwa jitihada walizofikia ya kuandaa rasimu ya makubaliano (MoU) baina ya Shirika la Nyumba la Taifa na Wizara yetu ya kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa

nikiwasilisha hotuba hii. Aidha, salamu zangu za pongezi pia zimwendee Mwenyekiti wangu wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Wajumbe wake wote kwa kukubali kuniteua mimi kuwasilisha hotuba hii kwa niaba yao kwenu Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine nikuombeni Waheshimiwa Wajumbe muijadili, mutoe ushauri pamoja na mapendekezo yenu na hatimae muunge mkono utekelezaji wa Maagizo haya.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hamad Abdalla Rashid kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea na mchangiaji wetu wa mwanzo naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali, akifuatiwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani na Mhe. Miraji Khamis Mussa ajitayarishe.

Mhe. Ali Suleimam Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kuichangia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa taarifa yake ya kamati ya mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambazo wanafanya kuhakikisha kwamba mambo mbali mbali tunafanikiwa kwenye chakula cha aina mbali mbali.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nampa pongezi za pekee Mhe. Waziri, kwa kazi zake nzuri na juhudi yake ambayo tunamuona, kwa sababu mimi husema kila siku Mhe. Waziri, Katibu nani wote haki yao ya kutembea katika maeneo kujua mazingira ya shida za watu, sio kukaa ofisini na kupulizwa na vipoza hewa au mafeni wakati huo umepitwa na wakati Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ana bidii ya peke yake na bahati nzuri na Naibu Wake sasa hivi kabadilika sana mimi nampongeza sana Mhe. Lulu Msham Abdalla najua ulezi kazi, lakini bado kaleleka vizuri na sasa hivi anafuata kwenye muelekeo ambao unatakiwa, pia katika majibu yake anayojibu sasa hivi tunasema ka-*improve* sana katika mambo yake ya maendeleo katika shughuli zetu, hongera sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kilimo ni uti wa mgongo wa nchi yetu na kilimo ndio roho ya nchi yetu, bila ya kilimo tutaharibikiwa sana katika maendeleo mbali mbali katika nchi yetu kilimo kina mambo mengi kuna kilimo cha mwani, kilimo cha mpunga, kilimo cha mihogo, mboga mboga na mambo mengineyo. Lakini pia tunategemea kwamba Zanzibar ni sehemu moja ambayo tunategemea sana chakula cha mchele kwa asilimia 90% ya Wazanzibari wanapenda chakula cha mchele.

Safari hii kwa mara ya kwanza nilipata taarifa tu namuomba Mhe. Waziri aje atupe jibu kuhusu taarifa hiyo. Kwa kweli, uliuzwa mchele kule Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi mchele huo ulikuwa unauzwa lakini una foleni kubwa sana tuliambiwa bei yake kuanzia 1,600/-, 1,800/- na 2,000/- lakini kama huna ubavu huupati, nasikia mbegu hiyo tamu sana na nzuri na watu walikuwa wanashinda hapo kwa foleni wanagombania. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba akija atupe maelezo na tuelewe wapi unapatikana na kiasi gani tani ngapi tulipata na wananchi wamenufaika kiasi gani. *(Makofi)*

Bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti sikubahatika kuuonja mchele huo au wali wake, lakini waliouonja waliokula wanasema ni wali mzuri wa ajabu. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri sana katika utafiti wao waiongeze hiyo mbegu kwa wakulima mbali mbali, ili wananchi wetu wafaidike na mchele huo mpya wa kisasa kabisa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, uvuvi ni sehemu moja kubwa katika nchi yetu, ambayo kisiwa chetu narudi kila siku tumezungukwa na bahari juzi nimeziona meli ya uvuvi za Kichina, na meli zile tunaambiwa hivi sasa hivi vijana wetu wengi wachaanza kupata ajira katika meli hizo. Naomba nimuulize Mhe. Waziri na hili, je meli hizi zipo hapa kwa muda gani na zitafanya kazi katika maeneo gani, lakini pia vijana wetu kwa bahati mbaya wengi lugha ya Kichina hawana wanasaidiwa na nani katika kuendelea kushirikiana na Wachina ambao wanavua katika bahari kuu.

Tumesikia kwamba juzi wameanza Dar-es-Salaam na hapa wamekuja na wamepokelewa vizuri. Kwa hivyo, hiyo ni changamoto ya mafanikio na naamini kwamba itaongezwa mipango basi vijana wetu wengi watapata faida ya ajira katika sehemu ya uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, bado wavuvi wetu wengi ni masikini na wavuvi wetu wana nyezo duni katika kufanya kazi zao za uvuvi. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na kuona kwenye taarifa hii, kuna mipango kadhaa imeandaliwa kupatikana vyombo vya kisasa vya uvuvi lakini huko nyuma tunapotoka vilikuwepo vyombo vingi sana viligawiwa katika madiko mbali mbali, sijui vipo wapi. Kwa kweli, hatujui kama viliuzwa au watu wamegawana wakafanya wanavyotaka lakini azma ya serikali ilikuwa vyombo vile visaidie wananchi wetu wapate ajira na kusaidia nchi yao katika upatikanaji wa kitoweo cha samaki, lakini chombo vile vimetoweka kabisa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri na kwa mpango huu namuunga mkono mzuri, lakini usimamizi uwe bora, ili kuvilinda vyombo hivyo na kuvijua faida yake visipate hasara.

Mhe. Mwenyekiti katika suala jengine ambalo nitalizungumza Zanzibar tuna rasilimali ya misitu, lakini misitu yetu kwa asilimia kubwa inapotea na kuna misitu yetu ambayo tunaitizama kama misitu ya kitaifa Ngezi na hapa Masingini tumeambiwa inaanzishwa rasmi sasa hivi na zimetengwa pesa kama milioni 60 kwa kuanzia ujenzi wa mkahawa utakuwa mzuri kama kivutio cha watalii au wananchi tu wa kawaida kwenye kutembea kwenye maeneo hayo ya misitu wa asili wa hapa Masingini. Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri autangaze rasmi, haidhuru unatangazwa lakini wananchi wengi hawauelewi, kwa sababu katika sehemu ya Masingini hapa sikukuu kubwa, au siku za

sikukuu tunajua wananchi wetu au vijana wetu au watoto wetu wanakwenda kutembea katika sehemu ya wanyama pale.

Sasa labda tuseme kwa kuwa watoto wanakwenda pale na patakuwa na sehemu ya mazingira ya kwenda kusoma au kujivunza. Kutokana na hali hiyo, ingekuwa ni vyema ukatangazwa rasmi msitu ule fedha naamini zitapatikana vizuri na wananchi watajua faida ya ule msitu uko vipi na maumbile yake, ili wananchi wapate kusoma na kuelewa na kuhifadhi.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti kwa wenzetu Tanzania bara ufugaji wa nyuki, ufugaji wa nyuki ni pato kubwa sana kwa nchi yetu, kwa sababu wenzetu Tanzania bara wanasafirisha na kwenda nchi za nje, lakini kwetu Zanzibar sijaona. Je hawa wafugaji nyuki wamepotea hawapo au mazingira ya misitu yetu haitoshi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri akija hapa atupe maelezo tujue huu ufugaji wa nyuki unakasoro gani au una faida gani tulikoanzia na hapa katikati ukapotea. Lakini naamini wafugaji wako wengi na wanaamini kufanya kazi nzuri, ili tupate faida kwa ajili ya maendeleo ya vijana wetu na serikali kupata pato lake.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na kilimo kizuri kilichotokea safari hii au mavuno yaliyopatikana bado tunahitaji matrekta, matrekta ni kilio kikubwa na matrekta ni sehemu moja ya uzalishaji rahisi lakini venginevyo wananchi wetu wanapata shida, kijembe kongoroka kimepita na wakati. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri matrekta kila eneo yakiwepo Cheju, Kilombero, Pemba sehemu mbali mbali basi wananchi wetu watafaidika na watalima vizuri na faida itapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya machache kwa heshima kabisa nampongeza tena Mhe. Waziri na Naibu wake na watendaji wote wa wizara, lakini nawatakia kheri na mafanikio yetu ya kilimo, ili mchele mpya tuupate na Waheshimiwa Wajumbe wajue wapi unakwenda kununulia, ili wananchi wote wafaidike.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Abdalla Maulid Diwani, akifuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ajiandae.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia katika Taarifa ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuhusu utekelezaji wa maoni. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima nikafika katika Baraza la lako tukufu.

Lakini haraka haraka kwa michango yangu kwanza niipongeze serikali kwa azma nzima wa kuleta utaratibu huu mpya ambao kwa mara ya kwanza unapitia maelezo ya kusimamia namna gani Baraza la Wawakilishi inayofanya moja ya kazi yake ya Kikatiba kuisimamia serikali nashukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Vile vile, nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti na Baraza la Mapinduzi, kwa namna ambavyo anavyotoa maelekezo yake kupitia wasaidizi wake, mawaziri kwa namna gani kuona Zanzibar tunapiga hatua katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu wakwezi, wakulima na wanyonge wa nchi hii namshukuru sana. Sambamba na hilo, ikapelekea mpaka dakika hii imekuwa hata kilio cha mawizara kuhusu upatikanaji wa fedha zao zile za bajeti kuweza kuvuka asilimia 70% na 80% niipongeze sana. Hali hiyo, inaonesha wazi kabisa watu makini aliowachagua Dkt. Ali Mohamed Shein wanasimamia makini zile sera na maamuzi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hilo nampongeza sana. *(Makofi)*

Nikiendelea mbele katika mchango wangu mimi nitaangalia sana katika hili buku lenye taaarifa hizo. Naomba kwenda kwenye agizo nam. 1 naomba nisome halafu nitoe maelezo yangu. Agizo nam. 1 wizara iwasiliane na wazabuni wanaoleta pembejeo za kilimo, ili pembejeo hizo ziwafikie wakulima, utekelezaji inakwambia wizara ikishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imepanga na tayari imeshapata. Je, huyu mtu aliyeshinda hii zabuni si yule ambaye aliyerudishiwa mbegu zile ambazo zilikuwa pembejeo zilizokuwa na matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, lilikuja swali kwenye Baraza hili hili na baadae tukaambiwa imerudishwa. Sasa je, inakuwaje tena katika utekelezaji huu, wa mwaka 2016/2017 kwamba tena anapata nafasi yule yule kuhusu kutuletea mbegu zile, napata shaka na hapo. Kwa kweli, Baraza hili lilikuja swali la Mhe. Masoud Abrahman Masoud kuhusu pembejeo au kuhusu mbolea isiofaa na wizara ikaamua kuirudisha, leo hii kwenye hichi kitabu yule yule yumo.

Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Waziri kidogo napata ukakasi kutokana kwamba hichi kitabu wamekitengeneza wenyewe na wamekipitia wenyewe na leo hii wametuletea sisi humu ndani tena. Wakati suala la huyu huyu sasa tulizungumza humu kwenye Baraza hili na kwamba akarudishia zile pembejeo zake tukaambiwa gharama gani, leo hii tunamuona kwamba kapata tena. Nadhani wakati atakapokuja Mhe. Waziri atakuja kutoa maelezo zaidi namna gani kinachoendelea nataka moja nisimamie hapo.

Lakini mbele nikiendelea Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu cha tano (5) juu ya utekelezaji agizo limetoka, limetoka kwamba wizara ishajihishe wananchi kulima kilimo cha *spices*, kwani kilimo hicho kimekuwa na soko kubwa ulimwenguni. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli soko kubwa ulimwenguni sio leo tu toka zamani *spices* tunajua mpaka Zanzibar imekuwa *Spices Island*, kwa sababu ya wakulima hivyo viungo, lakini chakusikitisha bado tukishatoka karafuu hatuna sisi kiungo chengine tunachojivunia. Kwa mfano, leo hii tukitaka pilipili manga *container* moja hatupati hapa na watu wanahitaji hizo *container*, tukitaka mdalasini leo *container* moja hatupati.

Sasa hapa tunaambia kwamba eti serikali majibu yake ya wizara, wizara ikishirikiana na Asasi Zisizo za Kiserikali ikiwemo *Zenj Spices, Zanzibar Organic Spices Growers* na Kampuni ya *Lecon* ya Ujerumani imewashajiisha vikundi. Je, Mhe. Waziri ni vikundi

vingapi vilivyoshajihishwa, kwa sababu hapa tuko katika utekelezaji wa bajeti ya 2016/2017 na wala sio 2017/2018.

Hivyo, angalau basi angetwambia baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe tumevishajihisha vikundi kumi na tano (15) Charawe, Mwakaje, Uroa na sehemu nyengine wapi na *impact* yake ishapatikana, lakini leo hii ndio kwanza unatwambia kwamba eti imeshirikiana na Asasi Zisizo za Kiserikali inawashajihisha, nini *impact* yake kushajihisha tuone kwamba mazao yanapatikana ndio jibu tunalolitaka sisi, na wala sio vyenginevyo kwenye maandishi wametuandikia wameshajihisha ni mwaka mzima kwa mujibu ya bajeti hii.

Huu utekelezaji huu ni wa mwaka 2016/2017 sio 2017/2018, tuko nje sisi ya muda, sasa ingelikuwa ungetujibu aa baada ya kushajihisha 2016/2017, leo hii 2017/2018 tumeanza kupata *impact* hii, vikundi hivi na hivi tayari vimevishajihisha na tunazo *spices* kiasi hichi, tunawakaribisha wanunuzi au wasafirishaji kupeleka nje ya nchi, ili kuzipeleka kule na kusema *Zanzibar Spice Island* watu wakubali, lakini sio haya ambayo yameandikwa hapa. Kutokana na hali hiyo, ndio napata shaka kama kweli ripoti hii kutoka maagizo ya Baraza la Wawakilishi wamekaa wakajadili kuisoma vizuri, leo hii tukaja tukaipitia tena humu. Mhe. Mohamed Said Mohamed alisema anapata ukakasi kuzipitia hizi ripoti, kwa sababu hazina kitu.

Mhe. Mwenyekiti, sisi bajeti iliyopita 2016/2017 tuliidhinishiwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi shilinigi 48,977,300,000/-. Je, aliweza kupata kiasi gani katika bajeti yake, nusu na robo ya bajeti ameipata, sasa je utekelezaji wake uko wapi ndio huu wakusajihisha bado mpaka dakika hii hakuna kitu.

Nikiendelea mbele Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye agizo nambari 7, wizara iendelee kufuatilia kuhakikisha Shirika la Umeme (*ZECO*) linafanya matengenezo ya nguzo zilizoinama katika bonde la Cheju. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi (*ZECO*) ni Shirika la Serikali lililo chini ya Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati. Agizo mwaka mzima jibu lake tumetwambia kwamba wizara imewasiliana na Shirika la Umeme tayari shirika limebadilisha nguzo 6. Aidha, wizara inaendelea kushirikiana na Shirika la *ZECO* kubadilisha nguzo 7 zilizoanguka narudia tena.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inaendelea, yaani kubadilisha nguzo za umeme Mhe. Waziri ni siku moja tu. Sasa sijui uendelevu huu wa siku ngapi hizo nguzo 7 ziwe mpaka leo wizara inaendelea na *ZECO* kuhakikisha kwamba inabadilisha nguzo, nguzo ya umeme inabadilishwa siku moja tu na tena ndani ya saa moja nguzo imeshahamishwa. Kwa kweli, tulitegemea hapa tuambiwe kwamba *ZECO* washakamilisha zoezi lile tunaangalia jambo jengine, sio leo 2017/2018 tunazungumza Wizara *ZECO* inaendelea *come on* nguzo moja inabadilishwa si chini ya saa moja, leo hii tunaambia.

Kwa hiyo, naona hizi ripoti zenyewe kwa kweli zinatia hata msisimko kuzisoma kwa sisi muliotuletea, jambo tukisema wengine tutaambiwa kwamba tunakuwa wakali tunaigomba sana serikali. Kwa kweli, hatugombi serikali isipokuwa sisi tunataka kusimamia Ilani ya Chama chetu kusimamia serikali yetu na ifanye kazi kwa umakini, ili

kuturahisishia katika Uchaguzi 2020 kupata ushindi wa kishindo. Lakini kwa muelekeo huu mnarudisha kule kupata shida tena mpaka Bwana Jecha atuonee huruma.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele katika agizo nam. 4. Wizara inaendelea kutafuta muekezaji kwa ajili ya kuanzisha viwanda kuzalisha pembejeo za kilimo na mifugo tulikuwa na *ZAPOCO* hapa kuna kiwanda kinazalisha chakula cha kuku kiko wapi. Kwa nini kimekufa. Sasa leo hii nashukuru kuna viwanda vidogo vidogo tu vya wananchi wenyewe wanazalisha Mhe. Mwenyekiti kama havijui Mhe. Waziri hivyo vipo kama vile Amani pale pana viwanda vinazalisha leo hii tunasema kwamba …

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba Mhe. Mjumbe afute kauli yake, sisi hatujaonewa huruma na Jecha.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, afuate utaratibu na ataje Kanuni…

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, sisi hatujaonewa huruma na Jecha. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alishinda kwa asilimia 91. Afute kauli hiyo Zanzibar iliingia katika uchaguzi Zanzibar ...*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri,

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Naam Mhe.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri umesimama lakini hujanambia Kanuni gani imetumia kwa hiyo unasema….

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Kanuni ya 68 na kama siyo tafuta Kanuni wewe Mwenyekiti kakosea huyo..

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri….

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Serikali haijaonewa huruma hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, mimi nilikuwa nakusikiliza, lakini na Waheshimiwa Wajumbe wengine nao wamewasha *microphones* wanasema. Kwa hiyo, nilikawa nashindwa nifanye maamuzi gani. Kwa maana hiyo, nilikuwa nakusikiliza umesimama nimekuruhusu kuhusu utaratibu sikusikia umesema hivyo na umesema kwa Kanuni ya 68 nimekusikia sasa subiri nitoe mimi maamuzi.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ndio Mhe. Mwenyekiti ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ndio maana nikakuuliza kwa Kanuni ya ngapi, taratibu gani aliovunjwa, ili tumwambie Mjumbe.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 68

Mhe. Mwenyekiti: Naam.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 68 tunamuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu atusomee. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tupo hapa katika mazingira ya kujenga na wala hatuharibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kuna Mjumbe anazungumzia Kanuni ya 59 (8) inayosema ifuatavyo:

"Ni maarufu kwa Mjumbe yoyote:

(a) kutumia lugha ya matusi au kashfa;
(b) kutumia haki yake ya kusema kwa madhumuni ya kutaka kushelewesha shughuli za Baraza;
(c) kuzungumza mjumbe au mtu mwengine kwa nia mbaya au kumshambulia binafsi, isipokuwa kwa kutoa hoja halisi, inayohusu mwenendo makhsusi wa mjumbe huyo;
(d) kujiingiza katika mambo ya kuwasema wajumbe wenzake.

Sasa Mhe. Mjumbe hapa alichukulia lugha za kashfa na matusi kwa serikali ndio anayozungumzia Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum). *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, nimekufahamu na nadhani Mhe. Abdalla Maulid Diwani kwa kitendo ulichosema kuwa serikali imeonewa huruma naomba ufute hiyo kauli, ili tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Nafikiri Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Jecha na ndiye aliyeakhirisha uchaguzi, nafikiri sijatukana wala sijazungumza lugha iliyokuwa siyo na kama anayebishana kama uchaguzi haujafutwa sijui nani atakataa humu ndani. Naomba niendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kauli uliyosema kuwa serikali imeonewa huruma na Mwenyekiti wa Tume. Sasa nadhani hoja ya Mhe. Mjumbe hili neno huruma ndio anahisi kama umelizungumza sivyo, kwa sababu hatukuonewa huruma, labda kulikuwa na makosefu katika uchaguzi, ndio maana Mwenyekiti akafuta matokeo. Kwa hiyo, wewe

ulitamka kuwa Mwenyekiti wa Tume ametuonea huruma. Hivyo, hii neno huruma nahisi uifute hiyo kauli, ili tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelekezo mazuri uliyonipa natamka kwenye Baraza hili kufuta kauli yangu kwamba ile ilikuwa sio nzuri. Naomba kuendelea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Abdalla Maulid Diwani, naomba uendelee kwa kumalizia dakika zako.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana naomba muda unilindie. Mhe. Mwenyekiti nilipozungumza agizo la 4 kuhusu kadhia kamba kutaka pembejeo tulikuwa na Kiwanda cha Chakula cha Kuku Zanzibar. Sasa utekelezaji tunaambiwa wizara kushirikiana na *ZIPA* inaendelea kufanya jitihada kutafuta muekezaji kwa ajili ya kuanzisha viwanda vya uzalishaji pembejeo ya mifugo. Hichi kiwanda kilikufia nini. Naomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie.

Lakini nikenda katika agizo nam 6 wizara iandae mpango wa kuanzisha Kituo cha Utafiti wa Mifugo kufanya tafiti za aina mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, ninavyofahamu Kituo cha Utafiti Zanzibar ...

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba utulivu wenu, mchangiaji anachangia minong'ono naona imekuwa mikubwa, kama ni ile hoja tayari tumeshaitolea uwamuzi. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe tutulie tuendelee na shughuli zetu. Mhe. Mjumbe endelea.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana. Kituo cha Utafiti Zanzibar kipo muda mrefu nchi hii, kipo Kizimbani kama sikosei. Katika utekelezaji wake tunaambiwa serikali tayari imeshaanzisha Taasisi ya Utafiti wa Mifugo kwa lengo la kuendeleza utafiti wa mifugo hapa nchi katika mpango wa taasisi hiyo, mpango wa utekelezaji unaoandaliwa katika robo ya pili.

Kwa mujibu wa bajeti hii robo ya pili imeshapita zamani, tuko 17, 18, robo ya pili ilitakiwa iwe Septemba ya 17 yaani hii Bajeti 16/17, robo ya pili baada ya Julai, Septemba pale 16 ndiyo robo ya pili, kwa sababu robo hizi ni nne katika mwaka miezi mitatu mitatu. Sasa wanaposema kwamba inaanzia kwenye robo hii kwa bajeti gani iliyopitisha hii, wakati Bajeti yake hii ni 2016/17. Mhe. Mwenyekiti, naomba ufafanuzi katika hicho.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tuna mambo mengi ya kusema katika hizi ripoti ambazo tumeletewa humu ndani ya Baraza. Lakini tunashindwa kuzisema nyengine ambapo ndiyo yale unaweza kuja kuambiwa kwamba unakiuka taratibu naomba Mwenyezi Mungu asijujaalie tukafika huko. Lakini kwa kweli tunaletewa ripoti imani yangu kwamba hata hao Mawaziri pengine hawaziangalii kwa umakini mpaka wakatuletea sisi humu ndani tuzichangie ripoti hizi. Kwa kweli acha tuendelee ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Sasa naomba nimwite Mhe. Miraji Khamis Mussa na atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi jioni ya leo kuchangia utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kwanza nianze kuwapongeza viongozi wa Wizara hii, Mawaziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji kwa hatua nzuri ya majibu ya utekelezaji, kila tukipitia tunaona mambo yamekwenda vizuri, baadhi ya sehemu tu ndivyo ambavyo tunaweza tukachangia tukapata ufafanuzi wa ziada. Kwa ujumla mimi naanza kwa kuwapongeza na niipongeze kamati kwa uwasilishaji wao mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye agizo Nam. 1 ukurasa wa 7 ambalo wizara iliagizwa na kamati iwasiliane na wazabuni wanaoleta pembejeo za kilimo. Katika majibu ya utekelezaji wameeleza vizuri lakini kuna maeneo wametaja tani ambazo zinapatikana lakini hasa wakazielekeza katika majibu kuwa watapatiwa wakulima wa umwagiliaji maji. Shida iliyopo eneo lote hili mpaka maelezo ya ziada wametajwa wakulima wa umwagiliaji maji. Tulichokuwa sisi tunapata mashaka tunawakulima wengi zaidi kuliko hawa wa kilimo cha umwagiliaji ambao wanahitaji pembejeo, wanahitaji mbolea hizi, lakini hawakuingizwa katika katiba hii yaani wale wakulima ambao wanategemea mvua.

Kwa kweli, ikawa tunapata mashaka maana ndiyo wananchi nchi pia, sasa katika utekelezaji huu umewalenga kundi moja lakini kundi kubwa halikulengwa hapa. Sasa sijui katika utekelezaji wa namna hii hawa wakulima wa kawaida wanaotegemea mvua tunawapeleka wapi. Sasa kama walikuwemo katika mpango huu kwa nini katika utekelezaji tusiwaainishe. Kwa hiyo, kidogo tu nilikuwa napata mashaka lakini sina tatizo sana waziri atakapokuja pengine kibinaadamu tumesahau lakini atupe maelezo ya ziada ya hawa wenzetu ambao ni kundi kubwa vipi tunawasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 9 agizo nam. 5, wizara ishajihishe wananchi kulima kilimo cha *spices*, kwani kilimo hichi kimekuwa na soko kubwa. Maelezo hapa kwanza tushukuru angalau tu kuwa wizara inashughulikia na inashirikiana na asasi tofauti. Kwa kuwa wizara ina jukumu la moja kwa moja la kuandaa *nursery* zake kwa kuandaa miche lakini pia kuandaa mashamba yake ambayo yatakuwa ni sehemu ya kutoa msaada, yaani nazungumzia mashamba darasa, kutoa msaada kwa wakulima wetu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa hatujaona mpango ule katika ukelezaji lakini tunaona katika maendeo mengine hasa katika kilimo cha migomba tunaona *nursery* zao, kilimo kama cha mikarafuu kunautekelezaji ule tunatoa miche bure, lakini kunako eneo hili la *spices* wizara hatujaona ikajipanga kuelekea huko. Lakini, bado inashirikiana na asasi nashukuru ndiyo hatua ya awali, lakini azma iwe endelevu ya kuonekana tunatia nguvu katika eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atwambie kuna mkakati gani wa kuelekea huko, angalau sasa tunashirikiana na asasi lakini mbele sisi wenyewe kama wizara tuwe tumeweka mpango maalum wa kuwa na *nursery* zetu au mashamba darasa ambayo yanaweza yakatusaidia katika kukuza kilimo hichi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende katika ukurasa wa 11 kunako agizo nam. 3. Wizara iongeze ajira kwa wataalamu wa mifugo, ili tuwe na wataalamu wa kutosha. Kwanza niipongeze wizara kwa hatua hii ya utekelezaji, inaonekana wazi wameshawasiliana na wizara ambazo inasimamia huu utoaji wa vibali vya ajira na wameweka hapa wameomba ajira 68. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo Mhe. Waziri labda nishauri tu. Mara nyingi tunapowaajiri mabwana shamba hawa, tunawaajiri watu ambao makazi yao makubwa inakuwa mjini, sasa inakuwa usumbufu mkubwa wa kuwapatia usafiri au vipando, wakati mwengine inakuwa tunapata mashaka. Lakini na ile dhamira hasa ya serikali ya kutimiza yale mahitaji inakuwa hayapatikani tunatimiza upatikanaji wa ajira lakini malengo hasa hayafikiwi. Kwa kweli, sitaki tubague lakini serikali ijipange kidogo katika kuona ile dhamira kubwa ya kuwatafuta wataalamu hawa basi angalau watoke katika maeneo ambayo tunawapeleka ya vijijini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende ukurasa wa 14 katika Agizo la 11, ambalo linasema Wizara ihakikishe upatikanaji wa hatimiliki katika shamba hilo. Shamba hili ni Shamba la Pangini na katika utekelezaji hili shamba lina miaka 60 ambalo limeshapimwa na ramani zimeshatolewa lakini kuna tatizo la upatikanaji wa hati. Sasa napata mashaka kidogo kwa sababu Wizara mbili hizi, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Ardhi kunaukaribu mkubwa sana, kwa sababu hata kuna mashamba mengine mnapoyajadili ya mikarafuu na mmeshaanza kuyatambua na kuyapima, kwa nini ndani ya miaka 60 mpaka leo hatujafika pahala tukaivumbua hii hati.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo Mhe. Waziri mimi sina mashaka lakini wasi wasi upo. Kabla ya hili shamba kuanza kumegwa hebu tuone utekelezaji au upatikanaji wa hii hati na kuliendeleza hili shamba upatikane. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anisaidia hapa mkwamo hasa katika upatikanaji wa hii hati ni nini ndani ya hiyo miaka 60, angalau wananchi na wao wafaidike na taarifa hizi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende ukurasa wa 15 katika agizo nam. 2, linalosema kuwe na usimamizi na utaratibu wa uchimbaji wa maliasili zisizorejesheka. Kwa kweli, niliposoma hapa pia napo naipongeza wizara. Mhe. Mwenyekiti, naomba katika kipindi kirefu hizi maliasili sizorejesheka tunazo, lakini tunaona hapa wizara yenyewe imekiri kuwa inataka kutayarisha mpango mkakati kwa muda mrefu au muda wote ambao tunaishi katika utaratibu wa kuwa na maliasili zisizorejesheka. Sasa hivi kuna taarifa hapa kuwa wizara ndiyo kwanza inataka kuanza kuandaa mpango wa mkakati wa matumizi endelevu ya maliasili zisizorejesheka hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hivi mpaka leo kuwa hatuna mpango mkakati katika kufanikisha eneo hili la kulinda mali asili zetu, hapa nataka mashaka sana. Najua

unaweza ukakosa kutayarisha mpango mkakati lakini ukawa na mpango kazi lakini hautoshi lazima mpango mkakati uwepo. Sasa kuna changamoto zipi mpaka leo zinapelekea kuwa tumekosa kuwa na mpango mkakati katika eneo hili muhimu sana hapa nchini. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende sasa katika eneo la agizo nam. 4 katika ukurasa wa 17 ambalo wizara itoe taarifa maalum mbele ya Baraza hili, kuhusu hali halisi ya uchimbaji wa mchanga ili Wajumbe wa Baraza hili pamoja na wananchi waelewe dhamira ya serikali juu ya matumizi ya rasilimali ya mchanga. Nikushukuru sana Mhe. Waziri maelezo yako yametosheleza lakini kuna faida tu kwa wananchi wetu ili tuweze kuipata.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya utekelezaji wizara yatari imetoa taarifa serikalini kwa wananchi kuhusu hali ya upatikanaji wa mchanga. Lakini wizara iko tayari katika maelezo yanayofuata, kuwasilisha taarifa maalum kuhusu hali ya uchimbaji wa mchanga Zanzibar katika Baraza hili. Sasa mpaka leo hatujaona katika ile ratiba ya ndani ya Baraza tumeona taarifa za *ZAWA* zinakuja lakini taarifa hii haipo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuulize Mhe. Waziri katika eneo hili kunachangamoto gani hivi ameshawahi kuwasiliana na kiongozi wa Baraza, ili kuleta taarifa ya ikakwama au mpaka sasa hivi hajawa na dhamira ya kuomba hicho kibali cha kuingiza taarifa hii ndani ya Baraza hili. Nafikiri ni vyema atupe taarifa tufaidike Wajumbe wa Baraza, ili tuone kama hatukupata ndani ya Baraza hili tutapata lini au kibali hichi amekwama wapi ili na sisi tufaidike katika kupata taarifa muhimu za eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuwapongeza viongozi wa wizara wamefanya kazi nzuri, niipongeze kamati maagizo yao yamekwenda vizuri, naomba nishukuru sana kwa kupata nafasi jioni ya leo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, akifuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Suleiman Makame Ali wa Ziwani ajiandae.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: *Bismillahi Rahmani Rahim*. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipatia nafasi na nitajitahidi kuchangia Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kuwa sina uzoefu nayo sana mambo haya lakini nitajaribu kuchangia ninavyofahamu kwa mujibu wa ripoti hii ilivyokuja.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na suala moja ambalo lipo katika page Nam. 5 ningetaka kujua kuhamasisha wafugaji wa samaki chaza, kaa na kamba ili kuendeleza uzalishaji wa mazao haya, pia juhudi zitachukuliwa katika kutafuta masoko kwa mazao ya baharini.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ningependa kuja kujua ufugaji wa samaki na vitu vyenginevyo ambavyo vimetajwa hapa kazi yangu havina athari au labda ladha yake

inakuwa tofauti au vipi katika vitu kama hivi, samaki, chaza, mlivyotaja na vitu vyengine vyo hawa wa kufuga. Tofauti yake haileti athari yoyote katika masuala ya afya au vipi.

Mhe. Mwenyekiti, tukienda kwenye ukurasa nam. 6 vile vile kusomesha wanafunzi 104 waliopo *diploma* 47 na cheti 57 na kuchukua wanafunzi wapya 100, *diploma* 50 na cheti 50 kupitia Chuo cha Kilimo cha Kizimbani. Mhe. Mwenyekiti, ningependa kutoa ushauri kwa sababu tumeona wanaopewa elimu hapa ni wanaotoka kwenye Chuo cha Kizimbani na sehemu nyenginezo ambazo wanazoona wao wanafaa kupewa elimu. Lakini je, katika vile vikundi ambavyo vinahusisha wakulima, ikiwa wafugaji na wengineo, wamejipanga vipi kuweza kuwatoa watu hata kama hawana elimu ya shule kubwa kwenda kuwapa elimu kama hizi wanazokwenda kuwapa watu ambao wamewataja hapa. Sasa kama wamefanya hivyo ni wangapi tayari wameshawapa elimu hiyo au kuna utaratibu gani ambao wameuwandaa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ukurasa huo huo nam. 6, kushajihisha na kuwaunganisha wakulima, wafugaji na wavuvi katika masoko ya ndani na nje ya nchi kwa kuwaunganisha pamoja na kuwapatia mikopo kutoka taasisi za kifedha. Hapa Mhe. Mwenyekiti, hadi hivi leo kama masoko tumeegemea zaidi kwenye masoko ya Unguja na Tanzania Bara. Lakini vipi wamejipanga zaidi kuweza kuwatangazia hawa wakulima, wafugaji, wavuvi, vitu vyao ambavyo wanavitengeneza katika ku-*create* kutoka kwenye akili zao kama masuala ya mbolea, wale wanaotengeneza pilipili nmeona kama karafuu na vitu vyenginevyo. Kwa hiyo, vipi wamejipanga kuhusu masoko ya nje zaidi ili kuitangaza Zanzibar nje kuliko soko la ndani ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kabla ya yote ningempongeza sana leo Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud kwa kumsaidia Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum) kwenye Kanuni za Baraza la Wawakilishi na kuweza kufanikisha, nampa pongezi sana.

Mhe. Mwenyekiti, suala la uvuvi ambalo nitalizungumzia mwanzo lenye *page* 30, 31, na 32 ambalo limezungumzia masuala ya uvuvi kwa ujumla. Wizara iandae utaratibu maalum wa usimamizi za madiko, kwani baadhi ….. samahani ukurasa Nam.7 ugawaji wa kilimo wa dawa.

Mhe. Mwenyekiti, wizara iwasiliane na wazabuni wanaoleta pembejeo za kilimo, ili pembejeo hizo ziwafikie wakulima kwa wakati. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja anisaidie hivi vitu vyote vilivyoletwa mbolea na vitu vyenginevyo ujagawaji wenu mmejikita kwenye njia gani, kila wilaya wanagawa vipi au wanagawa kila jimbo ama wanagawa kwa kikundi ambacho kinalima au vipi. Hivyo, napenda kujua ugawaji wenu uko vipi na wepi hasa ambao wamenufaika zaidi na ugawaji wa dawa hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea naomba nende kwenye *page* nam. 9 ambayo inazungumzia masuala ya viwanda, kwenye wizara itoe ushirikiano wa dhati kwa wawekezaji wote wanaowekeza au wanaokusudia kuekeza kwenye sekta zinazotumiwa na Wizara ya Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri hapa wanatafutwa wawekezaji wa vitu tofauti kuhusiana na wizara yake kwa kushirikiana na *ZIPA*, tukiangalia kwenye *page* nam. 10 naona *ZIPA* ipo hapa kuna sehemu ambayo wametaka washirikiane kwa ajili ya kutafuta *investors*. Je, tayari wanapokuja kupata *investors* wameshajitayarisha na *feasibility study* zetu ambazo zitaonesha kitu gani wanachotaka mtu a- *invest* labda kwenye masuala ya mifugo, afunguwe kiwanda cha nyama, au kwenye masuala ya uvuvi kifunguliwe kiwanda cha samaki, wameshajitayarisha na *plan* zao mtu anapokuja tayari wanamuonesha au wanataka mtu aje na maoni yake sio maoni yao. Ningependa kujua njia hizo ambazo wanazozitumia.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile *page* ya 10 inazungumzia serikali kupitia wizara iandae utaratibu maalum wa kudhibiti uingizaji wa bidhaa za mifugo kutoka nje ya nchi hasa zile ambazo zinazalishwa kwa wingi ndani na mambo ya dawa. Mhe. Mwenyekiti, naomba kujua Mhe. Waziri uletaji wa hizi dawa zinazokuja Zanzibar ni ngapi ambazo wameshawahi kukamata kwamba hazina kiwango au labda mtu kadanganya au kuna kampuni imeleta vitu ambavyo havipo kwenye kiwango zikaweza kuathiri wale watumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine nitakwenda kwenye *page* nam. 13 ambalo linahusiana na wakulima na wafugaji kwa mambo ya kisasa wanavyotaka Wizara. Wizara indelee kutafuta wawekezaji wa ajili ya kuanzisha ….*Sorry page* nam 13.

Katika suala la ukuwaji wa sekta ya mifugo tayari yameanza malalamiko ya maeneo ya ardhi kwa wakulima na wafugaji, ili kunusuru migogoro ambayo inaweza kujitokeza hapo baadaye serikali ianzishe mpango maalum wa kutenga maeneo ya mifugo waweze kutumia eneo dogo la ardhi kwa kufuga ng'ombe wachache wa kisasa na wenye tija na kuacha ufugaji wa kizamani.

Kwa kweli, suala hili Mhe. Waziri liko *very open*. Kwa hiyo, naamini wizara itapokuwa tayari kuwasaidia wananchi kuwapa elimu kuwasaidia na kuwafundisha, basi nafikiri *idea* hii hawatoikataa, ambayo wameipendekeza kutaka kuwapelekea kwao kufata ufugaji wa kisasa hata kilimo cha kisaa watapojiandaa na wao wananchi watakuwa wako tayari lakini wakisema wawaachie wananchi peke yao suala hili hawataliweza, kwasababu hivi vitu vinataka *capital* vinataka elimu vinataka nguvu. Sasa pindipo wizara itakapokuwa itapokuwa ishajidhatiti kuwasaidi wananchi kwenye suala hili, basi naamini wananchi waatakuwa tayari na hii *idea* sio mbaya ni nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nende kwenye idara namba 14 kuna Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka hapa imesema wizara kwa kushirikiana na Taasisi husika iendelee kukomesha matumizi ya misumeno ya moto. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri au kama nafikiri inawezekana wanalitumia tayari. Kwa kweli, suala la ukataji wa miti na mambo mengineyo Zanzibar hasa minazi, ambayo tulikuwa tunaringia sasa hivi imepungua hata madafu fedha nyingi sana, nazi hainunuliki na hasa nchi kama hii kununua nazi shilingi 1500/= ni pesa nyingi sana au dafu shilingi 1000/=.

Lakini ninachotaka kusema andaeni mfuko maalum kwa kuweza kuwapa watu ambao watatoa *information* kwa wale wanaokata minazi, wanaokata miti ambayo hawataki ikatwe waweze kuwapa *bonus* watoe *information* na yule watakayemkamata atapigwa *penalty* pesa zao zitakuwa zimerudi na watamuweka ndani kukomesha suala hili. Mhe. Mwenyekiti, hili ni wazo ambao najaribu kulitoa kama linakuwa halipo basi naomba walizingatie.

Nitaendelea kwenye *page* namba 17 Mhe. Mwenyekiti, *page* namba 17 inazungumzia suala la mchanga. Wizara itoe taarifa maalum mbele ya Baraza hili kuhusu hali halisi ya uchimbaji mchanga, ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili pamoja na wananchi waelewe dhamira ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna anayetaka kubishana na wala anayetaka kwenda kinyume na serikali lakini tuangalie athari ni ipi. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli serikali imezuia suala la mchanga Mhe. Waziri kutoka kule kwa mwanzo kwenda sasa hivi katika njia ambayo ya ku-*save* na kuweza ku *protect* labda masuala mengine ambayo wanajua wao kuweza mchangza kuwepo labda mambo mengineyo.

Lakini tatizo tunaloliongelea sisi sio kama hatutaki kuzuiliwe au hatutaki serikali ifanye maamuzi yake, tatizo mchango umekuwa pesa nyingi mara nne gari ambalo tumekuwa shilingi 180,000/= la tani kumi la mchanga sasa hivi tunalinunua kwa laki 750,000/= hichi ndicho kitu ambacho tunapigania nacho. Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali kwamba iendelee kuweka vikwazo inavyovitaka kwenye masuala yale ili kudhibiti haya masuala lakini mchanga uweko bei ya mwanzo, kwa nini mchanga upande wakati mchanga wakati mchanga utakapopanda tofali limepanda bei, saruji imepanda bei hapa hapa utakuja kukuta tunaumizi wananchi wa chini, waliokuwepo juu hawataadhirika sana kwa sababu uwezo wanao lakini watoathirika ni masikini wa chini ambao kipato chao kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, lengo letu sisi kwamba Mhe. Waziri afanye anavyotaka anavyoona yeye anaweze kuona nchi kuiweka katika hali nzuri hakuna tatizo, lakini suala la mchanga liwe bei kama ya mwanzo au hata kama imepanda kutoka laki 180,000/= iwe angalau basi iwe laki 250,000/=. Lakini sio tunvyonunua sasa hivi mchanga shilingi 750,000/= kutoka shilingi 180,000/=.

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye *green policy* mambo ya masuala ya kuotesha miti page namba 16. Mhe. Mwenyekiti, naiomba wizara kwa sababu hapa wameweka kila mwezi wa Juni wanasema ni siku ya kupanda miti lakini. Lakini nashauri suala la kupanda miti katika nchi au katika sehemu muhimu lisiwe la kila Juni la mwaka kila mwezi wa Juni, isipokuwa liwe la kila siku angalau kwa mwezi watafuta siku tatu kuweza kuotesha miti sehemu tofauti tusingejee Juni kwa ajili ya kuotesha miti.

Kwa kweli nchi nyingi ambazo ndogo mkama hizi tukienda zina *green* kubwa miti mingi kila *design* ya rangi na kivuli na mambo mengineyo. Sasa naomba hili suala kwamba kila

Juni liondoke naiwe mazoea kwamba tuoteshe miti kila tunapopata muda katika mwezi angalau mara tatu kwa siku.

Mhe. Mwenyekiti, niende *page* nam. 19 ambayo inazungumzia Msitu wa Jozani. Msitu huu unao magao wake kwa ajili ya kuendesha shughuli za msitu na itumike fedha hizo kama inavyoeleza. Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Waziri eneo la Jozani kwa sababu ni eneo la utalii na sehemu nyingi duniani tunaenda tunakuta kama *Ngorongoro National Park* na sehemu nyenginezo Tanzania kuna mahoteli je mtu atakayekuwa tayari ku *invest* hoteli ikiwa ndogo ikiwa kubwza ndani ya msitu wa Jozani yuko tayari kama wizara kushirikiana mtu ku *invest* ndani ya Jozani *Forest* ama kwenu kuna vikazo.

Kwa mfano, tukichukulia Tanzania bara kwenye *parks* kubwa kubwa za wanyama *Wild Park* hizo *National Reserve* hizo wana mahoteli makubwa makubwa na hoteli ndogo sasa ningependa kujua kwa upande wa Jozani muko tayari mtu kuweza ku *invest* hotel yoyote kwza mujibu wa uwezo ambao atataka kufanya.

Lakini vile vile ningeenda kwenye page namba 20. Wizara iandae mpango wa kupatika usafiri wa uhakikia kwa ajili ya usimamizi wa misitu. Mhe. Mwenyekiti, hapa wizarza ikajibu inatumia milioni 180,000,000/= kununua gari tatu kwa ajili ya Msitu wa Jozani. Mhe. Mwenyekiti, naomba kujua Mhe. Waziri hivi haiwezekani kutumika milioni 70,000,000/= kwa gari tatu *instead of* milioni 180,000,000/= kwa sababu milioni 180,000,000 ni fedha nyingi sana kwa kuzipitisha misituni kwenye ukaguzi, zipo gari ambazo *used Nissan* yake *Hilux* ya juu milioni 30,000,000/= mazuri tuu ambayo yametumika.

Kwa kweli, hapa tunakuta milioni 180,000,000 wakati *income* yenyewe ya Jozani *Forest* sio kubwa ya hivyo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri fedha hizi zingepunguzwa zingetafuta gari ambazo zitakuwa kidogo bei yake ya chini hata wanunue tano sita lakini kuliko gari tatu kwa milioni180,000,000 kwa sababu tu ya doria ya Jozani au kuingia kwenye vichochoro vya Jozani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri wangu wa mwisho kwa masuala ambayo hili suala la *page* namba 25 kuna watendaji waliondoka na vyombo vya moto. Lakini wizara ikaeleza kwamba virejeshwe na inaeleza kwamba kuna vyombo karibu 15 vimesharejeshwa na watendaji ambavyo waliondoka navyo pikipiki 15 na magari 13. Kwa kweli, nafikiri Mhe. Waziri haya mambo hayana haja kusubiri *order* kutoka kwenye kamati hii iweko kwamba kitu kiwepo *official* kuwepo *open* kabisa kwamba mtendaji hana haki kuondoka na kitu cha wizara au kitu cha serikali.

Suala hili ni zuri wamefanya. Lakini mengine kwamba nitakachoomba kwamba wizara inahusisha zaidi watu wanyonge, wavuvi tungeomba watafutiwe maboti mazuri waweze kupewa kwa kila kikundi, kama ikiwa Zanzibar kuna vikundi wakaanza basi kikundi kimoja kikapewa boti moja kuweza kwenda kuvua *deep sea*....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Nadiri naomba umalizie muda wako umekwisha.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hiyo, wakaweza kwenda kuvua *deep sea* mukawapatia meli za kisasa, na vile vile wale watu ambao wanaotaka kuwakamata basi huko *off shore* ndio wanaofanya mambo ya wizi wa samaki, na wale ambao *local* wanaovua kwa kiboti naomba sana waachiliwe kwa sababu uvuvi wenyewe uko taabani vitendea kazi hawana, washughulike zaidi na watu ambao wanavua *off shore* na meli kubwa.

Vile vile, wakulima wangu wa Jimbo la Chaani asiwasahau Mhe. Waziri naomba twende pamoja tuhudhurie tukutane nao tuwasikilize shida zao, kwasababu washaniomba sana Mhe. Waziri wa Kilimo aje na mimi leo nakupa tarifa hii kwamba ukipata muda twende zetu pamoja tukamalize mambo.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kama nilivyosema wizara hii sina udhoefu nao ndio maana nikajaribu kupiga piga kidogo na nashukuru sana na ripoti hii naikubali asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahante sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Mwakilishi wa Chaani kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma akifuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nikushukuru kunipa nafasi hii nikaweza kuzungumza machache katika kumsaidia Mwenyekiti wetu wa Kamati kutia nyama Ripoti ya Maagizo waliyotowa kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kama walivyotangulia wenzangu kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake na kama alivyosema Mhe. Ali Suleiman Ali kweli Mhe. Waziri wetu wa Kilimo ni mwalimu na anajua kulea namini Mhe. Waziri siku za mwanzo kidogo naibu wetu alipokuwa anajibu maswali kidogo yalikuwa yanamkanga. Lakini kwa kuwa amekaa na mwalimu sasa hivi tunashukuru tunapata majibu kutoka kwa Naibu Waziri majibu ambayo yanaturidhisha tunapongeza sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja nataka ninze katika ukurasa wa tisa katika kifungu cha 5 Ripoti inayosema Wizara ishajihishe wananchi kulima cha *spices,* kwani kilimo hiki kimekuwa na soko kubwa ulimwenguni.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mhe. Waziri namna gani wizara inavyoshirikana na Asasi ambazo Zisizo za Kiserikali yaani *NGO's* katika kuhamasisha uzalishaji wa hivi *spices*. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Kwa kweli, nilihudhuria Maonesho ya Sabasaba pale viwanja vya Dar-es-Salaam. Kimsingi ukiingia katika lile banda la Zanzibar na mimi kwa bahati nzuri miaka yote huwa ninakwenda kuna *improvement* kidogo imeanza kujitokeza hasa katika vile

vifunganishi, kwa kweli wanajitahidi sana katika kuwasaidia. Lakini kuna kilio cha wale wajasiriamali wetu na moja katika kilio chao wasema kwamba Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inawapa mashirikiano pamoja na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kuwapeleka kwenye yale maonesho.

Lakini kuna changamoto moja kubwa ambayo inayowakwanza hasa katika kuzitengenezea ubora, yaani kuziweka katika ile *standard* ambayo nafikiri hapa inaitwa *ZBS*. Sasa kitu ambacho wanalalamika wale wanasema ukiangalia wajasiriamali wetu wanaoshughulika na hizi *spices* kwanza ni wadogo, yaani mitaji yao midogo. Sasa hizi *spices* zao wanapokwenda kuzipeleka kwenye ukaguzi, yaani kila *spice* moja wanalipishwa kile kima cha fedha nimekisahau lakini wanalipishwa kidogo fedha nyingi.

Kwa hivyo, wanasema kwamba sisi biashara zetu wanauza *spices* kama tano. Kutokana na hali hiyo, kitu ambacho wanakiomba hawa kwamba zile *spices* zao wanapokwenda kule *ZBS* basi alau watengenezewe kama *package* ya pamoja, ili waweze kupata unafuu wa ile ada. Kwa kweli, wanasema ada inapokuwa kubwa ndio wakati mwengine wanakimbia kwenda kule *ZBS* na matokezeo yake wanakwenda kule kwenye maonesho *super market* zinakuja zinataka bidhaa, lakini inapofika pahala hebu nioneshe ile *ZBS* yako utakuta wengine wanao *ZBS* nyengine hawana sasa hii inatokana na mitaji yao midogo.

Sasa Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi pamoja na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Kwa kweli, miongoni mwa mawaziri ambao nawapongeza sana kwa jitihada za kufanya utafiti na kutafuta namna gani yakuweza kuinua kiwango cha bidhaa zetu wanajitahidi sana. Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu wangejaribu kutafuta *funds*, pengine kupitia kwa mabenki mbali mbali, na sasa hivi tuna Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa wenzetu Bara kule, nafikiri na hapa mjaribu ku *invite*, ili kuwasaidia hawa hasa katika hizi gharama za kupimisha zile bidhaa zao ili ziwe na kiwango vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano kuna mmoja yeye aliniambia tayari amepata soko kubwa sana kwenye *super market*, na kwa kweli hata ule uwezo wake wa ku- *supply* katika *super market* unakuwa ni mdogo, lakini sasa wengine hawa wachanga wachanga wanashindwa katika hiyo. Nadhani Mhe. Waziri naomba katika jitihada zake za kuhangaika huku na kule, basi wakae nao hawa, ili kuangalia hii changamoto ya kuweza kuwasaidia hasa hizi gharama.

Lakini jenine Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 12 hii *paragraph* ya 5. Kamati imesema serikali ianzishe mpango maalum wa kuhamasisha wananchi kula bidhaa za mifugo kama vile mayai, maziwa ikiwemo Siku Maalum ya Kunywa Maziwa. Mhe. Mwenyekiti, jawabu ya Mhe. Waziri imeeleza hapa kwamba kuna Siku Maalum ambayo imewekwa ya Mwezi Juni, lakini vile vile kupitia Idara ya Uhakika wa chakula na Lishe Program Maalum ya Lishe Maskulini inaendelea kutoa taaluma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli naomba Mhe. Waziri anajitahidi sana katika kuhamasisha kilimo cha uvuvi yaani ufugaji wa samaki, lakini naomba ajikite zaidi katika kuwahudumia au kuwasimamia hawa wafugaji hasa katika suala zima la maziwa.

Kimsingi kipindi cha nyuma tulikuwa tunapata yale maziwa zamani tunaita maziwa ya vibandani, lakini sasa hivi soko la maziwa kidogo wananchi wamekuwa wakiuza tu kienyeji enyeji kwenye chupa hivi kunakuwa hakuna hasa ile *package* nzuri ya maziwa ambayo wakulima wetu au wafugaji wetu wanaelekezwa.

Nadhani Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tunae muwekezaji wa Kiwanda cha Maziwa ndugu yetu Bakhresa tunamshukuru, lakini bado *support* yake kwa wakulima hawa wa maziwa haijakuwa nzuri na kiwanda kile sasa hivi tunaambiwa kinaagiza maziwa ya unga, ili kuweza kutengeneza maziwa ya kunywa. Kwa hivyo, maziwa ya unga sitegemei kama ubora wake yatakuwa sawa sawa na maziwa ya mifugo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti naomba Mhe. Waziri akae na muwekezaji yule aangalie ni namna gani anaweza akasaidia kununua maziwa kutoka kwa hawa wafugaji, au wafugaji hawa waweze kusaidiwa katika kutengeneza *package* nzuri ya kuhifadhi yale maziwa, ili yaweze kutumika katika kiwango ambacho kilicho bora. Kwa kwali, hili naliomba Mhe. Mwenyekiti, na wenzetu hawa wakulima au wafugaji wakiweza kusadiwa katika njia hiyo naamini wataweza kupata moyo wa ufugaji, ili kuweza kuendeleza maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ukurasa huu huu wa 12 kifungu No. 7 kinasema kutokana na agizo linasema kutokana na ongezeko kubwa la ukuwaji wa sekta ya kilimo sambamba na ukuwaji wa sekta ya mifugo tayari umeanza malalamiko katika maeneo ya ardhi ya wakulima na wafugaji, ili kunusuru migogoro ambayo inaweza kujitokeza hapo baadaye serikali ianzishe mpango maalum wa kutenga maeneo ya mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, hili nashukuru kwamba serikali wamejibu jawabu nzuri. Lakini hapa kitu ambacho nataka niseme zaidi katika kuyalinda hasa maeneo ya kilimo. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa hivi kama tunavyojua *population* Zanzibar inazidi kuongezeka na hili neno nitaendelea tena kulisema kwamba wakati tayari tuna dalili za uwekezaji wa sekta ya mafuta na gesi Zanzibar, basi tutegemee *immigration* itakuwa kubwa watu wataingia kwa wingi nchini.

Sambamba na hilo tena kwa bahati hapa Zanzibar bado Shirika letu la Nyumba halijaweza kuwa na uwekezaji mkubwa katika kujenga nyumba, ambazo zitakazoweza kuja ku-*afford* wale wahamiaji kuja kukaa katika nyumba zile. Kutokana na watu wetu pengine na unyonge wao na umasikini wao mtu akitokezea na pesa yake ndogo basi mara nyingi wako tayari kuuza ardhi zao kwa ajili ya kujenga nyumba za makazi. Kwa kweli hali hii, itapelekea sana haya maeneo ya kilimo ambayo yaliyobakia yataendelea kuvamiwa kwa ajili ya kujengwa nyumba matokezeo yake wakulima wetu wataanza kupoteza maeneo ya kulima.

Mhe. Mwenyekiti, hili naliomba kupitia Shirika la Nyumba ambayo Kamati yangu inasimamia inajitahidi, lakini vile vile Mhe. Waziri, waweze kuyatambua Wizara ya Kilimo hawezi kuyatambua maeneo ya kilimo na yalindwe maalum, ili kuhakikisha kwamba yasivamiwe katika ujenzi wa makazi ya watu.

Mhe. Mwenyekiti, suala No 14 wizara kushirikiana na taasisi ukurasa wa 14 Idara ya Misitu, Maliasili Zisizorejesheka, agizo linasema wizara kushirikiana na taasisi husika iendelee kukomesha misumeno ya moto.

Mhe. Mwenyekiti, tumeona jitihada ya wizara katika suala zima la kuzuia misumeno hii ya moto na katika jawabu la Mhe. Waziri humu ameeleza zaidi ya misumeno 55, Unguja 31, na Pemba 24 imeshakamatwa. Kwa hiyo, tunawapongeza sana serikali kwa jitihada hii kwa sababu ni kweli kwamba hawa watumiaji wa misumeno ya moto wakati mwengine wanaitumia vibaya, wanakata miti ya watu miembe michanga na miti mingine ambayo inasababisha kuwavunja moyo wakulima lakini bado jitihada hizi ziongezeke.

Nadhani tungeliwashirikisha zaidi masheha kwa sababu masheha wao ndio wanaokaa katika maeneo mbali mbali na hii misumeno ya moto inatumika katika shehia zao. Kwa mfano, tukiangalia kama sasa hivi zao la minazi, yaani minazi mingi kwa kweli inakatwa, kuna viwanda vingi vya mbao za minazi na kwa kweli minazi yetu inakuwa inaangamia hasa kupitia hii misumeno ya moto. Lakini tunaipongeza jitihada ya wizara, lakini vile vile wasipunguze kasi. Kwa hiyo, misumeno hii inaweza ikaangamiza miti yetu kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 16 katika eneo hili la Wizara ya Kilimo, kifungu Nam.3 agizo la kamati linasema serikali ianzishe sera maalum ya *Green Policy*, ili kuweza kupanda miti kwa wingi katika nchi yetu. Tumeona hapa Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi amesema kwamba kuna Siku Maalum ya Upandaji wa Miti Kitaifa katika mwezi wa Machi ya kila mwaka. Mwenzangu amezungumza hapa Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, lakini na mimi vile vile nataka kuongezea, hili zoezi Mhe. Mwenyekiti nadhani kwa kila mwaka mara moja kwa kweli bado kasi inakuwa ni ndogo, na watu inafika pahala wanasahau. Unajua hewe hewe Waswahili wanasema inasaidia kumfanya mtu aharakishe mwendo.

Nitachukulia mfano mdogo Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru Baraza letu kupitia ziara mbali mbali za kutupeleka kwenye kujifunza kwa vitendo, Baraza limeweza mimi mwenyewe limenisafirisha nimekwenda China. Wakati ule nilipokwenda China niligundua kwamba ndani ya barabara za ndani ya miji, yaani unakuta miti barabara zote zimezungukwa na miti, yaani ile miti inafuata zile barabara. Sasa sisi tukajaribu kuwauliza wale wenyeji wetu, hii miti mbona iko mingi mpaka mjini. Kwa kweli, wao wakasema kwamba kuna mwaka kulikuwa kumefanyika mkutano mkubwa kule nchini China, ambao ni mkutano wa Siku ya Mazingira Duniani, lakini vile vile mkutano unazungumzia masuala ya kuondoa hewa chafu, pamoja na suala la kuhifadhi ile wanaita tabianchi.

Kwa hiyo, kwa kuwa siku ile iliadhimishwa nchini China, kwa hiyo kupitia azimio katika mkutano ule wenyewe wenyeji nchi ya China wakasema kuanzia leo tutahakikisha katika kutekeleza huu mkutano au azimio la mkutano huu, tutahakikisha China nzima inapandwa miti. Kwa maana hiyo, utakuta kule wenzetu hawasubiri siku moja kwa mwaka wanashirikiana na Mabaraza ya Miji kuhakikisha kwamba wanapanda miti

maeneo ya mbali, yaani kama kwenye *nursery* halafu miti ile inang'olewa mizima mizima inakuja kupandwa mjini, kama walivyofanya hapa Forodhani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa imesaidia sana ile China kuifanya kwamba iko *green*, na hili nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri najua hakujipanga kwa bajeti hii, lakini tunashauri katika bajeti inayokuja kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, basi tuhakikishe kwamba tunaziboresha barabara zetu lakini pia tunapanda miti kila mara, ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa *green*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 17, kifungu kidogo cha 4 wenzangu wamezungumzia hapa suala hili la Kamati ilishauri kwamba wizara itoe taarifa kuhusu hali ya uchimbaji wa mchanga. Kwa kweli, hili suala ni kweli ni muhimu Mhe. Waziri nafikiri iko haja hii taarifa iletwe, ili tuipate kuichangia, kwa sababu wananchi wanalalamika upande wao lakini na wale wadau ambao na- *declare interest* Mhe. Mwenyekiti na wao vile vile wanalalamika upande wao. Sambamba na hilo, kama hivi karibuni kuna zoezi ambalo linafanyika ambalo sisi tulilishauri kwenye vikao mbali mbali vya wizara kwamba magari haya lazima yajuulikane hasa *capacity* yake ni tani ngapi.

Mhe. Mwenyekiti, hili zoezi Mhe. Waziri limeanza lakini naomba alisimamie kwa karibu, kwa sababu kama nilivyosema mwanzo mimi na-*declare interest* kwa sababu ni mdau katika sekta hiyo. Kuna wawekezaji hapa tulikuwa tunawasafirishia mchanga katika maeneo yao, hao ndugu zetu wa China wakapima gari, gari ni tani kumi na moja na nusu lakini sasa hivi gari imepigwa na Wizara ya Kilimo na Misitu inaambiwa ni tani kumi na nusu, sasa *which is which.* Mhe. Mwenyekiti, nadhani Mhe. Waziri hili suala ajaribu kulisimamia kwa karibu kwa sababu tusiangalie tu katika kupata mapato, kwa sababu mfano gari hiyo ambayo ilikuwa inasomeka tani kumi na nusu, ilikuwa inalipiwa shilingi elfu 78,100/= sasa hivi imepimwa tena inasomeka tani kumi na nne na nusu inalipwa shilingi 94,500=.

Sasa watendaji wetu wakichukulia zaidi kuangalia kwenye kupata mapato matokeo yake ile *cost* ina-*reflect* kwenda kwa wananchi vile vile. Tukiangalia magari haya yana gharama kubwa sana *running cost* zake ni kubwa. Kwa hiyo, unaweza ukakuta kwamba wananchi wanalalamika lakini vile vile ukiangalia na *running cost* vile vile zinaenda sambamba na hizo gharama. Sasa mimi nadhani wizara ingeliangalia namna gani ya kuweza kupunguza baadhi ya *charge* ili hii gharama isiweze kuongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia tunakushukuru sana Mhe. Waziri uko karibu sana na hili suala tunashukuru mara zote unapopata ushauri unauchukulia hatua haraka haraka, kwa hiyo tunakushukuru vile vile kwa mashirikiano yako.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa nilikuwa naangalia ukurasa wa 21, kifungu cha 12 kinachosema wizara iendelee kutumia wataalamu wake ili kubudi vivutio vyengine vya watalii na wananchi wanaokwenda kutembelea kwenye misitu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, naendelea tena kulishukuru Baraza la Wawakilishi kuna mkutano mmoja nilihudhuria kule Geneva na ile siku ambayo tuliyopata mapumziko tulipata nafasi ya kutoka kidogo

tukenda sehemu za mapumziko beach kule kama ilivyo Forodhani. Wenzetu kule wamejaribu kuweka yale mabango ambayo yana-*display* usiku zinawaka taa ambazo ukienda unaweza kusoma. Wameweka *species* kila *species* ya ndege aliyekuweko katika nchi ile kwa hivyo wanaandika…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza naomba umalizie.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya ndio namalizia.

Mhe. Mwenyekiti: Muda wako umekwisha malizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Haya ndio namalizia Mhe. Mwenyekiti, sasa ndio najaribu kumuhamasisha Mhe. Waziri tuandae ziara mimi na yeye kwenda Geneva ili nikamuoneshe vile vivutio ambavyo vinaweza kusaidia utalii wetu. Mhe. Mwenyekiti, na kwa sababu mfano ambao nautoa tena wenzetu wa China wanaweza wakakuelezeni kwamba kuna jiwe liko hivi, liko hivi lakini matokezeo yake ukienda ukisema ah jiwe lenyewe hili kumbe Zanzibar tuna mawe zaidi ya mia moja kama yale lakini tunashindwa kuyatangaza.

Kwa hiyo, nadhani Mhe. Mwenyekiti eneo letu la Forodhani sasa hivi limejengwa vizuri linapendeza tungeliweza ku-*display* maeneo hayo, tukaweka *species* zinazopatikana Zanzibar tukaeleza historia zake ingesaidia wageni wale kwenda kuwapeleka katika vivutio vya utalii bila ya wenyewe kukusudia.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii naunga mkono ripoti hii ya kamati, lakini vile vile utekelezaji wa Mhe. Waziri katika ripoti ya kamati. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, nina wachangiaji kama wanne waliobakia na tukiangalia muda wetu unatuacha mkono, sasa niwaombe wajumbe nitakaowapa nafasi wachangie Mhe. Suleiman Makame Ali umeniomba dakika tano nitakupa dakika tano halafu atafuata na Mhe. Omar Seif Abeid ili tupate tumpe nafasi Mhe. Waziri atoe majumuisho. Lakini kabla ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi nitampa pia nafasi Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud Mohammed na baadaye Mhe. Waziri atatupa ufafanuzi kwa zile hoja zilizotolewa. Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia taarifa hii ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuhusu utekelezaji wa maoni ya kamati.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 15 kamati walisema kwamba kuwe na usimamizi wa utaratibu kuhusu masuala ya misumeno ya moto. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze sana kamati pamoja na wizara kwa kuliona hili na kuhakikisha kwamba wanaidhibiti misumeno ya moto, kwa sababu kusema la ukweli misumeno ya

moto inaathiri sana na inatusababishia ukame na ndio ukaona jua hili linawaka kutokana na kwamba miti haipo kila siku inakatwa.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha kwamba wizara imesema kwamba kuna baadhi ya masheha hawatoi ushirikiano. Sasa naomba kusema hapa kwamba huyu sheha anafanya kazi kwenye Serikali hii ya Mapinduzi, ikiwa kama hawezi kutoa ushirikiano kwenye wizara hii basi huyo hafai aondoke Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ yupo.

Kwa kweli, kama sheha hawezi kutoa ushirikiano na anajua kwamba fulani na fulani ndio wanaodhibiti msumeno wa moto ndani ya shehia yake, lakini hawezi kutoa ushirikiano kwa sababu ni kwamba hawezi kukabiliana na kazi yake, kwani pamoja na majukumu ya kazi na hilo nalo ndilo. Kwa hiyo, sheha huyo itakuwa hafai na Mhe. Waziri nakuomba sana kwamba masheha hawa wote wakibainika basi ni kwamba waondoshwe kwa utaratibu na kisheria kama inavyojuulikana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwenye ukurasa wa 24 kuhusu masuala ya ukodishwaji wa mashamba.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali sana, sana kwa kuliona hili lakini pia nimpongeze huyo aliyepeleka wazo hili kuhakikisha kwamba mashamba yote ya serikali lengo ni kujuulikana ili kudhibitiwa. Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya watu kwa sababu tayari ile adhma ya muasisi wa Mapinduzi Mzee Abeid Amani Karume wengine hawakufahamu, tayari kuna baadhi ya wengine wameshayauza mashamba haya na ndio serikali ikaona kwamba ipo haja ya kuyatambua. Sasa maoni yangu kwa wizara pamoja na kamati na serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba mashamba haya yaliyotambuliwa na kama kuna mengine yawekwe wazi na ya juulikane lakini na kama kutakuwa kuna watu wanayaficha makusudi kama ilivyokusudia wizara wayarudishe kwenye serikali basi wachukuliwe hatua watu hao.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba wizara kwamba ikeshahakikisha basi wale wakulima ambao mashamba haya wanayashughulikia wakati ilikuwa lengo ni kuyajua, warejeshewe wenyewe kwa sababu wao ndio waliokuwa wakiyatunza mashamba yale. Kwa kweli, nina imani wakati ilikuwa kama wao ndio waliokuwa wakiyatunza mashamba yale, basi wakirejeshewa kwa utaratibu uliokuwa mzuri nina imani kwamba hawatuthubutu kufanya tena kitendo hiki ambacho walikuwa wanakifanya wengine.

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Waziri badala ya kuhakikiwa mashamba haya wale wote ambao kwamba walikuwa wakiyatunza mashamba haya warejewe kwa utaratibu mzuri na tayari wapewe kumiliki lakini isiwe kama kupewa kwa sababu kuna wengine huwa ni watarazakuna wakiwepa tawi wanachukua na lile shina kwamba ndio hao waliokuwa wakiuza mashamba. Hivyo, imani yangu ni kwamba wakifahamishwa wataweza kujua na wataweza kukaa na mashamba haya vizuri, ili kuhakikisha kwamba serikali inapata mapato yake.

Mhe. Mwenyekiti, mkulima wa karafuu kwa tunavyodhibiti magendo nina imani hatathubutu kuchuma karafuu halafu akaiuza kinyemela, kwa sababu tayari atachuma karafuu na atapeleka *ZSTC* kila sehemu sasa hivi kuna vituo vya kununulia karafuu. Kwa hivyo, naiomba sana wizara kwa sababu lengo ni kuyajua mashamba haya na si kama wanavyopotosha huko mitaani, kwa sababu kuna waliokuwa hawaitakii mema nchi yetu, wanasema kwamba mashamba ya mikarafuu wakulima wamenyanganywa.

Kwa kweli, hilo sio lengo hawakunyanganywa mimi naunga mkono kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar pia alisema mpaka kule Makonyo kwamba hawakunyanganywa, lengo ni kuyatambua ili yajuulikane lakini nina imani kwamba mashamba haya yatarejeshwa. Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Waziri kupitia wizara yako badala ya kuyahakiki mashamba haya wale wenyewe warejeshewe, ili waendelee kuyaenzi na kuyatunza.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye ukurasa 30 kuhusu suala la wafugaji samaki.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze sana wizara kwa kuhakikisha kwamba wafugaji samaki wamepewa taaluma na mimi hilo nathibitisha ni kweli, kwa sababu ndani ya jimbo langu Shehia ya Ndagoni wanafuga samaki na walikuja pale Maruhubi, Nyangumi *House* wakapata mafunzo pale kama mwezi mzima. Kwa hiyo, naiomba sana wizara kuhakikisha kwamba ufugaji samaki uendelezwe kwa sababu tayari watu wapo tayari kuhakikisha kwamba wanafuga samaki, pweza, chaza na mambo mengine. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini niende kwenye suala la uvuvi haramu imeelezewa hapa suala la uvuvi haramu. Mhe. Mwenyekiti, kuna uvuvi haramu unatuathiri kama vile utupa, nyavu za kukokota na mambo mengine. Lakini Mhe. Mwenyekiti, huyo mvuvi lengo ni kufika bahari kuu, bahari kuu atafikaje apate chombo cha uhakika cha kuweza kufika bahari kuu. Mhe. Mwenyekiti, kuna uvuvi unaitwa dhulmati pengine wengine hawaufahamu humu, lakini uvuvi ule wa dhulmati unavuliwa bahari kuu. Kuna uvuvi wa nyavu za jarufe unavuliwa bahari kuu.

Kwa maana hiyo, wale wavuvi wakipatiwa vyanzo hivi vya kuvua kwa bahari kuu basi mimi nina imani wataondokana na uvuvi haramu. Kwa hiyo, naiomba sana wizara wahakikishe waweze kuwapatia wavuvi vyombo vya uhakika ili kuweza kufika kule bahari kuu na waache kuvua kuvua uvuvi haramu wa mabomu na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana mheshimiwa kwa mchango wako sasa naomba nimpe dakika tano Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi na baadae atafuatiwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na baadae nitampisha Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na mwisho kabisa atatumalizia Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya mwisho mwisho na mimi kuchangia kwenye mada hii iliyowasilishwa na Wizara ya

Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, inayohusika na chakula, ndio maana chakula chote kinatokana na uzalishaji wa kilimo dunia nzima hii.

Kwanza kabisa kidogo niseme jambo lilonigusa kwamba mwenzangu hapa alichangia, alikuwa anachangia vizuri baadaye akaja akatoa maneno ambayo kwa kweli si ya kuridhisha. Kwa kweli, yamenivunja moyo sana nasema lakini namuomba Mwenyezi Mungu na mimi asinielekeze nikasema maneno kama yale hata nikiwa na jazba za aina gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa kuanza kuchangia nimesema kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa dunia nzima, kilimo ndio kinachotupa chakula. Ukitizama hapa mavazi tuliyovaa, chakula tulichokula chote kinatoka kwenye kilimo, hata hivyo viwanda vinavyotayarisha vyakula vinapata *raw material* kutoka kilimo chenyewe. Kwa hiyo, kilimo ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nimeangalia haya maagizo takriban yote kabisa halafu nikaangalia na mikakati yote iliyoelezwa humu ambayo wameleta malengo malengo 18, yote yanalenga kwenye kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula ambayo ni nzuri sana. Nasema uzalishaji hauwezi kuwepo wa kutosha kama hakuna jambo la kwanza kabisa utafiti. Jambo la pili elimu ya ugani, la tatu ambalo ni la maumbile mazingira yetu. Haya mazingira haya kuwe na misitu ilete mvua, kuwe na nini mambo yote yanayohusika na mazingira ambayo yatakuwa ni rafiki kwa mazao kuota vizuri, basi hayo mazingira hayo yanatakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tukiangalia uzalishaji wetu unavyokwenda na vile unavyokuwa kidogo haujaenda kwa ile kasi ambayo itatuwezesha tujitosheleze kwa chakula kwa kipindi pengine cha miaka mitano au kumi ijayo tuna muda mrefu sana. Sasa kwa sababu, ili tuzalishe lazima kuwe na utafiti wa kutosha, na utafiti wa kilimo unaambatana na mambo ya kujaribu mazao mbali mbali, mbegu mbali mbali kuzijaribu ukaona ipi inafaa kumpelekea mkulima.

Mkulima anafanyiwa *demonstration plot*, sasa hivi *demonstration plot* zinamvutia mkulima anaoneshwa labda hapa pawekwa mbolea kiasi fulani, hapa panawekwa dawa kiasi fulani halafu anaona matokeo pamoja na huduma zote zile za mbolea. Sasa sidhani kama kuna *demonsration plot* zinazoendelea kwa sasa kama zipo zinaweza kuwa zipo lakini zinahitaji kuongezwa kasi ya *demonsration plot*, ili uzalishaji uongezeke.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni *training* wakulima wetu, ili wazalishe lazima wafundishwe hiyo elimu ya *organ* tunaita. Kuna mabwana shamba wengi sana nafikiri kila shehia takriban kila shehia kuna bwana shamba kwa hilo tumefanikiwa vizuri sana. Kwa hivyo, sasa kinachotakiwa hawa mabwana *organ* wapewe teknoloji ya kisasa ambayo ni *innovation* tunaita, ili waweze kusambaza kwa wakulima kwa wakati inavyotakiwa na wakulima.

Vile vile, hizi pembejeo zetu ambazo siku zote tunatumia mbolea na madawa, lakini mbolea siku zote ni *NPK* yaani ile mbolea ya *ammonia* upate *nitrogen*, kuna ile ya

calcium na ile ya *potassium* siku zote na inaitwa *blanket recommendation,*yaani popote hatuangalii udongo wa aina wala wa aina gani. Kwa kweli, weka gunia moja la mbolea chumvi chumvi, weka robo gunia ya mbolea ya *potassium*, weka nusu gunia ya mbolea nyengine hivyo tunakwenda. Sasa utafiti hautaki hivyo, utafiti unatakiwa kila aina ya udongo una *recommendation* zake a mbolea, ili uweze kufanikisha pamoja na hiyo *irrigation* ambayo mimea ipate maji ya kutosha ili iweze kuzalisha mazao ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi sidhani kama kuna tafiti za kutosha nasema tafiti za kutosha za udongo, zipo tafiti za udongo zinafanywa lakini sijui kama zinatosha kabisa kukidhi haja ya kutuwezesha na sisi tukaweza kuzalisha. Wenzetu wa sasa hivi wanaweza kuzalisha hekta moja tani 20 pengine na zaidi, lakini tuseme tani 20 za mpunga. Hivi sasa sisi nadhani kama tumefikia labda tani 8 au 10 *average*, bado tuko chini sana. Hivyo, ili tujitosheleze tunahitaji kuongeza bidii, kuongea tafiti nyingi sana ili tuweze kupata mazao mengi na bora.

Sasa nikiingia kwenye mazingira yetu ukiangalia historia ule msitu wa Jozani na wa Kiwengwa ulikuwa umekwenda moja kwa moja mpaka Nungwi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, dakika tano tayari.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwa kweli, nilichokusudia kusema ni kwamba misitu sasa hivi tunahifadhi vizuri lakini bado inakatwa, tujaribu sana kuhifadhi misitu yetu tuwaelimishe wananchi wasikate misitu tuwatafutie njia mbadala za kupikia ili hii misitu yetu isikatwe. Vile vile na sehemu ambamo si lazima kujenga wanaweza wakapewa sehemu nyengine, basi wapewe sehemu za kujenga muzuri misitu yetu iendelee kuota.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo muda tutakuwa nao huko mbele kuja kuchangia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kwa hiyo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii leo, ni nafasi ya mwisho lakini ni nafasi nzuri.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi. Lakini kwanza nimuombe radhi Mhe. Omar Seif Abeid nilikutaja kabla ya Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi. Kwa hiyo, naomba radhi kwa hili kutokana na muda, hivyo naomba mchango wako upeleke kwa maandishi. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa dakika tano. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru nitajitahidi niseme kwa dakika tano. Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako tukufu hili ni chombo kikubwa sana. Sisi Waheshimiwa Wajumbe tuliomo humu wananchi wanatusikiliza kwa makini maelezo yetu, tunavyochangia kwa maslahi yao na maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, lazima tuwe waangalifu sana na kauli zetu, hasa pale tunapowazungumza wenzetu ambao wao hawana nafasi ya kuingia humu ndani wala

hawana nafasi ya kujitetea. Kwa hivyo, ni vizuri sana maneno yetu yawe yana misingi ya kufuata kanuni na taatibu zetu tulizojiwekea katika Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, ni hivi juzi tu, wakati ukimaliza mjadala wa Wizara ya Mawasiliano, Ujenzi na Usafirishaji Mhe. Naibu Spika, alituwaidh na kututaka sana Waheshimiwa Wajumbe tujikite katika kuchangia taarifa zinazowasilishwa, ili tuweze kutoa mchango wetu vizuri kwa kufuata taratibu zetu za kikanuni, lakini kwa kusaidia wananchi wetu na maendeleo yetu. Kwa hiyo, tunapotamka baadhi ya maneno yanaweza kabisa kutuondoa katika mstari ambao umekusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipo kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Tumefanya hivyo kwa kupitia misingi ya kidemokrasia mpaka kufikia hatua hii ambayo leo sote tupo hapa ndani na si kwa njia nyengine yoyote, lakini kwa sababu ya katiba na sheria ndio iliyoweka serikali kwenye mamlaka. Tulishindana vyama vingi Chama cha Mapinduzi ndicho kilichokubalika na wengi kwa wananchi kikachaguliwa na serikali yake inafanya kazi ya kutekeleza Ilani hiyo na kwa umakini mkubwa mawaziri wote wanafanya kazi zao vizuri kwa misingi ya katiba, sheria, kanuni na maelekezo yanayotolewa na serikali. *(Makofi)*

Naamini wajumbe wengi humu ndani wanaridhika na utendaji kazi kwa mawaziri na serikali kwa ujumla wake, na ndio maana taarifa zetu tunazoleta hapa, kwa kiasi kikubwa Waheshimiwa Wajumbe wamezipitisha vizuri sana na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sisi tutaendelea kushirikiana vyema na Baraza hili tukufu, ili kutekeleza kazi zetu kwa umakini mkubwa na kufuata misingi na taratibu zilizowekwa na kuhakikisha kwamba tunatoa huduma bora kwa wananchi. Lakini tungewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe baadhi yetu tuangalie sana kauli zetu, kwa sababu maelezo mengine yanaweza kutoa tafsiri tafauti na yakaharibu sura nzima ya nchi yetu. Kwa hiyo, hiki ni chombo kikubwa tuna wajibu sote kwa pamoja kutekeleza majukumu yetu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, sisi kwa upande wa serikali tunawahakikishia chombo hiki kitukufu na wananchi wote wa Zanzibar kwamba mambo yetu yatakwenda kwa kufuata katiba ya nchi, sheria na kutekeleza wajibu wetu kama unavyoelekezwa na serikali. Kwa msingi huo, tutaendelea kufanya kazi zetu kwa umakini mkubwa, kwa busara na kutekeleza yale yote yenye maslahi ya wananchi na nchi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, sasa naomba nimwite Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na uzingatie muda kwa sababu nitakupa dakika tano na dakika kumi zilizobaki tutamuachia Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana. Nimpongeze sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa

mashirikiano yao katika utekelezaji wetu wa kazi hizi za Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Moja kwa moja niende katika masuala ya kilimo kuhusiana na mchele.

Mhe. Mwenyekiti, mchele unapatikana katika wizara yetu kuna duka letu pale, mkulima huyu ana uwezo wa kuzalisha tani 5 itategemea na mpunga jinsi vile anavyoupata. Tumpongeze sana Mhe. Naibu Katibu anayehusiana na mambo ya kilimo kwa kutoa msaada mkubwa kumsaidia kijana huyu kuweza kupata mashine hii ya kukobolea mpunga.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye wakulima ambao wanamwagilia maji. Kuna Mhe. Mjumbe alisema kwamba labda tumewasahau wale ambao wanatumia mvua. Hatukuwasahau lakini hawa wa umwagiliaji maji kilimo chao kinaanza mwanzo halafu ndio wanafuata hawa wa mvua. Kwa hiyo, mwanzo tunawapa wao halafu baadae watafuata wale wa mvua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niondoke hapo kwenye kilimo niende moja kwa moja kwenye mifugo. Vijana ambao tumewapatia elimu hii ya mifugo ni vijana 204 kwa kupitia mradi wa *ASP*, *ASPDL*, vile vile vijana hawa wanajisaidia binafsi kwani ni ajira zao wenyewe na kuwa kama wamejiajiri kupitia wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, niondoke hapo niende kwenye maliasili. Maliasili bado tuna changamoto kubwa sana kuhusiana na misitu, bado wananchi hawataki kukubaliana na zile taratibu ambazo tumewawekea, bado uharibifu wa misitu ni mkubwa sana. Kwa hiyo, nitoe wito kwa wananchi pamoja na Wawakilishi wa Baraza hili tuweze kusaidiana katika kutunza misitu hii ambayo inazunguka katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye uvuvi. Uvuvi tuna vyombo ambavyo tumevisajili, mnamo tarehe 28/9/2017 tulizindua rasmi ukaguzi wa vyombo vya Bahari Kuu ambavyo vitavua hapa. Vijana wetu ni kweli wamebahatika kupata nafasi za kazi mule na hawa Kichina hawajui lakini wanasaidiwa na yupo mmoja ambaye anajua kuzungumza Kiingereza kwa hivyo wanasaidiwa katika lugha ya Kiingereza.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumtaarifu Mhe. Mjumbe kwamba, kuhusiana na samaki wa kufuga. Samaki hawa hawana athari yoyote kiafya ikiwa watafugwa kwa utaratibu unaofaa. Vile vile wana *taste* kama samaki ambao tunawavua baharini.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Mhe. Mjumbe aliomba lini nitakuwa na nafasi ya kwenda naye ziara katika jimbo lake la Chaani. Mimi niko tayari muda wowote yeye tu, nitakwenda na wataalamu wangu wa kilimo, ili tuweze kuona tunasaidia vipi wananchi hawa wa Chaani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa ajili ya kutoa ufafaunuzi juu ya hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru na niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe waliopata fursa ya kuchangia na wale waliopata nafasi ya kusikiliza.

Mhe. Mwenyekiti, waliochangia kwanza nimshukuru sana na naomba niwatambe kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamad Abdalla Rashid kwa kazi nzuri aliyoifanya kuwasilisha ripoti kwa niaba ya kamati.
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
4. Mhe. Miraji Khamis Mussa
5. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
6. Mhe. Hamza Hassan Juma
7. Mhe. Suleiman Makame Ali
8. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
9. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
10. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
11. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na
12. Mhe. Naibu Waziri wa Afya amechangia kwa maandishi na kama kuna mtu nimemsahau naomba radhi sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya muda hoja zilizotolewa ni za msingi sana nataka niseme tu kwamba kwa niaba ya serikali ambayo tunaiwakilisha hapa tunazipokea. Lakini nataka niseme mambo matatu. *(Makofi)*

La kwanza, sote tunafanya kazi hapa zaidi tukitizama Ilani ya Uchaguzi wa CCM ambayo ndio iliyoingia madarakani kwa kupitia ilani hiyo ya uchaguzi, na anayesimamia ni Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nataka niseme kama kuna mtu anafanya kazi kwa uadilifu mkubwa sana kwa moyo wa kujituma na upenzi mkubwa sana, na Mwenyezi Mungu ndiye aliyemchagua kushika madaraka, si tume, si chochote Mwenyezi Mungu ndiye anayepanga nani ashike madaraka. Mimi na wewe tuko hapa lakini Mwenyezi Mungu aliyepanga kushika madaraka, uki-*question* hiyo una-*question authority* ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyeikiti, sisi tumepitia Mwenyezi Mungu ametuteuwa tufanye hiyo kazi yake, tumeifanya kwa uadilifu, tumepata kiondozi muadilifu anafanya kazi kwa uadilifu pamoja na yule ambaye yumo humu ndani, basi mchakato ni huo huo. Kwa kweli, naomba sana hili jambo tuliheshimu sana ni jambo linatokana na Mwenyezi Mungu wenzetu wengine wanatangaza kuapishwa kila siku asubuhi hawajaapishwa, kwa sababu Mwenyezi Mungu hakuwachagua, hilo tu Mwenyezi Mungu hajawachagua. Uongozi unatokana na Mwenyezi Mungu someni aya za *Qur-an* ziko *very clear*. *(Makofi)*

Kwa hivyo, mimi nasema Mhe. Mwenyekiti, tusichanganye maneno. Lakini tujue wenzetu wengine mnatokana na vyama vyenu na mimi natokana na chama changu, huwezi ukakibeza chama chako kilichokufikisha kwenye madaraka, mana unapo-*question* uteuzi wowote ule ambao na wewe ni sehemu yake maana yake una-*question legality* ya chama chako na *authority* ya chama chako si sahihi hata kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa Wajumbe tuwe na tahadhari, tumeingia kwa sababu ya nafasi za chama tulichokipata ambacho tumekikubali wenyewe. Nataka niseme hili kwa sababu kwa uzoefu wangu nafaa kutoa wasia wakati mwengine kwa mambo kama haya makubwa yanapotokea. *(Makofi)*

Pili Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba Waheshimiwa Wajumbe wamesema mambo mengi sana na ya msingi, mengine ni ushauri mzuri sana. Tumepata ushauri wa Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi hapa mambo ya mbolea kwamba tuangalie udongo na kadhalika, tumepata ushauri wa namna gani *zero grazing* tufanye na kadhilika, ushauri wa kila aina. Kwa dakika 20 Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nitakuwa siufanyii haki ukumbi huu, ila niseme mambo mawili makubwa ambayo yameguswa sana.

Kwanza ni suala la mchanga. Mhe. Rais wa Zanzibar amelitolea maamuzi, amelitolea msimamo wa serikali. Makamo wa Pili Rais hapa ndani ya Baraza hili amefanya kazi hii, mimi nimefanya kazi hii, ndiyo tukasema katika *exercise* tunayoendelea nayo sasa hivi bado serikali itaendelea kutoa taaluma na kuelimisha. Waheshimiwa Wajumbe tukimaliza *processes* ya kupeleka kwenye Baraza la Mapinduzi tutakuja tena kwenye Baraza hili tutakuelezeni *latest position* juu ya mchanga wala msiwe na wasi wasi kama kamati ilivyoagiza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, la msingi tujue tu kama rasilimali hii haipo, hili neno nataka nilirudie na Mhe. Rais wa Zanzibar alilisema vizuri katika ziara zake Mkoa wa Kaskazini. Alisema na akatoa mifano kwamba hata Mombasa leo hawana mchanga, Ghana hawana mchanga, duniani kote ukenda kwenye mitandao unakuta kuna *crises* kubwa sana ya mchanga, kwa sababu matumizi ya mchanga yamebadilika sasa wanatumia hata kwenye kuchimbia mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza tukubali kwamba (*resource*) rasilimali haipo, tunahitaji kujipanga na serikali imejipanga itakuja itatoa maelezo ya kina namna gani ilivyojipanga katika suala zima la kuendelea na sekta ya mchanga. Hilo naomba tukubaliane kabisa wala msiwe na wasisi wasisi wowote Waheshimiwa Wajumbe tutakuja hapa tutakaa pamoja tutalitatua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, matatizo ambayo yanatokea ndani ya utekelezaji kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma tuko tayari wakati wowote njooni ofisini tukae pamoja, kama kuna kasoro ya kiutekelezaji ni kasoro za kibinaadamu tutazitatua kwa pamoja hilo nimesema niliseme.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mbolea kwamba kampuni iliyokuja pale wakati ule ikaleta mbolea, siyo mbolea ilikuwa ni mbegu mbovu na kampuni inaitwa Hanzwaa. Kampuni ya Bajuta tunataka tuishukuru sana kwa miaka minne mfululizo imeikopesha serikali mpaka inadai serikali 3,069,000,000/=, ilivumilia muda mrefu sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa mara ya kwanza tulikuwa tunapata mbolea asilimia 15 mpaka 20 ya mahitaji. Kwa mara ya kwanza Mhe. Rais wa Zanzibar mara hii ameagiza tupate mbolea na pembejeo zote kwa asilimia isiyopungua 50. Kwa kweli, hiyo imetokana na wale waliowahi kuonja mchele mara hii na nawakaribisha waje pale kwenye duka la kilimo wanunue mchele ambao ni mtamu sana unashinda wa Mbeya, waje waone kazi ambayo aliyoifanya Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kusimamia wizara hii tukahakikisha wakulima wetu wanazalisha vizuri, wanazidisha chakula vizuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo nilikuwa nawakulima kutoka Tumbatu, wanasema kwa mara ya kwanza wana magunia matano, sita, kumi ya mpunga ndani ya nyumba zao ni mafanikio makubwa sana. Kwa hivyo, nasema serikali imejipanga vizuri katika hili jambo la kusimamia kilimo na mimi nataka niwakaribishe Waheshimiwa Wajumbe hapa muje tarehe 10 kwenye siku ya Chakula Duniani kwenye Maonesho ya Kizimbani, muone hizo mnazosema *pilot project* tunazozifanya *demonstration farm* tunazozifanya, lakini kazi kubwa tujue ni sisi wananchi kazi yetu kufanya sio wizara kufanya.

Kazi ya wizara kubwa ni kusimamia *policy*, taratibu na taaluma kwa wananchi wafanyaji ni wananchi wenyewe siyo sisi hata kidogo, kwanza hilo tulielewe. Lakini serikali vile vile ilijiondoa katika kufanya biashara. Maana tumekuwa *questioned* hapa ooh! kwa nini hamjatekeza *ZAFICO* na nini. Tulikubaliana kabisa Mashirika ya Umma yamalizike muda wake twende katika sekta binafsi kuziimarisha. Mhe. Mwenyekiti, wasome vizuri kwenye Ilani ya Uchuguzi ya CCM inasema nini.

Hivyo, ndio maana serikali kwa kuona kwamba baadhi ya maeneo mengine hatujafanya vizuri tukaanzisha Kampuni ya Uvuvi sasa hivi, ni kwa sababu pale ambapo tunaona bado sekta binafsi haijachukuwa *role* na mahitaji ya wananchi ya yapo serikali ndio inachukua hatua ku-*intervene***.** Itakapofikia pahala *ZAFICO* tumekosa chakula cha mifugo hapatikani mtu serikali itachukuwa jukumu ya kufanya hivyo, ili kuhakikisha kabisa chakula cha kuku na mifugo kinapatikana.

Kwa hiyo, nasema serikali kwa upande mmoja inaendelea na kushajihisha kufanya sekta binafsi ishiriki pale inaposhindika serikali itatunza wajibu wake, ili kuwaondolewa wananchi shida ambazo wanazo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, niseme ni kweli mahitaji ya mchele ni makubwa lakini nataka niwashukuru sana wakulima. Kwa mara ya kwanza tumeshuhudia baadhi ya wakulima wamevuna si chini ya tani 3,5,6 mpaka 8 wengine kwa kutumia taalum ya Shadid. Jambo la msingi lililopo ni kwamba wananchi lazima wabadilike wakubali kutumia teknolojia za kisasa, wakubali kusikilizam taaluma ili waweze kupiga hatua na nina mfano ulio hai.

Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda kwenye bonde la Bumbwisudi na Mhe. Mwakilini hapa mmoja, jirani yao walikubali kufata taalum wamevuna vizuri, jirani hakufanya utaalamu kavuna vibaya, mashamba ya sehemu moja. Kwa hivyo, kama mkulima akikubali kufuata utaalam nahakikisha kabisa mambo haya yataweza kubadilika.

Jengine ambalo Mhe. Mwenyekiti, niseme haraka haraka ni suala la mifugo. Kweli kweli, kabisa katika Sekta ya Mifugo bado hatujenda vizuri sana, lakini tumefanya programu moja nzuri sana kopa ng'ombe, lipa ngombe. Pale tulipozungumzia *Zero Grazing* tayari tuna wafugaji wasiopungua 300 ambao wako katika ufugaji wa lipa ng'ombe, fuga ng'ombe wako katika *Zero Grazing*. Huu mradi bahati mbaya ulimalizika kati kati. Hata hivyo, hivi sasa kwa kushirikiana na Benki ya Kilimo tunaurudisha tena badala ya mkulima kukopa ng'ombe, akalipa ng'ombe, atakopa pesa anunue ng'ombe, alipe pesa na atapewa na *grace period* ndani yake.

Mhe. Mwenyekiti, najua muda wako unaniandama sana. Lakini nataka niseme haya makubwa la mchanga tutalishughulikia na taarifa itakuja mradi tuende kwenye *process* zile za serikali. Suala la mbolea kama nilivyosema Mhe. Rais wa Zanzibar amejitahidi sana tuweza angalau sisi kupata nusu naamini mazao yataonekana na asubuhi liliulizwa swala kama je, ahadi yangu ile la kujiuzulu ipo? Mhe. Mwenyekiti, narudia tena mimi namuani sana Mwenyezi Mungu na naamini kabisa Mwenyezi Mungu anasimama na uongozi ulio imara, meena mnazoziona zipo hizi hapa ni uadilifu na utiifu kwa Mwenyezi Mungu kwa Dkt. Ali Mohammed Shein na wafuasi wake. (*Makofi*)

Tuna kila sababu ya kujivuna mazao ya pembeleo ya chakula mara hii mengi, mazao ya matunda tulikuwa tunaagizia asilimia 80 kutoka Bara sasa tunaagizia asilimia 20, mazao ya karafuu mara hii hata hayasemeki. Kila neema Mwenyezi Mungu katupa iliyobakia ni hasada ambayo ipo na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ataijaalia itashindwa hivi karibuni. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili Mifugo na Uvuvi. Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na ripoti ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi wanyanyue mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe)*

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, namshukuru sana Mwenyezi Mungu lakini pia nimpongeza Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na watendaji wake wote pamoja na Wenyeviti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi kwa ripoti zao. Lakini pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa utulivu kwa muda wote tuliokuwepo hapa naomba niakhirishe kikao mpaka kesho saa 3 asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 6/10/2017 saa 3: 00 asubuhi)